ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Tano – Tarehe 29 Machi, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba nikupeni taarifa kwamba jana tumekuwa na wageni kutoka Bunge la Uganda ambao tunategemea si muda mkubwa baadae watakuwepo pale kwenye *seat of gallery* na mara wakifika watapisha pale mazungumzo yetu yalipofika kwenye maswali halafu tutawataja kwa heshima ya wageni hao. Hivi sasa bado wanajitayarisha watakuja na wakiingia tu basi nitaomba nichukue nafasi ya kuwataja ili tuweze kusalimiana nao kama kawaida. Ahsante sana.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 89

Serikali Kuongeza Kima cha Chini cha Mshahara

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza**:-**

Ndani ya Afrika ya Mashariki, Zanzibar ni nchi pekee ambayo wafanyakazi walio wengi hasa wa Serikali wanalipwa mishahara midogo sana pamoja na hali ngumu ya maisha.

Je, Serikali imejipanga vipi kwa Bajeti inayokuja ya mwaka 2011-2012 angalau mfanyakazi wa ngazi ya chini akalipwa TShs. 200,000/= ili aweze kumudu hali ngumu ya maisha inayotukabili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kwanza naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, kiwango cha mishahara hasa kima cha chini katika nchi nyingi za Afrika Mashariki ni kidogo na sio kwa Zanzibar peke yake. Hali hii inatokana na wigo mdogo wa ukuaji wa uchumi wa nchi hizo ambao hupelekea pia

mapato ya Serikali kuwa madogo ukilinganisha na mahitaji ya nchi hizo. Nikitoa mfano Mhe. Spika, kima cha chini cha mishahara kwa mwaka kwa baadhi ya nchi za Afrika ya Mashariki ni kama ifuatavyo:-

i) Kenya ni dola za Kimarekani 830
ii) Rwanda ni dola za Kimarekani 496
iii) Tanzania Bara ni dola za Kimarekani 1080
iv) Zanzibar ni dola za Kimarekani 800

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 89 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inalifahamu suala la udogo wa kima cha chini cha mshahara na inalifanyia kazi. Udogo wa kima cha chini cha mshahara unatokana na uchache wa mapato ya serikali ukilinganisha na mahitaji yetu. Ili kuondokana na hali hiyo ya kima kidogo cha chini cha mshahara serikali imeandaa mkakati wa kuongeza mapato na hatimaye kuongeza mishahara kila hali ya mapato itakapokuwa nzuri.

Mhe. Spika, jukumu la kutaja kima cha chini cha mshahara ni la wizara inayohusika na masuala ya Utumishi wa Umma Serikalini. Ni matarajio yangu wakati ukifika waziri husika atatutangazia kima cha chini ambacho nina imani kitapunguza hali ngumu ya maisha.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzibar kwa muda mrefu ilikuwa ikitangaza viwango vya mishahara kwa kuanzia hichi kiwango cha chini na wakati huo huo ndio vinatangazwa viwango vya mishahara kwa wataalam. Kwa kuwa swali langu lili-*base* kuwa kiwango cha chini cha mshahara kulingana na viwango vyengine vyote vinavyopanda vya wataalam.

(a) Je, Mhe. Waziri, haoni kutokana na hali inavyokwenda kwamba tukiendelea na hali hii tutakuwa tunatumia pakacha wataalam wetu watakuwa hawapo tena na badala yake tutabakia hatuna pakwenda.
(b) Kwa kuwa Mhe. Waziri alikiri kwamba Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndio ambaye angetangaza kiwango cha chini cha mishahara. Je, uchumi wake unaruhusu au ni ukorofi wa waziri tu hajatangaza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, nataka niseme tu kwamba katika upandishaji wa mishahara na

hasa ambao tunataka tuufanye kwa kupitia Serikali ya Umoja wa Kitaifa tutazingatia vile vile viwango vya mishahara ya wataalam, ili wataalam wetu waweze kubakia nchini na kuweza kutekeleza majukumu yao. Namuomba Mhe. Mwakilishi avute subira itakapofika wakati wa bajeti atasikia vile vile viwango vya wataalam vya mishahara.

Mhe. Spika, swali (b) nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba si ukorofi wa Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika hali nzima ya kupandisha mishahara. Ni hali yetu ya mapato ukilinganisha na mahitaji yetu. Pale mapato yanapokuwa mazuri nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma tutahakikisha kwamba maslahi ya wafanyakazi wetu nayo yanaimarishwa.

Mhe. Spika: Nashukuru Mawaziri wangu hakuna mkorofi hata mmoja.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi amesema kwamba kima cha chini cha mshahara katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni dola 800 kama sikosei. Je, Mhe. Waziri, dola 800 ni sawa sawa na kiasi gani cha pesa za Tanzania.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka niiweke sawa ili isije ikakaa katika *hansard* pamoja na vyombo vya habari. Mhe. Spika, kima cha chini nilichokitaja hapa ni kwa mwaka. Ili uweze kulinganisha vima vya chini kwa nchi mbali mbali lazima uvipeleke katika *unit* moja ndio kwa maana nikavipeleka vyote katika *unit* ya dola. Kwa sababu shilingi ya Kenya ni tofauti na shilingi ya Tanzania na halikadhalika. Kwa hivyo, vyote ili niweze kuvilinganisha nimevipeleka kwa dola.

Mhe. Spika, kima cha chini kwa mwaka kwa Zanzibar nimesema ni dola 800. Ukitaka kwa shilingi dola 800 zidisha mara 1,500 utapata shilingi kwa mwaka, ukitaka kwa mwezi gawa kwa 12.

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niliahidi kwamba si muda mkubwa wageni wetu Waheshimiwa Wabunge kutoka Bunge la Uganda ambao wengi wao ni Makamishna wa Tume ya Bunge pale Uganda ndio wanaofanya mambo mbali mbali ya *jurisdiction* na uongozi, mambo ya kifedha katika Bunge la Uganda watafika si muda mkubwa. Pia niliahidi kwamba wakishafika basi nitawajulisha ili tuweze kusalimiana nao.

I have the pleasure now to welcome our guests, our colleagues from the Parliament of Uganda as follows. I mention their names, some of the names are a little bit not easy to pronounce, but I apologize If I make mistake because the names are not very familiar to me.

Our colleagues who sit in the gallery right now are Hon. Daudi Migereko - Minister Government Chief Whip yule pale, thank you. Followed by Hon. Justine Lumumba - Parliamentary Commissioner, thank you. Hon. Lawrence Akweu Ibi – Commissioner, thank you so much. Followed by Hon. Denis Hamson Obua – Commissioner, thank you so much. Others are Mr. Benson Masereka – Principal Assistant Secretary of the Parliament of Uganda, thank you. Followed by Deborah Akube Okoropor, thank you very much. Followed by Mr. Paul Musamali Mwasa – Personal Assistant to Government Chief Whip.

I have the pleasure and very much delightful to welcome you all to the House of Representatives to observe our session this morning. It is the question session now. Thank you.

Wageni wetu wengine ni Serikali ya Wanafunzi wa Skuli ya Sekondari ya Kiembesamaki naomba kwa pamoja wasimame, wale pale. Vijana wetu nao wamependa kuja kuona wazee wao wanafanya nini ili ndio vizazi vipya baadae tuwaachie wao nao waendeleze. Nakushukuruni sana. *Thank you so much indeed our guests.*

Nam. 68

Wito wa Kuongeza Bei ya Kununulia Zao la Karafuu

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad - Aliuliza**:-**

Wakulima wa zao la karafuu wamekuwa na malalamiko makubwa kuhusiana na bei ya zao hilo kuwa ni ndogo pale wanapouza karafuu zao Serikalini, ukilinganisha na bei wanayopata wanapouza katika masoko yasiyo rasmi.

(a) Serikali ina kauli gani kwa wakulima wa karafuu juu ya kilio chao cha muda mrefu kuhusu bei ya kununulia zao hilo kuwa ndogo.

(b) Ni kwa nini Serikali haitoi ruhusa kwa wananchi kuuza karafuu hizo mahali popote wapendapo kama ilivyo kwa bidhaa nyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 naomba kutoa utangulizi ufuatao:-

Mhe. Spika, kupitia kwako kwanza naomba niwakumbushe ndugu zangu wakulima wa karafuu lakini pia na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba bado zao la karafuu ni tegemeo kubwa kwa uchumi na ustawi wa maendeleo ya nchi yetu. Hivyo kulinganisha bei inayotokana na mauzo ya karafuu katika masoko yasiyo rasmi na ile wanayoiata katika Serikali si kigezo sahihi kwa kuwa bei ya masoko yasiyo rasmi hufikiwa baada ya kukiukwa taratibu mbali mbali za kisheria kama vile kuepuka ukaguzi wa ubora na sifa za karafuu zenyewe au hata kukwepa ushuru wa Serikali pale karafuu hizo zinaposafirishwa kwa njia ya magendo.

Mhe. Spika, sifa tuliyojijengea Zanzibar katika masoko ya nje ni ubora na usafi wa karafuu zetu. Lakini taratibu zinapokiukwa kwa kujali manufaa ya wachache inapelekea kuondoa sifa ya karafuu zetu na hivyo bei nzuri tunayoipata huenda isipatikane na kupoteza sifa.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali wakati wowote imekuwa ikizingatia bei ya zao hilo kwa wakulima kulingana na bei ya soko na haikusita kuwaongezea bei wakulima pale bei ya soko inapokuwa nzuri. Uthibitisho wa hayo ni namna Serikali ilivyowapandishia bei wakulima katika msimu huu wa mwaka 2010/2011. Serikali iliweka bei ya Tshs. 3,500/-, Tshs. 3,000/- na Tshs. 2,000/- kwa kilo kwa daraja la kwanza, la pili na la tatu pale ilipofungua masoko yake tarehe 12 Julai, 2010.

Mhe. Spika, miezi mitano baadae yaani tarehe 22 Novemba, 2010 Serikali iliwapandishia bei wakulima kutoka bei zilizotolewa mwanzo na kuweka bei mpya ya Tshs. 4,000/-, Tshs. 3,500/-, na Tshs. 3,000/- kwa kilo kwa daraja la kwanza, la pili na la tatu. Kwa kuzingatia misingi iliyokwisha elezewa ya kuwaongezea bei wakulima kwa kadri ya hali ya soko duniani litakaporuhusu, Serikali haikusita kuwaongezea tena bei wakulima na hivyo tarehe 01 Januari, 2011 bei ikaongezwa kutoka ile ya Tshs. 4,000/- na kuwekwa ya Tshs. 5,000/-, Tshs. 4,000/- na Tshs. 3,000/- kwa kilo bei ambayo hadi sasa ndio bei inayoendelea kutumika.

(b) Serikali kufikia hatua hiyo ya kutoa ruhusa kwa wananchi/wakulima kuuza karafuu hizo mahali popote wapendapo, na hasa tukizingatia kuwa zao hilo bado ni mhimili mkuu wa uchumi wa nchi ni jambo linalopaswa kuangaliwa kwa umakini mkubwa sana ili kupeuka matatizo mbali mbali kama ambavyo yaliyowahi kujitokeza kwa bidhaa nyengine ambazo huko nyuma udhibiti wake ulikuwa chini ya Serikali. Kwa makini sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inalifanyia kazi suala hili na endapo itaona ipo fursa ya kufanya hivyo haitosita kuchukua hatua muafaka.

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe waelewe kuwa ni wajibu wa Serikali kuona hatua yoyote inayoichukua basi iwe ni kwa maslahi ya nchi na wananchi wake wote kwa jumla na si kwa ajili ya kuwanufaisha watu wachache.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, tunavyofahamu kwamba karafuu katika miaka ya nyuma zilikuwa ni tegemeo la serikali kwa vile Bajeti ya Serikali kwa sehemu kubwa ilikuwa ikitegemea Shirika la Biashara la Taifa *(ZSTC).* Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba bado karafuu ni tegemeo la uchumi.

(a) Je, Mhe. Waziri anaweza akalieleza Baraza hili ni kwa kiasi gain hivi sasa serikali inapata kutokana na karafuu.
(b) Ikiwa shirika halichangii ni utegemezi gani huo ambao uchumi wetu unapata kutoka katika Shirika la *ZSTC*.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, katika jibu mama nimesema kwamba zao la karafuu bado ni tegemeo kubwa la uchumi na litaendelea kutegemewa katika uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, jibu (b) ni kwamba *ZSTC* bado inaendelea kununua karafuu kutoka kwa wananchi ikiwa ni Shirika la Serikali kwa sababu kwanza ya kuwalinda wakulima. Serikali inaponunua haiangalii soko la dunia, inakuwa ni *security* kwa wakulima. Lakini pindipo tutabinafsisha na kuchukuliwa na watu binafsi hawatonunua karafuu kama soko la dunia limekufa na hivyo tutawaacha wakulima na matatizo ya kutokununuliwa karafuu zao.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake kwamba zao la karafuu ni uti wa mgongo wa uchumi wetu na bado ni tegemeo kubwa.

Hivi karibuni kuna shirika linaitwa *Life Years* la Marekani limefanya uchunguzi kusikilizana na Tanzania na jinsi gani uwezekano wa kuzifanyia *branding* unaweza kusaidia kuziinua hadhi yake. Waligundua kwamba bei ya karafuu wakati hapa ndani kwa mkulima anapata wastani wa dola 2 na serikali kuuza nje kwa wastani wa dola 6. Lakini kwa wale *importers* wanapata takriban dola 102 na katika bei ya rejareja katika soko la dunia inauzwa karafuu ya Zanzibar kwa dola 128 kwa kilo.

(a) Sijui wizara inayo taarifa juu ya ripoti hii na ukweli huu uliokuwepo kuhusu bei ya karafuu.

(b) Kama inayo taarifa inachukua hatua gani ili kuona kwamba Zanzibar nayo inaingia katika utaratibu wa branding kama ilivyofanya nchi ya Ethiopia kwa kahawa yake, ili na sisi karafuu zetu ziweze kumnufaisha mkulima wetu na pia ziwe kweli uti wa mgongo wa uchumi wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kusaidia kutoa ufafanuzi juu ya suala lililoulizwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ripoti anayoizungumzia Mhe. Mwakilishi nataka nimhakikishie kwamba tunayo na sisi serikali tunaipitia tuweze kuona ukweli wake juu ya suala linalozungumzwa katika ripoti hiyo, ili kwa pamoja Wizara yangu inayosimamia masuala ya Uchumi na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tuweze kulifanyia kazi suala lililomo ndani ya ripoti hiyo.

Mhe. Spika, nataka niliarifu Baraza lako tukufu kwamba serikali tayari inafanyia kazi suala la *branding* na kuna timu ya wataalam tuliipeleka nchini Ethiopia kuweza kujifunza masuala mazima ya *branding*. Sasa hivi tunapitia ripoti yao na baadae tutaangalia ni maeneo gani na mazao gani tunaweza tukayafanyia *branding* likiwemo pendekezo la zao la karafuu.

Nam. 119

Matatizo ya Walimu Maskulini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Ni wazi kuwa katika visiwa vyetu vyote kuna tatizo kubwa la upungufu wa walimu hasa hasa walimu wa sayansi. Kwa upande mwengine Serikali inaonekana kuelekeza juhudi zake katika kuongeza majengo ya maskuli.

(a) Je, Mhe. Waziri, Serikali haioni kuwa kinachohitaji zaidi ni walimu wenye sifa kuliko majengo mengi na makubwa.

(b) Ni lini Serikali itaanza kufikiria mbinu muafaka za kuhakikisha kuwa matatizo yaliopo ya walimu na maslahi ya walimu yanafanyiwa kazi ipasavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 119 lenye vifungu (a) na (b) lakini kwanza napenda kutoa maelezo ya ufafanuzi kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kuwa skuli zetu nyingi zina uhaba wa walimu hasa wa masomo ya sayansi. Pia skuli zetu zina uhaba mkubwa wa madarasa kiasi kusababisha wanafunzi kusoma kwa mikondo miwili na pia kuwepo msongamano mkubwa wa wanafunzi madarasani.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, skuli zetu zinahitaji madarasa na walimu wenye uwezo kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi kila mwaka. Mambo yote mawili ni muhimu na ndio maana Wizara inachukua hatua ya kuyatatua mambo yote mawili kwa wakati mmoja. Haiwezekani kuandaa walimu na kusahau au kupuuza kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa walimu na wanafunzi. Miongoni mwa sababu zinazochangia utoro au walimu kutoipenda kazi ya ualimu ni mazingira duni ya sehemu za kufundishia.

(b) Mhe. Spika, Wizara siku zote inatafuta mbinu mbali mbali mpya za kutatua matatizo ya walimu na kuweza kuwapatia walimu maslahi mazuri zaidi. Miongoni mwa mbinu hizo ni pamoja na kujenga nyumba za walimu kwa ajili ya kuwawezesha walimu wazuri kuweza kuishi katika maeneo ambayo yana uhaba wa walimu, kuongeza huduma ya likizo za walimu na kuwapatia walimu fursa za kujiendeleza kielimu. Hata hivyo, utekelezaji wa mbinu hizo unategemea sana hali ya kiuchumi wa nchi yetu. Napenda kuwahakikishia walimu na wananchi kwa jumla kuwa Wizara inawajali walimu na wafanyakazi wake na itaendelea na juhudi za kuimarisha hadhi na maslahi ya walimu kwa kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza maswali matatu ya nyongeza. Mhe. Spika, bado Mhe. Naibu Waziri hajatueleza mbinu gani wizara inachukua ili kuweza kujitosheleza kwa walimu wenye uwezo.

Ni kiasi gani inahitaji walimu kwa mujibu wa tathmini ya wizara. Kwa vile umekiri kuwa kuna ukosefu wa walimu wa somo la sayansi, Jambiani ni miongoni mwa skuli zenye ukosefu mkubwa wa somo la sayansi, mwalimu wao amepata maafa au tuseme amepata ajali kwa kipindi cha miezi mitatu yuko hospitali amepasuka kichwa, sijui kama ameshatoka hospitali kwa kwa muda huu, sijui wizara yako suala hili inalionaje kuwapeleka walimu wa ziada na inahitaji siku ngapi.

Vile vile walimu na wazee wa Jambiani wameshawahi kumuona Mhe. Waziri wa Elimu kuhusu suala hili.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tunategemea maswali yenu yawe mafupi, ya moja kwa moja na yawe yanafahamika.

Sasa naona umekuwa ni mtiririko mrefu kama unachangia. Nadhani itoshe kwa hayo maswali mawili au matatu ulioiuliza. Kwa kweli sio zaidi ya mawili kwa mujibu wa kanuni ili tumruhusu Mhe. Naibu Waziri kujibu. Jibu maswali mawili kati ya yale aliyouliza kwa mujibu wa kanuni.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Spika, hatua ambazo tunachukua kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhakikisha kuwa tunapata walimu wengi wa sayansi. Moja ni wizara kwa kushirikiana na Chuo cha SUZA imeanzisha Diploma ya Sayansi ambayo hii itawasaidia wanafunzi wetu wengi kuchukua diploma hii na baadae wataweza kuwasaidia wanafunzi wetu. Pia mafunzo kazini kwa wafanyakazi.

Mhe. Spika, katika jitihada nyengine mara tu baada ya kutoka matokeo ya kidato cha sita mara hii tutaanzisha kozi maalum ya sayansi ya diploma katika vyuo vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, jana katika swali langu nambari 91 nilielezea ni namna gani wizara inajitayarisha na kuhakikisha kwamba walimu tunawaweka katika mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Miongoni mwa mambo ambayo niliyataja ni ile kueleza kuwa tuna skuli 13 ambazo tunazijenga za kisasa kabisa, na kila skuli kumi tuna ujenzi wa nyumba za walimu tatu tatu, ambapo nyumba hizo Mhe Spika, zikimalizika tutakuwa na uwezo wa kuchukua walimu wazuri na kuwapeleka katika skuli hizo, hususan walimu wa sayansi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi mpaka hivi leo hii maslahi ya walimu pamoja na pesa zao za posho kuwa hazijakamilishwa, na wewe unatuambia kwamba uko katika utaratibu wa kuweza kukamilisha.

Je, ni lini suala hili litaweza kukamilika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kuhusu maslahi na malimbikizo ya posho na madai ya walimu nadhani nililijibu juzi hapa katika swali mama.

Mhe. Spika: Rejea kumbukumbu za majibu hayo ambayo Mhe. Waziri alijibu. Waheshimiwa Wajumbe maswali ni mengi kidogo naomba tuendelee.

Nam. 87

Suala la Mafuta Kuondolewa Katika Orodha ya Mambo ya Muungano

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

Kwa kuwa Baraza la Wawakilishi la Saba, katika mwaka 2009 lilipitisha kwa kauli moja juu ya suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta liondolewe katika mambo ya Muungano na pia lilizungumziwa na Rais Mstaafu, Mhe. Amani Abeid Karume katika hotuba yake ya Sherehe za Mapinduzi Januari, 2010 katika Uwanja wa Gombani.

Kwa maslahi ya kuinua uchumi wa Zanzibar, Je Wizara imechukua hatua gani kuendeleza hatua hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 87 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa suala hili limo katika mchakato wa kuliondoa katika mambo ya Muungano na kwa sasa lipo katika ngazi za juu za maamuzi ya kikatiba.

Mhe. Spika, utakumbuka kuwa mwaka 2009, Baraza lako tukufu kwa kauli moja lilipitisha kuondolewa kwa suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta katika suala la Muungano. Changamoto iliopo sasa kwa wizara yangu ni kuandaa taasisi itakayojitegemea itakayoshughulikia masuala yote ya mafuta,

ikiwa pamoja na suala la uchimbaji na utafutaji wa mafuta. Aidha, wizara yangu tayari imeshapeleka masomoni vijana wa Kizanzibari kusomea fani mbali mbali za utafutaji wa mafuta. Vijana wengine wataondoka hivi karibuni.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa kuwa hivi karibuni tumesikia harakati kubwa Tanzania Bara za utafutaji wa mafuta. Katika ziara ya Mhe. Rais wa Tanzania aliyoifanya katika Wizara ya Nishati, alipewa taarifa kwamba tayari visima 17 vimeshachimbuliwa Tanzania Bara katika utafutaji wa mafuta, vikiwemo na vya gesi.

Kwa kuwa harakati hizo zinatutia ari ya kuona kwamba sisi tumebakia na kufunga mikono. Je wizara inaona vipi tubaki kufunga mikono au tutachukua hatua za kuyaita makampuni ili waje watafute mafuta.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongeza jibu la ziada, kutoka kwenye swali la Mhe. Mjumbe. Mhe. Spika, wizara haijakunja mikono na suala la kwamba Tanzania Bara utafiti unaendelea na visima kadhaa vimegundulikana. Mimi hilo silijui wala wizara yangu haina taarifa hiyo.

Mhe. Spika, ninalolijua mimi ni kwamba wizara yangu iko mbioni sana, kutafuta wataalamu kuangalia uwezekano wa kuwa na mafuta na gesi hapa Zanzibar, yaani Unguja na Pemba. Ziara yangu ya juzi katika nchi za Falme za Kiarabu inahusiana na harakati hizi, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nimpongeze Mhe. Waziri kwa kurudi safari yake kwa salama salmini. Baada ya shukrani hizo naomba niulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali lake, alisema suala hili lipo katika ngazi za juu kwa maamuzi. Naomba kujua kuna ngazi za juu hapa Zanzibar kuliko Baraza la Wawakilishi.

(b) Mhe. Spika, mwaka juzi mimi nilikuwa mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kwa busara zako ulinipeleka Songosongo, miongoni mwa watu walioshuhudia visima hivyo 17 vikiwa vya gesi na mafuta. Mhe. Waziri anasema leo kuwa wizara yake haina habari, anakusudia kutuambiwa kwamba hajapewa taarifa au watendaji wake ni wavivu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza suala la kwamba kuna visima 17 vya gesi vimeonekana huko Tanzania Bara, nilisema mimi wala wizara yangu haina habari hizo. Tuna habari za kusoma kwenye magazeti, hatuna habari za maandishi rasmi ambazo hizo ndio unaweza kuziita rasmi zenye uhakika.

Mhe. Spika, pili sisi hatufuatilii yanayofanywa na wenzetu Tanzania Bara. Sisi tunafanya yetu, kama nilivyokwisha kusema kuwa tuko mbioni sana na dalili ya kuwa kuna gesi na mafuta hapa Zanzibar, sasa hivi dalili hiyo haina mashaka ni sahihi kabisa.

Mhe. Spika, naomba arejee swali lake lile la kwanza. Nimejibu swali la pili, lakini la kwanza sikulisikia vizuri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, swali langu la kwanza nilisema kwamba Mhe. Naibu Waziri alisema suala hili la mafuta liko katika ngazi za juu kwa hatua zaidi. Naomba kujua, Je kuna ngazi ya juu zaidi hapa Zanzibar kuliko Baraza la Wawakilishi?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, maelezo yake haya nayakubali kwamba hakuna ngazi ya juu zaidi kuliko Baraza la Wawakilishi, lakini kauli ya Mhe. Naibu Waziri wangu aliyosema kwamba suala hili lipo katika ngazi ya juu, ni kwamba linazungumzwa katika ile kamati ya kuondosha makero ya Muungano na liko katika ngazi ya mawaziri na hivi karibuni mawaziri walikutana na wakajadili mambo mbali mbali likiwemo na hilo.

Lakini tunazingatia uwezekano wa kuliingiza suala hili katika mabadiliko ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hiyo ndio itakuwa ngazi sahihi, kwa sababu wabunge wetu walioko huko watapata nafasi ya kulizungumza na sisi tulioko huku tutapata nafasi ya kuwapa *feedback* ili wakilizungumza basi walizungumze kwa uhakika. Nia ya kulizungumza ipo, kwa sababu kauli za wakubwa zimetoka kwamba linazungumzika na kwa hivyo tutalizungumza.

Nam. 82

Serikali Kupunguza Kambi za Kijeshi za JWTZ Zilizopo Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Nalipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa umahiri wake wa kulinda mipaka na uhuru wa nchi ya Tanzania. Aidha, JWTZ limekuwa mstari wa mbele kwa ujenzi wa taifa hili pamoja na kutoa huduma mbali mbali kwa

wananchi wetu. Hata hivyo, pamoja na mazuri yote hayo, JWTZ limekabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo ile ya mlipuko wa mabomu.

Kwa mfano, milipuko ya mabomu ya mwaka 2005-Gongolamboto, mwaka 2008 katika kambi ya JWTZ-Mbagala na ile ya hivi karibuni ya tarehe 16/02/2011 iliyotokea tena katika Kambi ya Gongolamboto ambayo imesababisha vifo vya zaidi ya wananchi 20 na kujeruhi idadi kubwa ya wananchi.

(a) Kwa kuwa matokeo hayo yanaendelea kutokea, Je. Wizara inawafahamisha nini wananchi wa Zanzibar kuhusiana na sababu za matokeo hayo.

(b) Kwa kuwa milipuko hiyo ya mabomu husababisha maafa na kwa kuwa hatujui usalama wa kambi nyengine za JWTZ zilizopo nchini, Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hazioni kuwa kuna haja ya kuunda timu ya wataalamu kufanya ukaguzi wa usalama wa mabomu katika maghala yote ya JWTZ.

(c) Kwa kuwa Zanzibar ni nchi ndogo na ina vikosi vyake vya ulinzi wa ndani, Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika sasa wa kupunguza kambi za JWTZ hususan zile ziliopo Mjini Magharibi karibu na makaazi ya wananchi, ikiwa ni pamoja na Kambi ya Migombani, Welezo (Unguja), na Ali Khamis (Pemba).

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: (Kny: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais) - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kupokea pongezi alizozitoa Mhe. Mwakilishi kwa Jeshi letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wake wa kulinda mipaka na Uhuru wa nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya shukrani hizo sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa ulinzi wa taifa ni suala la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa baada tu ya tukio la miripuko ya mabomu, taasisi husika ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, lilitoa taarifa kwa vyombo vya habari *press relies* halikadhalika JWTZ

lilifanya mkutano na vyombo vya habari *press conference.* Aidha, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alitoa taarifa ya awali kuhusu tukio la miripuko katika Kambi ya Gongolamboto.

Pia viongozi wetu wa kitaifa waliotembelea eneo hilo, walitoa maelekezo mbali mbali kuhusiana na tukio hilo. Hivyo, hatua zote hizo zilikuwa na lengo la kufahamisha umma juu ya tukio hilo la ajali, pamoja na hatua ambazo zimechukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa.

Mhe. Spika, hata hivyo wizara imefuatilia suala hili na kupata taarifa kuhusu hali ya usalama kwa upade wa kambi za Jeshi la Wananchi wa Tanzania ziliopo Zanzibar na wahusika wametueleza kuwa hali ni shwari na salama.

(b) Mhe. Spika, napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia JWTZ, kutokana na tukio la miripuko ya mabomu Gongolamboto, tayari limeunda Baraza la Uchunguzi kuchunguza tukio hilo. Kulingana na aya ya 13.07 ya kanuni ya Jeshi la Ulinzi kama anavyofafanua, sehemu ya 9 ya sheria nambari 24 ya mwaka 1966, baraza hilo linaendelea na uchunguzi.

Aidha, wana usalama wa JWTZ nao wanaendelea na uchunguzi wa kiusalama ili kujiridhisha na kujua nini hasa chanzo kilichosababisha ajali hiyo. Vile vile timu ya wataalamu kutoka nchi rafiki, nayo inaendelea na uchunguzi kwa kushirikiana na Jeshi letu ili kusaidia jitihada za jeshi hilo.

(c) Mhe. Spika, kuhusu suala la kambi za JWTZ kuwa karibu na makaazi ya wananchi. Kambi za JWTZ hujengwa kwa ajili ya kukidhi mahitajio ya ulinzi wa nchi na taifa kwa jumla. Kinachofanyika sio kuhamisha makambi ya JWTZ bali ni kuhamisha miripuko iwe mbali na maeneo ya wananchi, pamoja na kujenga maghala ambayo hata mabomu yakiripuka yasiweze kutoa madhara kwa wananchi.

Shughuli hizo ni za gharama na zinahitaji fedha nyingi. Hatua za haraka zimeanza na zitafanyika katika mipango ya muda mfupi na muda mrefu kulingana na uwezo wa bajeti. Aidha, napenda kutoa wito kwa wananchi kuacha kujenga nyumba za makaazi, pamoja na kufanya shughuli nyengine karibu na makambi ya vikosi vya ulinzi na usalama.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Waziri amesema kwamba jeshi limeunda baraza la uchunguzi kwa ajili ya kupata usahihi wa kambi zetu. Naomba kujua ni muda gani taarifa ya jeshi itatoka kwa wananchi ili kujua usalama wa kambi zetu.

(b) Kwa kuwa kambi nyingi ziko katika maeneo ya watu, mbali na adhari za mabomu, hivi sasa na wanajeshi wamekuwa wakiingia mitaani na kuwapiga watu kama matukio ya Jang'ombe. Je, wewe kama Mhe. Waziri, una ushauri gani kwa kambi zetu kuziondosha katika miji ili kuondosha athari, mbali na mabomu, lakini hata kuwapiga watu bila ya sababu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: (Kny: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuhusu muda, kwa kuwa Baraza hili halikutoa muda maalum wa kumaliza kazi yake kutokana na mazingira yenyewe ya tukio na ukubwa wa tukio lenyewe.

(a) Mhe. Spika, namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba Baraza hili litafanyakazi kwa haraka iwezekanavyo kutokana na hali halisi ilivyo ili kuweza kujua chanzo cha tukio na hatua zitakazochukua katika kukabiliana na matukio kama haya, ili kupunguza athari za majanga ya aina hii huko mbele twendako.

(b) Mhe. Spika, kuhusu wanajeshi kujenga karibu na makaazi ya wananchi na sasa wakati mwengine hutokea hata kupiga wananchi. Mhe. Spika, kwanza askari kupiga wananchi hairuhusiwi ni kosa. Kwa vyovyote vile wanaofanya hivyo, kwa mujibu wa taratibu zao za kijeshi hatua huchukuliwa. Pia wananchi wanaopigwa wana haki ya kwenda mahakamani, kwa sababu hawapigwi na jeshi wanapigwa na watu wakati ule, hairuhusiwi wananchi kupigwa na askari yeyote yule.

Vile vile tungependa kutoa wito na wananchi wale ambao wanasogelea kujenga karibu na makambi basi wasifanye hivyo, kwa kuwa mara nyingi kambi huwepo mwanzo kabla ya ujenzi ule. Mara nyingi makambi haya hujengwa kutokana na mahitaji ya ulinzi wa taifa letu. Kwa hivyo, hatutoweza kuyaondoa makambi kutokana na umuhimu wake wa kuwepo pale, lakini wananchi nao wafuate taratibu za ujenzi, hakuna viwanja

vinavyopimwa karibu ya makambi, isipokuwa ni ule uvamizi wa kujenga karibu na makambi. Kwa hivyo, natoa wito kwa wananchi kuacha kujenga karibu na makambi na askari yeyote haruhusiwi kumpiga mwananchi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa na mimi ya kumuuliza Mhe. Waziri suala la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, moja kati katika yanayosababisha miripuko ya mabomu, inasemekana kwamba ni askari katika kambi zao huwa na mabomu ambayo huyazika katika kambi zao, na kwa kuwa askari wanahama, waliokuwepo sasa hivi wanaondoka wanakuja wengine na hata viongozi wao wale wakubwa wanaondoka wanakuja wengine na mabomu hayo yamezikwa na wakati yameshapitwa na wakati.

(a) Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba sasa kunahitaji uangalivu mkubwa sana ili kujua mabomu yaliyozikwa zamani kama ni kweli.

(b) Kwa sababu Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali alisema kwamba imeundwa timu ya wataalamu wa ndani na nje nchi jirani kuangalia utaratibu wa kuyaona hayo mabomu ili isisababishe miripuko tena. Je, kuwaruhusu wageni wakaingia katika kambi zetu, wakaangalia na kujua siri za ndani zilizomo kwenye kambi zetu. Je, hatuoni kama hilo ni tatizo, pindi likitokea tatizo kama hilo tutamlaumu nani.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: (Kny: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nia ya kuunda baraza hilo na kufanya uchunguzi ni kuhakikisha kwamba unatafutwa ufumbuzi wa matatizo yanayojitokeza kwenye miripuko ya mabomu. Ndio maana ukachukuliwa uangalifu mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba tunaunda baraza la uchunguzi ndani ya Jeshi la Wananchi, Kikosi cha Wanausalama wa Jeshi la Wananchi wanafanyakazi hiyo, pamoja na ushirikiano wa nchi rafiki ili kufanya tathmini ya kina kuhakikisha kwamba tatizo hili linalotokea litafutiwe ufumbuzi ikiwezekana lisiweze kutokea tena na kujua nini hasa chanzo chake. Ndio maana zikatumika tume zote hizo, nia yake ni kutaka kujua chanzo na kutaka kutafuta ufumbuzi.

Mhe. Spika, kuhusu wageni kushirikiana. Nilisema katika swali langu la msingi, nchi rafiki ni zile nchi tunazoziamini katika masuala ya ulinzi na ndio hao hao wanaotuuzia silaha na wanajua kila siri ya mambo yetu. Kwa hivyo, unaficha nini katika ulimwengu wa leo, madishi yaliyokuwepo, huna njia ya kuepuka hayo mambo na watu wanajua kila ulichonacho katika nchi hii. Kwa hivyo, ndugu yangu wanapotokea rafiki zetu kutusaidia katika kutatua tatizo la

msingi basi tusiogope na sisi jeshi letu liko makini sana katika kulinda nchi yetu.

Nam. 51

Uchafuzi wa Mazingira Kupitia Mahitaji ya Ujenzi

Mhe. Mohammed Haji Khalid - Aliuliza:-

Kutokana na kuongeza kwa ugumu wa maisha kwa wananchi wengi, kumekuwa na ongezeko kubwa sana la ukataji wa miti kwa ajili ya uchomaji wa mkaa na chokaa. Aidha, ongezeko kama hilo pia linahusu uchimbaji wa mchanga na uchongaji wa matofali katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kwamba, huu ni uchafuzi wa mazingira.

(b) Serikali ina mpango gani wa kuwapatia ajira wananchi wanaojishughulisha na shughuli hizo, ili kunusuru uchafuzi huu wa mazingira.

(c) Kwa kuwa miti, mchanga na matofali hutumika kwa ujenzi wa nyumba, Je Serikali itaweka mbadala wowote wa kutotumika kwake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51, naomba nikubaliane naye kuwa kutokana na kuongezeka kwa ugumu wa maisha, kumekuwa na ongezeko kubwa sana la ukataji wa miti kwa ajili ya uchomaji wa mkaa na chokaa. Vile vile, nakubaliana naye kuwa ongezeko kama hilo pia linahusu uchimbaji wa mchanga na uchongaji wa matofali katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba. Aidha, ni vyema ifahamike kuwa ongezeko la idadi ya watu hapa Zanzibar nalo linachangia kwenye ongezeko liliopo la ukataji wa miti na matumizi ya maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenvye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, hali ya ukataji wa miti kwa ajili ya uchomaji wa mkaa na chokaa, na uchimbaji wa mchanga na uchomaji wa matofali si uchafuzi wa mazingira, isipokuwa ni uharibifu wa mazingira. Mhe. Spika, uchafuzi wa mazingira hutokea baada ya kuingia vitu vigeni kwenye mazingira ambavyo sio vitu vya asili vya kimazingira, na

hupelekea mabadiliko ya mfumo wa kimazingira ya eneo, mabadiliko ambayo husababisha athari mbaya za kimazingira na afya ya jamii. Aidha, uchafuzi wa mazingira hutokana na mambo kama vile utupaji ovyo wa taka, maji machafu kutoka majumbani na viwandani, utupaji wa madawa ya sumu, umwagikaji wa mafuta na moshi wenye hewa chafu ambazo zimekuwa chanzo cha mabadiliko ya tabia nchi.

Mhe. Spika, uharibifu wa mazingira, hutokana na matendo kama vile ya mmong'onyoko wa fukwe, uchimbaji wa mchanga au uchongaji wa matofali; ukataji wa miti na mfano wa mambo hayo. Aidha uchafuzi wa mazingira hupelekea kwenye uharibifu wa mazingira. Ni vyema ifahamike kuwa uharibifu wa mazingira unahitaji gharama kubwa za kufanya marekebisho ya eneo lililoharibiwa, na kuna uwezekano mdogo wa kufanikiwa, na ili mafanikio yakipatikana yanachukua muda mrefu.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kuna wananchi wengi waliojiari katika shughuli za ukataji wa matofali na kuchimba mchanga katika sehemu mbali mbali za visiwa vyetu, ikiwa ndio shughuli zao za kujipatia riziki. Hata hivyo, pamoja na kuharibu mazingira kazi hizo ni ngumu zinahitaji nguvu nyingi, zinaleta athari kwa wanaozifanya kutokana na vumbi jingi, lakini pamoja na yote hayo kipato chake ni kidogo.

Mhe. Spika, ili kupunguza uharibifu wa mazingira ndani ya visiwa vyetu, lakini pia muhimu zaidi kunusuru afya za wananchi wetu ambao kwa sasa wanajiajiri katika shughuli hizo. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo na Mali Asili, ina lengo la kukaa pamoja na kuwaelimisha na kuwashajiisha wananchi hao, kujiajiri katika shughuli mbadala ambazo zitakuwa salama kwa afya zao na zitanusu mazingira yetu.

Mhe. Spika, miongoni mwa ajira hizo ni ufugaji wa kuku, uanzishaji wa mabwawa ya kufugia samaki, pamoja na shughuli za kilimo kwenye maeneo yaliyo bora kwa shughuli hizo. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais pia inaendelea na jitihada za kuielimisha jamii kufahamu umuhimu wa kutunza mazingira yetu.

(c) Mhe. Spika, kwa sasa serikali haijawa na mbadala wa miti, mchanga na matofali kwa shughuli za ujenzi. Hata hivyo, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mashirikiano na Wizara ya Kilimo na Maliasili, zinaendelea kuchukua juhudi za kuwaelimisha wananchi kufuata

sheria na taratibu zilizopo katika uvunaji wa miti na uchimbaji wa mchanga, ili kunusuru uharibifu wa mazingira yetu. Kwa wananchi wenye hali nzuri kiuchumi wanashauriwa kutumia mbao na miti inayoingizwa nchini, ili kupunguza ongezeko la matumizi ya maliasili hizo zinazozalishwa ndani ya nchi yetu. Aidha, naomba nichukuwe nafasi hii kutoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar wakiwemo Wajumbe wa Baraza lako kutumia mvua za masika za msimu huu kupanda miti kwa wingi kwa faida ya jamii na maziangira ya visiwa vyetu.

Mhe. Spika, kuhusu matumizi ya matofali ya kuchonga serikali inaendelea na juhudi za kuwaelimisha wananchi kutumia matofali ya saruji badala ya yakuchonga.

Aidha, serikali inaendelea na hatua za kutayarisha muongozo wa uvunaji wa maliasili zisizorejesheka ikiwa ni pamoja na ukataji wa matofali ya kuchonga. Muongozo huo utasaidia uvunaji endelevu wa maliasili hizo na kuwa na mfumo wa kuendeleza mashimo yaliyoachwa bada ya uvunaji kumalizika.

Mhe. Salum Amour Mtondoo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Misumeno ya moto inasababisha uharibifu mkubwa wa ukataji wa miti hasa minazi. Je, serikali ina mpango gani wa kuzuia misumeno hiyo, ili kunusuru miti ya minazi na uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanywa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa kulielewa hilo Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kushitikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili, tayari imeshaandaa kanuni ambayo inakusudia kupiga marufuku matumizi ovyo ya msumeno wa moto na hivi karibuni itatolewa rasmi. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moa la nyongeza. Mhe. Spika, ukataji wa miti unaofanywa si kwa sababu ya uchomaji wa mkaa na chokaa tu, lakini miti inakatwa kwa kupasua mbao na kadhalika na wengine wanafanya kwa biashara.

Kwa bahati mbaya jimbo ambalo lina miti mingi na msitu hivi sasa ni Jimbo la Mtambwe na hili nimelipigia vita sana. Lakini nililogundua ni kuwa Wizara ya Kilimo kwa kutumia Idara yake ya Misitu kwa kushirikiana na Sheha wao binafsi ndio wanaotoa vibali vya kukatiwa miti hii. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Waziri pamoja na kuwa kazungumza atashirikiana na wizara hizi ili kuliondoa, vipi ataweza kushirikiana nao wakati wale ndio wanafanya kazi kwa mujibu wa uwezo wa idara yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inafahamu kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili ndio yenye udhibiti katika kutoa vibali vya ukataji miti. Lakini sina taarifa kwamba wizara hiyo inatoa vibali ovyo na kutokufuata taratibu, ambazo wamejiwekea katika kutoa vibali hivyo.

Hata hivyo, ninachoweza kumuahidi Mhe. Mwakilishi ni kwamba tutawasiliana na Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa ajili ya kulizungumza suala hili kwa kina, ili kuhakikisha kwamba vibali hivyo vinatolewa kwa kufuata kanuni na masharti tuliojiwekea.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, inachosha kuwaomba radhi, lakini nawaomba radhi tuendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Nam. 106

Nyongeza za Mishahara kwa Wafanyakazi wa Serikali (*Increment*)

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza:-

Kwa kuwa hapo nyuma serikali ilikuwa na utaratibu wa kuwapatia wafanyakazi wake nyongeza (*increment*) ya mishahara kila mwaka na kwa kuwa tangu mwaka 2007 nyongeza hiyo imesitishwa.

(a) Mhe. Waziri, je ni sababu gani zilizopelekea nyongeza hiyo kusitishwa.

(b) Lini serikali itarudisha nyongeza hiyo kwa wafanyakazi wake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakllishi swali lake Nam. 106, lakini kabla sijamjibu swali hilo naomba kutoa maelezo ya msingi kuhusiana na suala hilo. Kwanza napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba imedhamiria kwa dhati kuboresha maslahi ya watumishi wake, ili waweze kumudu hali ya maisha.

Kila mmoja wetu anajua kuwa hali ya maisha inabadilika siku hadi siku na bidhaa zinazongezeka bei. Dhamira hii inathibitishwa na ahadi zinazotolewa na Viongozi Wakuu kwa kuangalia upya maslahi ya wafanyakazi na kuyanyanyua kwa kadri inavyowezekana.

Mhe. Spika, hivi sasa wizara yangu inakamilisha zoezi la utekelezaji wa ahadi hizo za Viongozi Wakuu. Taarifa rasmi za matokeo ya zoezi hilo zitatolewa mara tu zoezi hili litakapokamilika katika kipindi kifupi kijacho.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 106 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mwaka 2007 serikali ilifanya zoezi la kurekebisha maslahi ya wafanyakazi kwa kuzingatia taalum na viwango vya elimu vya wafanyakazi na ikafuatiwa kuunganisha mishahara na maposho (*consolidation*). Baada ya kufanyika kwa zoezi hilo kulibainika matatizo mbali mbali, ambayo ilibidi yasawazishwe kabla ya zoezi la kurejesha nyongeza kuanza tena, kazi zilizokuwa zinafanyika ni pamoja na:-

(i) Kuhakiki upya idadi ya wafanyakazi,
(ii) Kuangalia usahihi wa kumbukumbu za kielimu kwa kila mfanyakazi,
(iii) Kuweka muundo mpya wa mishahara na ngazi zake,
(iv) Kuandaa maslahi ya muda wa utumishi (*Scheme of Service*),
(v) Kufanya mapitio ya maposho mbali mbali ambayo yanalipwa kwa sasa na
(vi) Kupanga upya vianzio vya mishahara kwa waajiria wapya.

Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kuwa hivi sasa wizara imo katika hatua za mwisho ya kukamilisha zoezi hilo.

(b) Serikali inatarajia kuwarejeshea nyongeza hizo pamoja na maslahi mengine yakiwemo ya "*Scheme of Service*" ndani ya mwaka wa fedha 2011/2012.

Nam. 131

Watoto Wanaopotea

Mhe. Viwe Khamis Abdalla – Aliuliza:-

Kila siku kwenye vyombo vya habari huwa tunaona na kusikia watoto wanapotea, lakini hatuoni watoto hao wakionekana kutangazwa.

(a) Je, Mhe. Waziri unaliambia nini Baraza hili kuhusu watoto hao na habari zao zinakuwaje.

(b) Ikiwa watoto hawa hawapatikani, wizara yako ina mpango gani kuweza kuliondosha tatizo hili hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 131 lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Vyombo vyetu vya Habari siku hizi mara kwa mara hutangaza taarifa za wazee wanaopotelewa na watoto wao. Kwa kweli ni kwamba wanaokwenda kutoa taarifa ni wazee wanaopotelewa na watoto wao na wanapopatikana taarifa hupelekwa kwa mzee husika na sio kwa wizara.

Hata hivyo, kutokana na kwamba wizara ina jukumu la kusimamia haki za watoto, basi wizara itajaribu kufuatilia taarifa hizo, ili iweke kumbukumbu kwa maslahi ya taifa letu.

(b) Suala la matunzo, malezi na makuzi ya mtoto ni jukumu la jamii nzima tukianzia kwa wazazi, walezi, Taasisi za Usalama na viongozi mbali mbali katika jamii na sio la Wizara ya Ustawi wa Jamii pekee.

Mhe. Spika, hivyo natoa wito kupitia Baraza lako hili tukufu, ili kuliondosha tatizo hili, kila mmoja wetu awajibike katika malezi na kuwa waangalizi wakuu wa watoto wetu.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Waziri mtoto anakuwa ni mali ya taifa kwa wazazi wengine. Je, kama wanaonekana kwa nini serikali kwa kupitia wizara yako haichukui hatua tena ya kutangaza kwenye vyombo vya habari kwamba hawa watoto waliopotea wameonekana, ili wale wazazi wengine na wao waweze kushusha pumzi.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nimeeleza kwamba kuanzia sasa tutajitahidi kufuatilia

mambo haya ya taarifa zinazotolewa na wazee. Kwa kweli si rahisi kusema kwamba kila mzee anapompata mtoto wake kumfuatilia mzee alipo. Hata hivyo, tutaweka utaratibu maalum, ili tuone kwamba mtoto amepatikana na taarifa zimepatikana.

Nam. 33

Uagizaji wa Mbegu za Kupandishia Ng'ombe

Mhe. Salma Mohammed Ali – Aliuliza:-

Kuna taarifa kwamba, Wilaya ya Chakechake iliagiza kwa wingi mbegu za kupandishia ng'ombe kutoka nje ya nchi wakati huo huo uhaba wa mbegu hizo unaendelea kuwepo katika sehemu nyengine Kisiwani Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri, kuna usahihi gani wa uagizwaji wa mbegu hizo.

(b) Je, kama ni kweli mbegu hizo ziliagizwa, ni nchi gani zilikoagizwa na kwa utaratibu gani uliotumika.

(c) Je, kuna sababu gani zinazokwamisha mbegu hizo kupelekwa katika wilaya nyengine.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba. 33. Lakini kwanza naomba uniruhusu nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi kwa kuwa karibu na shughuli za mifugo zinazosimamiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na ninaamini ufuatiliaji wake anaofanya kama Msimamizi wa Serikali, utasaidia sana wizara yangu kukamilisha majukumu yake kwa wananchi.

Aidha naomba nisahihishe maelezo yalioko kwenye swali lake Nam. 33 kwamba sasa uhaba wa mbegu hauendelei tena kuwepo katika sehemu nyengine Kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo pamoja na shukrani hizo kwa Mhe. Mwakilishi. Sasa naomba nimjibu suala lake Nam. 33 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli Wilaya ya Chakechake iliagiza na kupokea mirija yenye mbegu 5,000 kwa ajili ya kupandisha ng'ombe kwa sindano.

b) Mhe. Spika, mbegu hizo ziliagizwa kutoka Manispaa ya Cles nchini Italy, Mji ambao unamashirikiano ya kiurafiki na Mji wa Chakechake, ambapo mbegu hizo zimeletwa kama msaada kutoka kwa Mji rafiki wa Cles kwa lengo la kuendeleza ufugaji wa ng'ombe katika Wilaya ya Chakechake.

c) Mhe. Spika, kama nilivyogusia katika kifungu (b) hapo juu, makubaliano ya msaada huo kutoka kwa ndugu zao wa Italia ni kwa ajili ya Mji wa Chakechake, hivyo isingelikuwa vyema na busara kugawa mbegu hizo kwenye Wilaya nyengine bila ya idhini ya Mfadhili mwenyewe.

Mhe. Salma Moh'd Ali: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Waziri mbegu hizo zimehifadhiwa wapi na zimeshatumika ngapi kwa ajili ya wafugaji.
b) Kwa vile mbegu hizo ni msaada kutoka nje kwa ajili ya wafugaji wa Chakechake, ni kwa nini wafugaji wa Chakechake wawe wanazinunua mbegu hizo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kifungu (a) mbegu hizo zimehifadhiwa katika Ofisi ya Mifugo ya Wilaya ya Chakechake na hivi sasa zimeshatumika mbegu 300.

(b) Wafugaji wa Wilaya ya Chakechake wanauziwa kwa sababu msaada huu umeleta kwa ajili ya Baraza la Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Chakechake ili kuendeleza shughuli za mifugo katika wilaya hiyo. Kwa hivyo, lengo ni kuendeleza shughuli za mifugo.

Kinachofanyika hivi sasa ni kuuziwa wafugaji angalau kwa nusu ya bei ile ambayo iko katika soko ili Halmashauri ya Wilaya na Baraza la Mji hapo baadae iwe na uwezo wa kuagiza mbegu hizi, isiwe kila mara kuwa wanaomba msaada tu. Hilo hasa ndio sababu.

Mhe. Farida Amour Moh'd: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa ng'ombe wengi waliopo katika Kisiwa cha Pemba na maarufu ni wa kabila la Jezi.

(a) Je, mbegu hizo zilizoagizwa ni za kabila la jezi au kabila gani.

(b) Kama sio ng'ombe wa kabila la jezi, wana ila gani na sifa gani?

(c) Je, watahimili mazingira ya Pemba.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza katika maelezo yake amesema kwamba ng'ombe wengi walioko Pemba ni wa kabila jezi. Usahihi ni kwamba, ng'ombe wengi walioko Pemba ni wa kabila la ng'ombe wenye nundu, ndio wengi zaidi, wakifuatiliwa na kabila la Jezi na ***Frision.*** Hao ndio ng'ombe walioko wengi Pemba, lakini wengi ni wale wa kienyeji.

Sasa katika suala lake ni kwamba, mbegu hizi si wa kabila la jezi isipokuwa ni kabila wanaita ***Bronsrist*** na hili ni kabila geni na sifa yake ni kwamba ni aina ya ng'ombe wenye nyama nyingi na maziwa mengi. Kwa hivyo, tukilinganisha na mbegu nyengine mfano ya Jezi wao wana maziwa mengi, lakini kiwango chao cha nyama ni kidogo, ***Bronsrits*** wana mwili mwingi kwa hivyo nyama yao ni nyingi.

Kwa hiyo, wana nyama nyingi na maziwa mengi, hivyo mfugaji anapoamua kuuza anaweza akapata bei nzuri, kwa sababu wakiamua kuchinja basi atapata faida kubwa.

Kuhusu ila yake ni kwamba, kwa vile ni wakubwa watalazimika kulishwa zaidi kuliko wengine. Mhe. Spika, uwezo wao wa kula ni mkubwa kidogo. Kuhusu kuhimili maradhi Mhe. Spika, ni kwamba ng'ombe hawa huko kwa wenzetu Bara wapo na kama utawatunza vizuri, basi uwezo wao wa kuhimili maradhi ni mzuri, ikiwa utawaacha ovyo ovyo tabaan hali yao itakuwa si zuri. Kwa hivyo, namna ya kuhimili maradhi itategemea matunzo ambayo mfugaji anamtunza ng'ombe mwenyewe.

Nam. 56

Uharibifu wa Mazingira ya Misitu

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Miongoni mwa athari kubwa za ukataji wa misitu iliyopo Zanzibar ni pamoja na kupoteza makaazi ya wanyama kama vile komba na hivyo kusababisha wanyama hao kukimbilia katika majumba makubwa, yaliopo maeneo mbali mbali ya Mji wetu. Kwa mfano, Vuga, Mkunazini na kadhalika, wizara

inachukua hatua gani katika kudhibiti tatizo hilo, ili tusiendelee kupoteza rasilimali zetu muhimu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba hali ya ukataji misitu na miti katika maeneo ya makaazi ya watu imekuwa kubwa na imesababisha kupotea kwa baadhi ya rasilimali za wanyamapori hapa nchini.

Mhe. Spika, maisha ya komba kitabia ni tegemezi, yaani anategemea binaadamu kuendeleza maisha yake. Ukweli huu unadhihirika hata katika yale maeneo yenye misitu mikubwa kama Jozani, ambapo komba hutoka msituni nyakati za usiku na kuingia maeneo ya makaazi ya watu kwa ajili ya kujitafutia chakula. Hali hiyo inajitokeza pia katika maeneo ya Miji ikiwemo Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Kwa kweli ni tofauti na maeneo ya mashambani, ambapo komba baadaye hurudi katika makaazi yake ya kawaida ya msituni. Sasa katika maeneo ya mijini kutokana na ongezeko la ukataji miti, basi kombo hushindwa kurudi katika makaazi yake kwenye miti mikubwa na hivyo huamua kujihifadhi katika majumba makubwa ya maeneo ya Vuga na Mkunazini.
Mhe. Spika, hatua ambazo inachukua katika kudhibiti hali hiyo ni pamoja na:

- Kudhibiti ukataji wa miti ovyo na isiyo na lazima katika maeneo ya mijini, sio tu kwa kudhibiti upotevu wa wanyamapori, lakini pia kuimarisha hali ya mazingira na mandhari nzuri ya miji yetu;

- Kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu na wanyapori na umuhimu wake kwa jamii hapa nchini na

- Kuwashajiisha wananchi kuendelea kupanda miti katika maeneo husika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, moja ya kivutio cha watalii ni kuona rasilimali zetu zilizopo Zanzibar. Je, Mhe. Waziri huoni kupotea kwa rasilimali hizo ni kukosa mapato kwa Wazanzibari.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, ni sahihi kabisa kwamba watalii na hata sisi wenyewe ni jambo la kusikitisha sana tunapokosa rasilimali

za wanyama pori na vizazi vijavyo na wageni wetu wakashindwa kuviona. Hayo yametokea kwa chui maarufu wa chui wa Zanzibar na wanyama wengine pia kutokana na tabia yetu hivi sasa ya ukataji miti ovyo na ujenzi wa makaazi ulivyoshamiri wanaelekea hatarini kupotea.

Jitihada zitaendelea kufanywa na wizara yangu kudhibiti hali hiyo na tunakuombeni Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nanyi mtumie muda wenu kuwasihi na kuwaelimisha wananchi majimboni mwenu, kuwa makini zaidi na wapenzi wa miti na wanyama.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kwa kuwa amekiri kwamba suala la komba kuhamia Mji Mkongwe linatokana na ukataji wa misitu na hivyo husababisha kutafuta maeneo yenye makazi ya watu kwa ajili ya kupata hifadhi yao.

   Kwa kuwa ukataji huu wa misitu ni jukumu linalopaswa kusimamiwa na wizara yake. Sasa kwa kushindwa kusimamia jukumu hilo na kupelekea ukataji wa misitu hadi komba kukimbilia Mji Mkongwe. Wizara yake ina mpango gani wa kufidia wananchi wa Mji Mkongwe wanaoathirika na komba hao kuingia katika majumba yao na kuwaletea madhara mbali mbali.

b) Kwa kweli tunajua kuwa komba wana harufu mbaya sana. Je, ni hatua gani inachukuliwa, ili kuhifadhi harufu nzuri za Mji Mkongwe zisichafuliwe na harufu za komba hao. Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kutokubaliana naye kwamba wizara yangu imeshindwa kuhifadhi rasilimali za misitu. Wizara yangu inao uwezo wa kutosha ambao ni mkubwa wa kuhifadhi rasilimali za misitu ya nchi yetu na tutaendeleza hilo kwa kasi.

Vile vile nimueleze kwamba komba wana asili ya Mji Mkongwe, kwa maana yeye amewakuta kama walivyowakuta babu zake na babu zangu mimi na harufu yake pia Mhe. Spika tumeshaizowea. Kwa kweli kama nilivyosema kwamba tumewakuta sisi na babu zetu kabla ya sisi, isipokuwa tu kwa bahati mbaya miti tunaikata sana, kwa hivyo sasa tunawakaribisha zaidi majumbani.

Kwa hivyo, nimuombe yeye akiwa Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mji Mkongwe aendelee kuwashajiisha, basi vile vitalu vya asili vya mji huo

wasiviguse tuendelee kupanda minazi na miti ya asili ambayo tulikuwa tunaipanda mle, ili hali ile iendelee kuwa nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa naomba tuendelee, lakini tu niwaombe kwamba wengi wetu leo tumealikwa katika shughuli mbali mbali, ikiwa ni pamoja na kutawadhwa Mhe. Rais wa Zanzibar kuwa Mkuu wa Chuo cha *SUZA.*

Kwa hivyo, utakuta kwamba, pengine Mhe. Waziri watakuwa wanakwenda huko, lakini naomba tujigawe basi, sisi tuliopo hapa tuendelee kuwepo pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe, ambao mmealikwa waliokwenda wawe ndio wanatuwakilisha, ili shughuli zote mbili ziende hii na ile ya Mhe. Rais kutawadhwa kuwa Mkuu wa Chuo cha *SUZA*.

Muda unakaribia kumalizika na maswali mengi tumeyaacha kutokana na matatizo mbali mbali, nimuombe basi Mhe. Waziri wa Nchi tuongeze muda ili tumalize maswali yaliyopo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza maswali yaliomo kwenye *Order Paper* ya leo naomba waheshimiwa wajumbe waridhie kuweka kanuni kando, ili tuweze kumaliza maswali yaliyo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono.

Nam. 79

Uimarishaji wa Chuo cha Uandishi wa Habari, Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Mhe. Waziri, pamoja na ukweli kwamba Wizara yako imeanzisha Chuo cha Uandishi wa Habari nchini, wananchi wengi hawafahamu umuhimu wa chuo hicho na matokeo yake, hukimbilia kusoma kozi mbali mbali zinazosomeshwa na vyuo vyengine kinyume na kozi ya Uandishi wa Habari, inayotolewa na chuo chetu.

(a) Je, Wizara imechukua hatua zipi za kukitangaza Chuo hicho nchini na nje ya nchi, kwa lengo la kupokea wanafunzi wengi zaidi.

(b) Kwa kuzingatia masomo yanayosomeshwa chuoni hapo, Je, kuna tofauti ya somo la *"Information Technology Assistance Journalism* (IT-Assistance Journalism) na *International Technology Operation Journalism (IT-Operation Journalism)".*

(c) Kwa kuwa mwandishi mzuri wa habari ni yule aliyepata mafunzo yake kwa njia ya vitendo *(practical).* Je, chuo kina Kamera ngapi kuwawezesha wanafunzi wanaosoma chuoni hapo kuzitumia katika mafunzo yao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 79 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza Chuo hakina ukahika iwapo wapo wanajamii ambao hawafahamu umuhimu wa Chuo chetu kwani hakijafanya utafiti na kupata majibu ya kitaalamu juu ya suala hilo.

Hata hivyo, Wizara inaamini kwamba watu wengi wanafahamu umuhimu wa Chuo kwa sababu zifuatazo:-

- Chuo kimeweza kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka ishirini na nane (28) wa cheti 2009/2010 hadi kufikia arobaini na tatu (43), 2010/2011 wakati wanafunzi wa Stashahada *(Diploma)* wameongezeka kutoka thelathini na tano (35) hadi hamsini na tatu (53) kwa mwaka wa masomo unaonedelea. Aidha, maombi mengi yamekuwa yakiwasilishwa lakini Chuo kina uwezo mdogo wa kudahili wanafunzi kutokana na ufinyu wa nafasi na uchache wa madarasa.

    (a) Mhe. Spika, wizara kupitia chuo imekuwa ikifanya juhudi mbali mbali za kukitangaza chuo ikiwa ni pamoja na Mashirika ya Kimataifa kama *UNESCO*, Radio ya Kimataifa ya China *(CRI)* na mengine, na pia kupitia kwa baadhi ya Mabalozi wadogo waliopo Zanzibar. Aidha, hatua hiyo inakwenda sambamba na mashirika ya ndani kama vile *Tanzania Media Fund (TMP)* na Baraza la Habari Tanzania..

        - Programu za Raidio na Televisheni
        - Vipeperushi pia vinatumika

Kutokana na juhudi hizo, hivi sasa Chuo kinatekeleza mradi wa kufundisha Darasa la Kichina *(Comfucus)* lugha ya kichina ambalo tunaamini kwamba litasaidia sana kukitangaza Chuo chetu ndani na nje ya Zanzibar.

(b) Ni kweli kwamba ipo tofauti kati ya nadharia ya *"International Technology Assistance na International Technology Operation Journalism (IT- Operation Journalism).*

(c) Hivi sasa Chuo kinazo Camera saba (7) za kisasa ambazo wanafunzi hupata nafasi ya kuzitumia kwa vitendo katika mafunzo yao. Napenda kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Mwakilishi kwamba idadi hii sio kubwa lakini sio ndogo sana ikilinganishwa na Vyuo vyengine vikongwe viliopo nchini ambapo wastani wao ni kama hivi za kwetu. Kwa kuzingatia kuwa Chuo kinafundisha *"Photo Journalism"* na sio Camera *Operation* idadi hiyo inasaidia sana mafunzo kwa vitendo huku juhudi za kununua nyingi zaidi zikiendelea kila fedha zitakapopatikana.

Nam 39

Kuimarisha Vituo vya Afya

Mhe. Salma Mussa Bilali – Aliuliza:-

Kwa vile Vituo vyenye uchakavu uliokithiri ambavyo vinatoa huduma za msingi kama vile Vituo vya Umbuji, Kitogani na Kizimkazi Dimbani.

Je, Wizara yako ina utaratibu gani wa kuviimarisha Vituo hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake Nam. 39 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kuwa kuna vituo vinavyotoa huduma ya msingi ambavyo ni vichakavu ikiwemo Kituo cha Umbuji na Kizimkazi Dimbani. Naomba nimueleze Mhe. Mwakilishi kuwa kituo cha Kitogani hakimo katika hali mbaya ya kukithiri ila kinahitaji kufanyiwa marekebisho madogo madogo. Suala hili Wizara inalielewa na

kwamba mimi mwenyewe nikiwa Naibu Waziri wa Wizara hii nimevitembelea na kuona hali halisi ya vituo hivyo.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa maendeleo imeandaa mikakati ya kuvifanyia matengenezo vituo vyote vyenye hali isiyoridhisha. Kazi za ukarabati wa Vituo vya Afya kwa Wizara yangu ni jambo la kawaida katika mipango ya kila mwaka. Aidha, Wizara imeweka kitengo maalum *(Health Care Engineering Unit)* kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuangalia ubora na uzima wa vituo ikiwa ni pamoja na zana. Pale inapoonekana kuna haja ya kufanya marekebisho makubwa kitengo kinawasilisha taarifa ili ziwekwe kwenye mipango wa mwaka *(Annual Plan of Action).*

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya jumla jumla ya Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa msimu wa masika umeingia na kwa katika uchakavu wa vituo hivyo ni pamoja na uvujaji uliokithiri.

Je, Mhe. Naibu Waziri wizara yako ina mpango gani wa dharura kwa vituo hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Nafahamu kwamba msimu wa masika unakuja na baada tu ya kupata suala lako hili nimehakikisha kwenda kuangalia hicho kikubwa kilichopo huko na kukifanyia matengenezo, kwa hivyo najua kwamba hawatoathirika wakati wa mvua.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala maja la nyongeza. Katika vituo vya afya vilivyo katika hali mbaya sana ni kituo cha Mzambarauni kilichopo katika jimbo langu ambacho hivi sasa kimeshafungwa na huduma inakwenda katika nyumba ya watu binafsi.

Je, Mhe. Waziri kwa umuhimu wa afya atanisaidiaje kuona kile kituo kinafanyiwa ukarabati unaostahiki na badala ya matibabu kufanyika katika nyumba ya mtu binafsi tuondoe dhiki hiyo na turejee katika kituo chetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakubaliana na wewe kwamba kituo cha Mzambarauni ni kibovu na huduma hizo zimehamishiwa kwenye nyumba ya mtu binafsi kwa makubaliano ya kamati ya afya pamoja na shehia, pamoja na wenye kituo kwa sababu wameona kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo ili watu wao wasihangaike kutoka pale kwenda mbali na hilo sizani kama lina ubaya, kama tatizo limetokea na kamati ya afya pamoja na

shehia na wafanyakazi wa afya tulionao pale wakaweza kuchukua hatua kama hiyo inaonekana kwamba sehemu ile ina mashirikiano mazuri baina ya jamii pamoja na Wizara yetu ya Afya.

Nimefika kituo cha Mzambarauni binafsi mimi mwenyewe nimekiona na kituo cha Mzambarauni kiko katika awamu ijayo ya majenzi ya *ADB* katika awamu ya tatu kitajengewa kituo kipya na kitafanyakazi kama ilivyokubalika.

Nam. 26

Matengenezo ya Barabara za Ndani (*Feeder Roads*)

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Ujenzi wa baadhi ya barabara za ndani *(feeder-roads)* zilizoko katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambazo zimepatiwa msaada kutoka Akaunti ya *Milenium Chalenge (Millennium Challenge Account)* bado haujaanza kwa muda mrefu sasa tokea kumalizika kwa hatua za matayarisho ya awali.

(a) Je, kuna sababu gani zilizopelekea ucheleweshaji wa ujenzi wa barabara hizo.

(b) Je, Wizara inaahidi kuanza kwa ujenzi wa barabara hizo lini.

(c) Serikali ina mpango gani wa matengenezo kwa baadhi ya barabara zilizoko Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambazo kwa sasa hazipitiki kabisa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza miradi ya ujenzi wa barabara kwa njia tatu kama zifuatavyo.

Njia ya kwanza ni ile inayomuhusisha mshirika wa maendeleo kwa kushirikiana na Serikali ambapo malipo ya ujenzi wa barabara husika huchangiwa kwa pamoja baina ya mshirika na serikali kwa gharama za fidia kama nyumba, miti, huduma za umeme, uhamishaji wa maji, simu pamoja na malipo ya barabara hiyo.

Njia ya pili ya utelekezaji wa mradi ni ile ambayo inagharamiwa na serikali peke yake aidha kwa kutumia fedha za serikali kupitia hazina au kutoka katika mfuko wa barabara.

Njia ya tatu ni ile inayoshirikisha utekelezaji wa mradi kwa kutumia fedha za ufadhili peke yake, aina hii ya tatu ndio aina ya mradi wa barabara sita za Pemba zinazotokana na suala lililoulizwa na Mhe. Mwakilishi.

Aina hii ya utekelezaji wa mradi huu ni aina yake kwa mradi huu wa Pemba ambapo utaratibu wa uendeshaji na ulipaji wa gharama zote za mradi uliotajwa zinafanywa na mshirika wa maendeleo, na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar italipa gharama za uondoaji wa huduma za maji, umeme na simu tu.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kuwa ujenzi wa barabara za ndani zilizoko Mkoa wa Kaskazini Pemba ambazo zimepatiwa msaada kutoka *account* ya *millennium challenge* bado haujaanza kwa muda, lakini taratibu za kuanza kwa mradi huu hazijasimama na zimekuwa zikiendelea kama zilivyopangwa. Hivi sasa ofisi ya *millennium challenge account* tawi la Tanzania kwa kushirikiana na Wizara yangu inakamilisha hatua za mwisho za kumpata mshauri msimamizi wa mradi huo, hatua iliyofikiwa ni kuwa dhabuni zimeshaitishwa tathmini imefanywa na ripoti imepelekwa kwa mfadhili kwa ajili ya kupata idhini yake, aidha taratibu za kupata mjenzi zinaendelea ambapo tarehe 30/3/2011 yaani kesho dhabuni zitapokelewa na kufunguliwa na kazi ya kufanya tathmini itafuata baadae. Mhe. Spika, matumaini yetu makubwa ni kwamba kunako mwezi wa tano mwaka huu mkandarasi atakuwa amepatikana na kazi za ujenzi zitaanza mara moja.

Mhe. Spika, kuhusu matengenezo ya barabara nyengine za ndani za Mkoa wa Kaskazini Pemba ambazo hazipitiki kabisa zitafanyiwa matengenezo kila hali ya fedha itakaporuhusu kwa kutumia fedha kutoka mfuko wa barabara, ukarabati huo utahusisha na uwekaji wa kifusi pamoja na kupitisha *grader* kwa maeneo yale yote yanayoonyesha ipo haja na ulazima wa kufanya hivyo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, baadhi ya barabara hizi ambazo zinahifadhiwa na *NCC* zinapitika kidogo lakini kuna zile ambazo hazipitiki kabisa na kuna barabara ambazo hazimo katika utaratibu huu ambao wananchi wenyewe wameshatumia fedha nyingi sana angalau waweze kupita.

Mhe. Spika, kwa kuthamini jasho na juhudi ya wananchi haiwezekani kuwa Mhe. Waziri kuweka mkakati maalum kwa kule ambako fedha imeshatumika ukaweza kumaliza matengenezo yaliyobaki kwa kuwapa nguvu iliyokwishatumika kwa mfano. Barabara Mkarafuu Mmoja/Kiuyu tumetumia fedha zetu wenyewe kuitengeneza lakini ikibakia mpaka serikali itakapokuwa na uwezo ile nguvu itakuwa imepotea na itakuwa haipitiki tena na itakuwa ni kuanza kazi upya, kwa hivyo kwa barabara kama hizi haoni kuna haja ya kutoa kifua mbele kuona kuwa kuna jasho la wananchi linathaminiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Wizara yangu imekuwa ikieleza kwa muda mrefu barabara zipi ambazo zimo kwenye jukumu la kujengwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa maana ya kwamba Wizara yenyewe na barabara zipi ambazo zinapaswa kujengwa na Manispaa. Wizara yangu muda wote imekuwa ikishirikiana na Baraza la Manispaa na Serikali za Mitaa kutoa kila aina ya ushirikiano katika kuwapunguzia shida, tabu na matatizo ya usafiri kwa kufanya ukatabati wa barabara zote za Zanzibar.

Napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi Wizara yangu inaendelea na jitihada hizo na tutafanya ukarabati wa maeneo yote ya barabara ambazo hazipitiki ili kuweza kuwaondoshea matatizo wananchi wetu kwa huduma ya usafiri, tumefanya hivyo katika maeneo mengi nay eye mwenyewe Mhe. Mwakilishi atakuwa shahidi jimboni kwake barabara nyingi zilikuwa hazipitiki tumeanza jitihada hizo na kuondoa matatizo hayo na namhakikishia Mhe. Mwakilishi jitihada hizo hazitoishia hapo tutaendelea na namuomba sana ushirikiano wake.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Watoto 2011

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nakushukuru Mhe. Spika, nami kuwa mchangiaji wa mwanzo leo kwa mswada huu muhimu ulioko mbele yetu, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mimi na wenzangu kufika siku hii tukiwa na afya njema pamoja na mapungufu ya hapa na pale lakini bado tuna uwezo wa kuendeleza shughuli tulizokabidhiwa na wananchi wetu.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuleta mswada huu muhimu sana na wakati muafaka kwa vizazi tulivyonavyo sasa, wajumbe wa baraza lako tukufu wameuchangia mswada huu kwa mapana na marefu na nawaomba kadiri hali itakavyoruhusu waheshimiwa waendelee kuuchangia kwa umuhimu wa mswada huu kwa watoto wetu na taifa kwa jumla.

Mhe. Spika, kidogo kulikuwa na sitofahamu ya tafsiri ya neno mtoto mimi niseme kwamba kwa upande wangu sina cha kuongeza wala kupunguza zaidi ya vile mtoto alivyotajwa ndani ya kitabu cha mwenyewe Alla Subhanah Wataala.

Lakini jengine baada ya hapo tumejenga mazingira ya ulezi na utunzaji wa mtoto huyo ndio pale serikali nayo ikasema kwamba mtoto ni yule ambae bado atakuwa chini ya umri wa miaka kumi na nane (18) saa yanayotokea hapa mpaka tukamkuta kwamba mtoto kapewa tafsiri ya kutokuwa mtoto ni mtu mzima, huyu hajafuta ile *defenetion* sahihi lakini sasa ni mazingira ndio yamemkumbwa mtoto huyu ameingia au ameingizwa huku ambako kapata sifa ambayo bado hajaifikia. Katika hili Mhe, Spika, mimi nimelenga kuzungumzia vyombo viwili vikubwa.

Kwanza sisi wazazi leo tumepoteza kabisa dhamana yetu kwa watoto wetu tafsiri nyembamba kwangu mimi ni hiyo, wazazi wengi tumejisahau dhamana zetu ndani ya ulezi wa watoto wetu hatimae tumeyavuna makubwa na mazito badala yake tunaisukumia serikali kwamba inachangia. Serikali ina mchango wake lakini asilimia kubwa naiweka kwa wazazi.

Mhe. Spika, mswada madhumuni yake ni kutunga sheria hii kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za watoto unaoendelea sasa hivi, tunashuhudia sisi wazazi maharusi yanayoendelea hivi sasa wanashirikishwa watoto wadogo wengine wana umri hata miaka sita au chini ya hapo wanakamatishwa mikasi kwenye chai za harusi, kuna majina mengi tu yanaendelea sasa hivi watoto ndio wanaoshiriki wanapangwa na wazazi wao, kukamatishwa maveli mambo yale tukiyaona kwenye magazeti tulipokuwa bado lakini leo ni watoto wetu wanaokamatishwa yale, mtoto yule anaanza kuona yale ndani ya umri wa miaka sita, atakapofika miaka tisa yuko shule au miaka kumi na zaidi yupo shule hata kama kajaaliwa anafanya vizuri lakini mazingira yale ambayo kashahusudu na anahisi ndio mazuri kwake kuliko elimu ndio pale anapokwambia baba mchumba wangu huyu na usiponiozesha utakiona wewe.

Mhe. Spika, baba kwa kuepusha hilo anaweza kumuozesha mtoto wake hata kama hapendi iwe hivyo, lakini mengine Mhe. Spika, wenzetu walioko majumbani wake zetu watoto wanajenga urafiki kwa wenzao wanaosoma darasa moja, leo yuko Wete Kipangani anamtembelea mwenzake aliyoko Limbani Wete mzazi bila ya kufuatilia kuna nini katika uhusiano huu, yule anaaga anakwenda *tuition* Limbani na Walimbani anaaga anakwenda *tuition* Kipangani mkutano ni hapo kati kati hakuna *tuition* inayokwenda kusomwa ni nyengine mpya nje ya ile iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, haya yapo hapa Unguja, Pemba yapo mtihani mkubwa umetukabili sasa hivi wiki nzima watoto wamefungiwa pahali watoto ndio wanaletwa shuleni, mswada umekuja wakati muafaka nasema kwa sababu tumepata jamii mbaya sana haina imani, haijui vibaya wala haina haya katika hili. Lakini wazazi tuna zima kubwa na lazima tukubali kwamba tuna jukumu zito kwa vizazi vyetu, kina mama wana mchango wao mkubwa katika kusaidia ulezi lakini nawao wanayaporomosha maadili haya kwa watoto kuwapenda zaidi ya viwango vinavyostahiki, wakati mwengine baba mkali anarusha cheche ndani ya watoto mama anakwambia unamuonea bure wakati wa sasa sio ule wako wewe na mimi siajabu maneno kama hayo mtoto kujisikia ana haki ya kufanya anayoyafanya kinyume na taratibu bado lawama yangu ipo kwa wazazi. Kwa hivyo wazazi tunapaswa kurudi kwenye kitabu chetu haya yapo tokea awali tumeyapuuza na sasa maneno mengine yanasema ng'ombe anatupiga wenyewe.

Mhe. Spika, upande wa serikali mara nyingi huwa napiga kelele kwamba wahusika wanaotoa vibali kwenye kumbi za starehe baa zilizoko mitaani ni baa kweli, ni balaa zaidi ya baa yanayotendeka ni magumu watoto wetu wanayashuhudia mtoto ni mtoto anachokiona anaweza kuvutika nacho akaona na yeye ajaribu, tuyaondoeni mabaa yaliyopo mitaani Mhe. Spika, yanatumalizia watoto hawa lakini sasa hivi na kumbi za starehe tuna disco toto hapa hoteli ya Bwawani, muda hautoshi kuyaeleza ambayo yapo kwenye disco lile mimi ni mjumbe wa Kamati ya Uvuvi Mifugo na Habari karibuni tulikuweko tumepata mengi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, serikali nayo kwa upande wake lazima nayo iwajibike katika hili mambo kama haya taarifa zinapatikana kwa sehemu husika lazima hatua zichukuliwe, watoto tunawahitaji ni taifa la kesho watoto hawa tunawahitaji kuja kukamata dhamana nzito, lakini kama jamii tutaijenga katika misingi hii tutashindwa na hili litakuwa ni taifa la ajabu mno. Katika hili tusimtafute mchawi kwanza tujue wazazi wenyewe tuna kazi hiyo tusaidiane na serikali yetu.

Mhe. Spika, nashukuru kwamba kwenye mswada kuna suala la mahakama kuwasaidia watoto hawa tofauti na mahakama ya leo inayobeba watoto na wazazi wao, mengi yameshazungumzwa kwa Mahakama zetu zinazofanya juu ya watoto. Lakini haraka haraka nataka niseme kwamba tunapitisha sheria hii huku tukishuhudia vitendo visivyofaa kwa taasisi zetu nitazitaja.

Wizara ya Afya mtoto anafanyiwa vitendo vibaya kila kitu kipo wazi kimeonekana. Wizara ya Afya siisemi kama ilivyo itaingiza wengi. Kuna watu sio waaminifu katika shughuli zao, hawana uadilifu, wanaficha ukweli kusaidia wahalifu wale.

Mhe. Spika, mtoto akishabakwa huyo keshavunjiwa maisha yake yote. Familia nayo haina raha katika macho ya jamii. Nasema kwamba na wizara ya afya kwa watu kama hawa wenzetu ambao sio waaminifu, hawana uadilifu katika shughuli zao. Wizara nayo iwachukulie hatua ipasavyo. Wengine Polisi. Badala ya kufanya kazi yao inastahiki wao hujifanya ndio mahakimu. Sambamba na Polisi na Mahakama zenyewe.

Mhe. Spika, kama kweli tuna nia ya kulinda sasa watoto wetu, taasisi hizi zina msaada mkubwa wa kuhakikisha kwamba watoto wanatendewa haki zao. Nadhani sheria hii pia ingesema kwa wale wazazi wanaofika mahali wakaweza kuwatendea watoto wao vitendo vya kinyama bila ya aibu yoyote ile ni hatua gani ya kisheria ichukuliwe dhidi yao.

Mhe. Spika, ni aibu kubwa hasa kwa jamii ya kizanzibari kusikia vitendo hivi vinatokea kwa mzazi kumtendea mtoto wake aliyemzaa. Hatimaye anapelekwa polisi, wanatokea watu wanakwenda kumfunika huyu mtu, ati kufungwa kwake yeye labda na mama kule atakuja kuachwa. Hayatizamwi maisha ya mtoto huyu na hatima yake ishapotea. Huyu mzazi ni mzazi hatobadilika na atabaki kuwa mzazi, lakini amebadilika kwa namna nyengine kwenye utu, lazima akarekebishwe.

Mhe. Spika, kwa upande wangu mimi nilisema angalau tu niweze kutia baraka zangu. Mswada ni muhimu, waheshimiwa wajumbe nakuombeni sana muuchangie, maeneo ni mapana ya kuwekwa sawa. Kuna vituo vya ulezi vya watoto hawa vipi viwekwe, mahakama vipi ziendeshwe, kusudi tuweze kujenga jamii tunayoihitaji itakayokuwa na faida na hatima ya taifa ili.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Naomba *inshallah* wajumbe watoe baraka kwa wingi. Ahsante sana.

Mhe.Ussi Jecha Simai: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Mswada wa Sheria ya Watoto. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya. Vile vile kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa na hali ya amani na utulivu katika nchi yetu. Jambo ambalo linatufanya tuweze kujadili mambo yetu kwa utulivu mkubwa zaidi.

Mhe. Spika, kwa upande wangu mimi katika kuuchangia Mswada huu, nitakwenda moja kwa moja hasa katika sehemu ya pili ya Mswada huu ambayo inazungumzia Maslahi Bora na Haki za Mtoto.

Mhe. Spika, sehemu hii muhimu sana katika Mswada huu ambao tunaujadili hapa. Amezungumzia hasa haki za mtoto. Mimi mapendekezo yangu kwa hapa, pamoja na kwamba umeonesha haki za watoto lakini haukuonesha wajibu wa watoto kwa wazazi. Kwa mawazo yangu naomba Mhe. Waziri katika kifungu cha 15 tungeliongeza kipengele cha (c) ambacho kinamuonesha mzee na yeye awe na nguvu juu ya mtoto wake. Kikataze mtoto kumdhalilisha mzee ama mlezi. Kama tunavyojua kuna watoto wengine ni watukutu au wakorofi, wanaweza wakamdhalilisha mzee. Lakini wao katika sheria hii haikuonesha kwamba kuna kikwazo gani ambacho kitawapata wao endapo watawafanyia vitendo vibaya wazazi wao.

Mhe. Spika, suala la udhalilishaji ambalo limezungumzwa katika sehemu ya pili ya Mswada huu. Suala la udhalilishaji watoto ni suala ambalo kila siku linakuwa. Kila siku zinatungwa sheria za kuwalinda watoto lakini bado kasi inaongezeka, utadhani zile sheria zinawafanya watu kuwaruhusu wafanye vitendo vile badala ya kuwakataza.

Mhe. Spika, katika eneo hili la udhalilishaji wa watoto tunashuhudia mara nyingi kesi zinazohusu udhalilishaji wa watoto, washukiwa wanakuwa hawatiwi hatiani. Watu wengi wanakuwa wanalaumu wazee kwamba mtoto wake wamefanyiwa vibaya lakini hakuna lililopatikana au lililofanywa. Tatizo la hapa sio kama mahakama zinawaonea watu hawa au zinawapendelea wahalifu. Pamebainika kwamba ushahidi ambao unatolewa katika kesi hizi za udhalilishaji wa watoto mara nyingi ushahidi wake unakuwa hauwi mzito kiasi ambacho unashindwa mtu kutiwa hatiani kwa tuhuma ya kosa hilo.

Kwa mfano zinapokea kesi za ubakaji, tumebaini mara nyingi wazazi au walezi baada ya kitendo hicho kufanyika tu wanawachukua wale watoto na kuwasafisha kuondosha ule uchafu ambao umeingia pale. Jambo hili linaanza kuutia mashaka ushahidi juu ya kesi ya ubakaji.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri Mswada huu tutaupitisha Mungu akitujaalia. Lakini namuomba sana pamoja na serikali kwa ujumla basi itilie maanani juu ya kutoa ushahidi kuwafundisha watu juu ya ushahidi wakati yanapotokea matendo haya ya udhalilishaji wa watoto. Wawape zile kinga ambazo wao watazichukua kwa ajili ya kuharibu ushahidi hii.

Jengine la pili katika ushahidi huu. Mhe. Spika, tumeona kwamba watu wengine wanashindwa kwenda kutoa ushahidi Mahakamani pengine kwa kushuhudia au kwa kujua taarifa juu ya jambo baya ambalo amefanyiwa mtoto. Nasisitiza katika hili kwamba Mhe. Waziri au kupitia serikali kwa ujumla waliangalie sana suala la kuwapa watu elimu ambayo inahusu masuala ya kuhifadhi ushahidi katika matendo ya udhalilishaji kwa watoto.

Mhe. Spika, niende katika kifungu cha 11 kimezungumzia hasa watoto wenye ulemavu. Kutokana na uzito hasa wa suala la wenye ulemavu kufanyiwa vitendo vibaya na jamaa zao ndani au walezi. Katika jamii kwa ujumla naona haikuzungumza sana kutokana na uzito wa jambo hili mimi nilikuwa nadhani kwamba lizungumzwe sana suala la watoto wenye ulemavu.

Namuomba sana Mhe. Waziri zifanywe juhudi za makusudi kuweza kuwatambua watoto wenye ulemavu na wanafichwa ndani, hawajui kama sasa hivi ni mchana au sasa hivi ni usiku, wanaekwa na wanatengwa na jamii. Tufanye juhudi za makusudi Wizara yetu hii kuwatambua watoto hawa ambao wamefichwa na wazazi wao.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 115 cha Mswada huu tumezungumza jambo moja zuri sana. Skuli za marekebisho ni skuli ambao zitatumika kwa ajili ya kuwarekebisha watoto wenye tabia zisizo nzuri. Hili ni jambo zuri sana. Mhe. Spika, huko nyuma mimi sikufahamu lakini nimepata habari kwamba ilikuwepo skuli ya manunda au chuo cha manunda. Hiki kilitumiwa kwa ajili ya kurekebisha tabia za watoto. Inasemekana watoto wengi waliopelekwa kule serikali kwa wakati ule haikufanikiwa badala yake watoto hao walizidi kuwa watukutu zaidi badala ya kurekebisha zile tabia zilizokusudiwa.

Skuli ya marekebisho ambayo itaanzishwa basi ziwe za marekebisho kweli. Serikali ijitahidi na ifahamu kwamba kule mwanzo hatukufanikiwa sijui kwa sababu zipi. Zile sababu ambazo zilipelekea kutokufanikiwa kwetu tuziangalie. Isijekuwa skuli za marekebisho zikawa skuli za maharibiko.

Mhe. Spika, mwisho nadhauri Serikali au Wizara inayoshughulikia masuala ya wanawake na watoto ni vizuri kupitia sheria hii au Mswada huu wa Sheria ikaanzisha lile Baraza la watoto la taifa. Humu halikuoneshwa katika sheria hii. Ni vizuri sana hili lilikuwa lianzishwe kupitia Mswada huu wa Sheria. Baraza hili litawaweka pamoja watoto na itakuwa ni chombo chao cha kutoa kauli juu ya mambo mbali mbali ambayo yanawagusa watoto.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kabisa niseme kwamba Mswada huu naunga mkono kutoka herufi ya kwanza ya Mswada huu ambayo ni G lakini mpaka hefufi ya mwisho R ambayo imeunda neno la Zanzibar. Nawaomba wenzangu Waheshimiwa Wajumbe tuupitishe Mswada huu kwa maslahi ya watoto wetu na kwa maslahi ya taifa.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naona nimalizie hapo na ahsante sana na asanteni sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza nashukuru kupata nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu mdogo tu katika Mswada huu muhimu ambao upo mbele yetu tokea jana.

Pia naipongeza Wizara inayohusika kwa kutayarisha Mswada huu kwa ajili ya kuwalea na kutatunza watoto wetu ili kuwaepusha na vitendo vya unyanyasaji ambavyo hivi sasa vinaendelea kwa baadhi ya watu wasiokuwa na huruma kwa watoto wetu.

Mimi nitazungumza machache tu mengi yamezungumzwa na wajumbe mbali mbali kuanzia tokea jana. Mengi yalikuwa ni muhimu yameshaelezwa. Na mimi nimeona nitie baraka zangu katika Mswada huu.

Mhe. Spika, naamini kwamba watu wanaowanyanyasa watoto hawa ni wahalifu sana. Naiomba wizara inayohusika kama walivyotangulia wenzangu kwa aina yoyote ya ushahidi utakaothibitika juu ya watu wanaowanyanyasa watoto kijinsia watiwe mkononi bila ya huruma ya aina yoyote. Watoto ndio rasilimali yetu na wao ndio wanaotarajiwa kulijenga taifa hili baada ya wazee wao.

Mhe. Spika, jengine ambalo nahitaji kulichangia katika Mswada huu ni kuhisiana na suala zima la Mahakama ya watoto. Ni jambo zuri kuwekwa mahakama ya watoto. Mahakama kuu kwa watoto kwanza ingeanza katika familia. Tukiangalia utamaduni wetu wa Kizanzibari watoto wengi walikuwa wanafanya makosa tofauti, wanaingizwa katika familia matatizo yale yanazungumzwa katika familia. Badala yake yanatatuka bila ya kuyapeleka Serikali Kuu.

Nalizungumza hili kwa sababu jana Mhe. Juma Duni alizungumza kitu kimoja. Alisema kuna kitu hakizungumzwa, sijakisikia na mjumbe yoyote kuhusu habari ya kukosa radhi. Hili limenichoma kidogo nikaona nilikumbushe. Tutakapokuja kuwapa watoto uhuru mkubwa wa kuwashtaki wazee wao, nahofia kujakukosekana kitu kukosa radhi. Kukosa radhi kwa mdomo tu utaliona kama ni jambo jepesi lakini ni jambo kubwa sana.

Mtu yeyote ambaye anakosa radhi ya mzee wake basi mtu huyu basi si rahisi hata kuingia katika pepo ya Mwenyezi Mungu. Jambo ambalo lipo katika maisha ya milele. Mhe. Waziri suala la watoto kuja kuwa na vichwa vikubwa dhidi au mbele ya wazee wao nahofia kuja wakakosa hili suala la radhi, suala ambalo litakuwa ni gumu katika maisha yao ya dunia na maisha yao ya akhera. Pamoja na kuweka haki za watoto basi iwekwe na wajibu wa watoto kwa wazee wao ili kulidhibiti suala hii la kupata radhi za wazee wao.

Mhe. Spika, pamoja na hayo watoto watukutu wapo kama walivyosema wenzangu. Ndio maana kukawa na skuli za manunda hapo zamani kwa ajili ya kurekebisha tabia zao na pia hivi sasa kuli hizi tumezibadilisha jina tunaziisha skuli za marekebisho. Vyovyote iwavyo tujue kwamba watoto watukutu wapo. Mswada huu uzingatie haki za watoto na wajibu wa watoto kwa wazee wao.

Pamoja na hayo Mhe. Spika, ninukuu maneno ya Mhe. Subeti aliyozungumza jana kwamba wale watoto wenye akili taahira walio na matatizo mbali mbali ambayo hawajimiliki wale wanakuwa wananyanyaswa ziada kuliko wale wanaweza kujikurupusha. Sasa hawa ni vyema serikali ikaweka maeneo maalum ya kulelewa watoto hawa.

Katika nchi zilizo na uwezo nafikiri Miswada hii wameipitisha kutokana na uwezo wa nchi zao. Watoto wana maposho maalum ndani ya serikali zao. Sijui serikali yetu sisi itakuwa na posho la namna hiyo au tunaweka Mswada huu halafu tunawaachia wazee majukumu makubwa. Mzee huyu ambaye tunamuwekea mahakama ya mtoto ndiye mzee ambaye anamsomesha mtoto huyu kwa kupitia nguvu zake mbovu. Mzee huyu huyu anatibia kwa kupitia nguvu zake hizo hizo na kwa hali hii na ile.

Wizara yako Mhe. Waziri imejikita kiasi gani kuwasaidia wazee wasiokuwa na uwezo ili kuweza kuwakidhi watoto hawa na kuwalinda watoto na wazee wao yasipatikane haya madhara ambayo tunayahofia kutokea kwa watoto hawa. Mbali ya hayo Mhe. Spika, nimalizie maneno yangu kwa kusema kwamba samaki mkunje akiwa mbichi, kwa sababu akikauka hakunjiki. Msemo huu nautoa kwa kusema kwamba kuna haja kubwa ya wazee na watoto wao ndani ya familia kuwalea vizuri na kuwalea kiuadilifu na kuwafundisha utamaduni wetu wa Kizanzibari tuliourithi ndani ya wazee wetu ili ipatikane amani, upatikane utulivu, upatikane upendo ndani ya Zanzibar yetu. Bila ya malezi mazuri kwa watoto wetu basi hayo yote yatatoweka. Jambo ambalo ndio rasilimali tunayojivunia hapa Zanzibar.

Kwa haya machache Mhe. Spika, nashukuru na mimi kutoa baraka zangu ndani ya Mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, kwanza nami kama walivyoanza wenzangu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kukutana hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya kuendeleza mambo yetu ya Baraza. Pia nikushukuru wewe kunipatia nafasi hii kwa kutoa machache kuhusu Mswada huu ambao hatimaye utakuwa sheria ya Mtoto.

Mhe. Spika, kwa kweli Zanzibar tumefika pabaya kwa watoto wetu. Kiongozi mmoja Mwalimu Nyerere huko nyuma alisema maendeleo yetu ndio

yanayoleta baadhi ya matatizo. Kwa wakati huo alitoa mfano wa ongezeko la watu kwenda kwenye vituo vya afya ambapo nyuma ilikuwa hawaendi, elimu watu waliyoipata ndio iliyowaamsha kwenda kwenye tiba na kukawa na ongezeko la watu. Kwa wakati huo ilikuwa hatumudu kuwahudumia wote. Maendeleo yetu baadhi ya wakati ndio yanayotuletea matatizo.

Kuhusu watoto ni maendeleo yetu ndio yaliyotufikisha hapa tulipo leo. Tuna kazi ngumu kuweza kujitoa hapa tulipo. Mengi wanayoyafanya watoto wetu mabaya chanzo chake ni sisi wazazi wao. Njia zetu za mawasiliano redio, televisheni, simu, hizi tunawapa sisi wenyewe. Michezo wanayoiona kwenye televisheni inachangia kuwafundisha vile wanavyoona mle. Mimi zamani nilikuwa mwalimu, falsafa moja ya uwalimu inasema *children are curious*. Watoto wapo *curious* kwa baadhi ya mambo, lile wanaloliona na wao wanataka kuliiga. Leo wanaona mchezo watu wananyonyana baba upo mama upo, sote tunakaa pamoja na watoto wetu. Sasa tutawalaumu nini na sisi ndio *source* ya yale. Ni televisheni uliyoinunua wewe mwenyewe ndio unayomuachia mtoto afanye vile.

Zamani ilikuwa uharibifu kama huu watoto wanatumia njia ya barua tu na kulikuwa ni ngumu kumfika aliyemkusudia kwa haraka, mara nyengine mashuleni ilikuwa barua zinakamatwa. Leo mtoto mmoja yupo Kengeja mmoja yupo Makangale, wanawasiliana na wanapanga yao. Baba na mama huna habari. Lakini ni pesa yako uliyompa mtoto yule na kumnulia simu ndio iliyomfanya mtoto huyo afikie hapo. Tuna kazi ngumu na ya ziada. Itabidi tubadilishe malezi yetu. Je, kwa hapa tulipofika itawezekana?

Yapo mazuri yaliyofanywa zamani ikiwezekana tuyaige. Na yapo mabaya ya zamani haya tuyawache. Malezi ya zamani yaliyokuwa mazuri yalikuwa ni malezi ya pamoja. Mtoto wangu anapomkosea mtu mwengine yeyote mzee yule alikuwa ana haki ya kumrudi na akija kwangu analia, ukimuuliza umefanyaje? Anasema bwana fulani kanipiga. Huyu baba na yeye anamuongeza kofi. Bila ya kumuuliza kakupiga kwa nini. Leo mambo kama hayo yakitokea baba au mama anafunga kibwebwe kumfuata kwa nini ukampiga mwanangu, na wewe zaa wako, lugha kama hizo. Hapa tunampa mtoto kichwa.
Tuna haja kwa baadhi ya wakati kuwa na malezi ya pamoja, sio ya kupiga lakini ya kuelimisha nyendo bora kwa watoto wetu.

Mimi nilikuwa mwalimu na nilipewa dhamana moja kwa watoto. Nilikuwa mwalimu wa paunia. Nilikuwa nakaa na watoto muda mwingi wa kike na wakiume. Kwa kipindi hicho ilikuwa ni rahisi kurekebisha tabia za watoto. Heshima ya mtoto na mwalimu, mtoto na mzee ilikuwa vyengine kuliko ilivyo hivi leo.

Mhe. Spika, hapa tumeweka kifungu cha hukumu ya mtoto anapofanya kosa. Pengine ni kwenda kumtafutia kazi anayoiweza yule mtoto, mzee au mtu aliyemkosea. Sisi vijijini watoto licha ya kumfanyia kazi mtu mwengine, akimuona baba yake mwenyewe na mzigo anamkimbia. Leo mtoto huyu kafanya kosa kwa mtu mwengine umwambie akamfanyie kazi nyumbani kwake kazi anayoiweza, kwa kweli haiendi. Adhabu iliyekuwepo hapa juu ya mtoto anapofanya kosa bado haikidhi haja. Kwa sababu hatujafikia hatua hiyo ya kuweza kuwamiliki watoto kuweza kutekeleza yale ambayo tunayapanga. Sheria hii mtoto haikumpa wajibu wowote, imemtafutia haki tu. Haji na wajibu ni mambo yanakwenda sambamba.

Sisi hapa tunapodai haki ni lazima tutekeleze wajibu wetu. Kwa sisi wajibu wetu wa kufanya hapa ni kusema, kutetea na kuelekeza. Kwa hivyo tukidai haki, tunahaki ya kudai haki kwa sababu tunatekeleza wajibu wetu. Lakini mtoto hatujamuwekea wajibu wake, tumemuwekea haki yake tu. Wizara ningeiomba hapa itafute kifungu vile vile cha kumuwekea mtoto wajibu wake kwa wazazi wake.

Hapa pametajwa Mahakama za watoto. Mimi naunga mkono tufungue Mahakama za watoto. Lakini wanapotiwa hatiani kuwe vyuo vya mafunzo vya watoto. Pale ambapo kahukumiwa aende chuo cha mafunzo, asiende kuchanganyika kwenye vyuo vya mafunzo ya watu wazima. Tulipokuwa katika Kamati za Baraza, tulikwenda katika vyuo vya mafunzo. Tulikuta watoto waliotajwa katika Sheria hii ni watu chini ya miaka 18 wapo mahabusu kule wamechanganyika na watu wazima, watu wa miaka 18 kwenda juu.
Hapa hii haki ya mtoto imepotea. Kama tunaanzisha Mahakama ya mtoto pia tuanzishe vyuo vya mafunzo vya watoto ili kule watakapokwenda Chuo cha Mafunzo iwe ni kama sehemu ya kufunzwa kama lilivyo jina la chuo, pengine itakuwa ni sehemu moja ya kurekebisha tabia.

Mhe. Spika, hali yetu tuliyonayo lazima tubadilike kwanza sisi wazee ndio tuweze kuwabadilisha na watoto wetu. Hivi leo Mhe. Spika, niseme baadhi ya wazazi tunawaogopa watoto wetu, tunahisi nikimwambia hivi atanijibu vile na nikimwambia hivi tunaogopa kuwa atahamaki labda atatoroka nyumbani. Kwa hivyo, huu woga baadhi ya wazazi tulioujenga kwa watoto wetu ndio uliofikia pahala ikawa watoto wanakwenda jinsi wanavyohisi wao ndivyo. Mhe. Spika, hapa ndipo tunapowaachia watu wa korofi kufanya ule ukorofi wao, ni kweli kuwa katika jamii zetu wako watu wazima ambao wamepoteza mwelekeo kwa sababu mtu mzima mwenye akili timamu baba akaweza kufanya uchafu na mtoto wake wa kumzaa hili ni jambo la kusikitisha na halivumiliki. Mhe. Spika, mbali ya baba na watu wengine kwa sababu uislamu unakataza jambo ambalo hutaki kufanyiwa wewe na mwenzako basi usimfanyie.

Mhe. Spika, ni yupi katika sisi yuko tayari kuona mtoto wake anadhalilishwa na mtu mwengine, sisi sote tuliokuwemo humu hatuko tayari. Lakini wako watu waliokuwa tayari kumdhalilisha mtoto wa mwenzake lakini kumdhalilisha wake atakuja juu kweli kweli hasa falsafa ni kuwa lolote lile ambalo wewe huko tayari kufanyiwa basi na wewe usimfanyie mwenzako. Mhe. Spika, bahati mbaya kuna wenzetu watu wazima wanaotumia wenzao mbali mbali ama kimadaraka au kwa uwezo mwengine au pengine kwa kutumia mabavu yao kutudhalilishia watoto wetu. Kwa hivyo, ningeomba vyombo vyote hivyo husika kuanzia wizara hii ya wanawake, polisi na vyengine vinavyohusika pale ambapo atapatikana mtu hatia hii na ikathibitika basi achukuliwe hatua kali za kisheria.

Mhe. Spika, hukumu ya kifungu iliyotajwa kwa mtu anayedhalilisha watoto hii ya kifungo nahisi mimi ni ndogo mno imetajwa miezi sita nadhani isizidi mwaka mmoja hii hukumu ndogo sana kwa mtu ambaye amethubutu kuvunja utu wa mtoto wetu . Mhe. Spika, mengi tumeyaeleza na mengi yataelezwa lakini tuhisi kwamba tunayo kazi kubwa yakuweza kurekebisha tabia za watoto ili hatimae taifa hili lipate watoto wazuri kuliko huko tulikotoka. Mhe. Spika, Waswahili wanasema "nguvu za maji ni mawe mlimwengu na watoto wake". Kwa hivyo, hapa msemo huu unaonesha kuwa mtu lazima aweze kumlea vyema mtoto wake ili hatimae na yeye aje awe mzuri kama yeye au kuliko mwenyewe.

Mhe. Spika, inawezekana sisi wazazi tutimize wajibu wetu vyenginevyo sisi tutasema kwamba watoto wameharibika, lakini nani aliyewaharibu na chanzo chake kinatokea wapi. Mhe. Spika, kwa hivyo inawezekana tutimize wajibu wetu na wajibu wetu ni kuhakikisha kuwa tunawalea watoto ili hatimae na wao wawe raia wema katika yao. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache na mimi niseme naunga mkono mswada huu ambao unalenga kumlea mtoto wa Kizanzibari kuwa na maadili mema na hatimae kuwa raia mwema wa nchi hii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuzungumzia mswada huu wa mtoto. Kwanza Mhe. Spika, sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha leo salama na nikafika katika Baraza lako hili tukufu. Pili, Mhe. Spika, nakushukuru wewe kunipa nafasi hii kuweza kuchangia mswada huu mtoto. Mhe. Spika, vile vile nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu katika Baraza lako hili tukufu tukiwa tunausubiri kwa hamu sana kuhusu sheria hii ya mtoto.

Mhe. Spika, kwa kuwa jana ilikuwa mimi niwe ni mtu wa mwanzo kuchangia na leo nimebahatika nadhani kuwa mtu wa nne au watano lakini vile vile najua

alilopanga Mwenyezi Mungu ndio linalotendeka. Kwa hivyo, wengi wameshayazungumza wenzangu lakini na mimi nitachangia kidogo niliyonayo ambayo yana umuhimu yake.

Mhe. Spika, kwanza niseme kuwa mswada huu umechelewa lakini kuchelewa kwa mswada huu ndio mafanikio ya kufanikisha kwa sheria hii. Mhe. Spika, kwa sababu tangu Baraza lilopita ilikuwa tunauomba mswada huu wa mtoto uletwe na upitishwe hapa kutokana na madhila ya watoto wanayoyapata, lakini kwa vile Mwenyezi Mungu anapopanga lake hivyo utapitishwa hapa ukiwa na waziri wake Mhe. Zainab Omar Moh'd.

Mhe. Spika, nataka niiombe serikali pindipo sheria hii itapitishwe, basi serikali ichukue mkondo wake kwa wale ambao watawadhalilisha watoto kwa sababu kwani zipo sheria nyingi hapa zinapitishwa lakini nyengine huwa hazitekelezwi. Kwa hivyo, mimi naomba sheria hii itakapopitishwa imuhukumu mtu yeyote yule atakayefanya makosa juu ya mtoto isitegemee waziri, isitegemee mwakilishi, isitegemee mtu wowote sheria hii imuadhibu kwa makosa atakayoyafanya juu ya mtoto.

Mhe. Spika, jengine niseme kuhusu elimu kwa wananchi ni muhimu sana ni lazima walezi, wazazi na walimu wote kwanza wapewe elimu kuhusu hii sheria. Kwa sababu hii sheria ukiiangalia na wenzetu huko nje watasema sasa hivi tunawapa kipaumbele watoto wetu wanataka kuja kututovukia adabu wazee wao. Hivyo ni lazima kwanza wapewe elimu wazazi, walezi na walimu watakaokuwa wanasimamia juu ya sheria ya mswada huu itakayopitishwa.

Mhe. Spika, vile vile jengine ni kupiga marufuku kanda za video. Mhe. Spika, kwa kweli siku kanda za video zinatuharibia sana watoto wetu kuanzia saa moja utakuta banda lina watoto wanaume mabaleghe mna wanaume watu wazima, mna watoto wari, mna watoto wa miaka sita na mitano au saba hao wote wako pamoja wanaangalia video. Je, hii tutasema kwamba watoto hawa kweli hii sheria itawafanya nini wakati watoto hawa wanaingia katika mabanda wanaangalia michezo ambayo haistahiki kuangalia mtoto, tena mtoto huyo anatoka hapo kama saa sita za usiku anatoka na baleghe wanafuatana hujui anaweza kumfanya nini mtoto huyo.

Mhe. Spika, jambo la mwisho niseme kuwa utamaduni wetu wa Kizanzibari tumeupoteza sana kwa sababu zamani ilikuwa mtoto hatembei na kanzu mpaka kwenye goti, mtoto kanzu yake inashonwa mpaka chini inamsitiri maungo yake. Lakini hivi sasa tusiseme ni watoto tu na sisi wenyewe wazee tunachangia, sisi wenyewe tunachangia mama anakwambia mtoto anakwenda na wakati. Mhe. Spika, mtoto kwenda na wakati hilo ni tatizo kwa sababu mtoto yule ikiwa anakwenda na wakati lakini usimfanyie wakati wake kwako

wewe, wewe mtoto huyo ni kumpa heshima na matunzo yaliyokuwa mazuri. Mhe. Spika, leo mtoto utamvisha kanzu mpaka kwenye magoti na shati inakuwa kawoshi, hivi kweli haya ni malezi mazuri kwa mtoto.

Mhe. Spika, haya ni matatizo makubwa ambayo watoto wetu itabidi kuwapa watu kuwabaka kwa sababu mtoto akimuona kavaa vitu kama hivyo anavutia watu huko njiani. Vile vile utawakuta watoto wengine wamevalishwa mawigi, pete za dhahabu, herini za dhahabu huu utamaduni wetu sasa hivi tumeuondosha huu tulionao ndio unatuharibia zaidi watoto wetu. Mhe. Spika, baada ya hapo niseme kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukakutana katika mkutano huu tukiwa wazima na afya njema. Nikushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika mjadala huu. Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa wizara hii pamoja na watendaji wake kwa kututayarishia mswada huu muhimu sana katika nchi yetu kwa maslahi ya watoto wetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Spika, mimi nitaingia kwenye vipengele tu moja kwa moja ambavyo nimehisi kidogo vinataka masawazisho kwa mawazo yangu au viongezwe au vipunguzwe maana yake vyengine vikali sana. Nianze na haki ya kuandikishwa kuzaliwa Nam. 8 kwenye kipengele hiki mimi nahisi hawa wazazi ambao hawawaandikishi watoto wao wakati wa kuzaliwa nao pia waekewe adhabu kwa sababu kumekuwa na mtindo sasa mara nyingi sana utakuta watoto mpaka wanakuwa wakubwa ndio wanakwenda kutafuta targisi ile ya kuzaliwa wao wenyewe watoto, wakati hii ilikuwa ifanywe na mzazi mwenyewe wakati mtoto anapokwishazaliwa.

Mhe. Spika, utakuta kuna fursa nyingi watoto wanakuja wanazikosa kutokana na kutokuwa na vyeti vya kuzaliwa. Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba ile adhabu iliyokuwepo kwenye aya ya 16 ile ya 6,11,13,14(1) adhabu ya kwenda kinyume basi na hii fungu la 8 liongezwe pale ili na wao wawe wanapata adhabu kama ile ambayo wataipata wale waliokuwepo kwenye fungu hilo nililolitaja mwanzo. Hilo ilikuwa ni wazo langu katika hili.

Mhe. Spika, jengine niende kwenye kifungu cha 14 hapa hapana mtoto atakayepewa mateso au adhabu za kikatili au zisizokuwa za kibinadamu au za kudhalilisha au utamaduni au mila zinazoondoa ubinadamu au zenye kuumiza mwili na akili. Mhe. Spika, haya mateso kwa kweli yanaonekana ni makubwa lakini adhabu inaonekana ni ndogo, kwa hivyo nilikuwa napendekeza mimi hapa hii adhabu ya watu wa namna hii iongezwe kidogo ili kukomesha vitendo

vya namna hii. Kwa hivyo, nilikuwa nahisi hii adhabu iongozwe juu kidogo kuliko hii ambayo inaoneshwa hapo katika fungu la 16.

Mhe. Spika, sasa nisogee mbele kidogo kwenye udhalilishaji wa mtoto kifungu cha 15 kuwa mtu yeyote anayekaa, anayesimamia na kumtunza mtoto, hii kwa ufupi ni mlezi. Hapa kidogo mimi nimepata shaka nahisi mpaka sisi wazazi itakuwa haturuhusiwi hata kumpiga mtoto wetu na kwa mila na desturi zetu sisi tunavyolea lazima mtoto anapokuwa anakosea kidogo unatakiwa kidogo umchape. Wakati mwengine kwa bahati mbaya unaweza kumpiga akaumia mtoto hukukusudia lakini inawezekana unampiga huku akajigonga na ukuta basi ataumia, ina maana wewe mzazi akiumia utakwenda kukumbana na ile adhabu ambayo imeoneshwa hapa.

Mimi nafikiria hii sheria hapa ifafanuliwe zaidi ili tuweze kuona namna ya yule mzazi namna gani atakapokuwa anamrudi mtoto akaumia kwa bahati mbaya, basi hii adhabu isiende tu moja kwa moja hata ile kwa bahati mbaya iende kwa yule ambaye amekusudia kufanya kwa makusudi. Hapa kidogo hii sheria ikae vizuri ituelekeze katika hilo.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele nirudi kwenye ile tafsiri ya mtoto, mimi nashauri tafsiri ya mtoto ibakie ile ile ya miaka 18 tusiibadilishe. Mhe. Spika, tukibadilisha sana hapa nahisi tutafika mahala tuje tushindwe kumjua mtoto ni yupi maana yake wengine wanasema miaka tisa tumalizie hapo, mimi nahisi miaka 18 ndio sahihi tusije tukachanganya mambo sana kwani suala la umri la mtoto libakie kwenye sheria ya nchi.
Mhe. Spika, mimi nafikiria hili tulibakishe hivi hivi kama lilivyo.

Mhe. Spika, hii tukiibadilisha sana tutamnyima mtoto fursa mbali mbali ambazo engepaswa kuwa nazo kama raia pamoja na kinga zile ambazo mtoto anapaswa kupata kama sheria za kimataifa zinavyosema. Kwa hivyo, tuubakishe ule umri ili aweze kupata zile fursa mbali mbali ambazo zinatolewa katika mataifa mbali mbali au katika sheria nyengine, tusiibane sana kiasi ya kwamba tukawa tunashindwa kuja kumuweka mahala pazuri.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye kifungu cha 18 hapa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atupe ufafanuzi zaidi juu ya vipi mtoto wa kiume amebaguliwa kwa kushtakiwa katika Mahakama tofauti kwa makosa ya kubaka. Hapa naona mtoto wa kiume atapelekwa kwenye Mahakama kubwa kwa makosa ya kubaka, nahisi hapa itakuwa kama mtoto wa kiume amebaguliwa kupelekwa kwenye Mahakama hizo kubwa ilikuwa na yeye abakishwe kwenye Mahakama ile ile ya mtoto, ili aweze kuhukumiwa kwa mujibu wa mahakama za mtoto. Kwa hivyo, nilikuwa nashauri hapa Mhe. Waziri aje atupe ufafanuzi vizuri ili tuweze kuelewa zaidi.

Mhe. Spika, nikija kwenye kifungu cha 76 kwenye mambo ya kuwasili. Mhe. Spika, hapa mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho atusaidia kidogo kutupa ufafanuzi zaidi ili tuweze kujiridhisha nafsi zetu zaidi kuweza kukikubali kipengele hiki kiendelee kubaki kwenye mswada huu. Mhe. Spika, ingawa kidogo kinaonekana kina matatizo kulingana na mila na silka zetu sisi Wazanzibari tulivyo. Kwa hivyo, mimi nilikuwa namshauri Mhe. Waziri ajiandae kidogo kuja kutupa maelezo mazuri zaidi ili tuweze kujiridha zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu kwenye sehemu za Mahakama za Watoto zaidi ya marekebisho yale niliyoyazungumza sina pingamizi nayo ni kitu kizuri sana na ninaomba tuupitishe mswada huu ili Mahakama hizi ziweze kufanya kazi mara moja.

Mhe. Spika, baada ya michango hiyo miwili mitatu nisipoteze muda mwingi sana niliona haya kidogo ndio yanahitaji marekebisho. Kwa hivyo, nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu na niwaombe wajumbe wenzangu tuupitishe mswada huu kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mkwajuni mimi nauunga mkono mswada huu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa asubuhi hii ya leo, nakushukuru na wewe kunigaia muda kidogo nikazungumza na mimi.

Mhe. Spika, kwanza mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake pia niipongeze serikali. Mhe. Spika, mswada uliokuwa mbele yetu ni hatima ya vizazi vyetu tulivyonavyo na vijavyo. Mhe. Spika, tukisema mtoto ni watoto wote tutakaowataja hapa wa aina zote kwani watoto hawa wana haki kama haki nyengine za wototo wengine katika nchi nyengine.

Mhe. Spika, mtoto ndiye mtoto anataka matunzo, ana haki za ulezi bora, ana haki ya kulala, ana haki ya kuvaa ana haki ya masomo na mambo mengine. Mhe. Spika, watoto hawa Mwenyezi Mungu akitujaalia mswada huu ukipita basi naona kama Mwenyezi Mungu atatujaalia kutufanikishia lile lengo tunalopiga kelele kila siku.

Mhe. Spika, watoto wana idhilali na hawa watoto Mhe. Waziri nikimwambia kwanza kuna watoto waliokuwa wanakosa haki zao wengi sana kimasomo, kimalezi sisi ndio tunaowaona katika vijiji tukitembea. Mhe. Spika, watoto hawa kwanza ukija ukitoa hili fungu la watoto wa kawaida ukija kwenye watoto walemavu waliokuwa hawana akili, hawa watoto wanafanywa kama ni watumwa. Mhe. Spika, akitokea mtoto aliyekuwa ni mlemavu wa akili taahira

nyumbani pako basi tunawashuhudia watu wengine mtoto huyo anaambiwa huyu nitakuwozesha wewe, basi kama korja za kuni sita atachangishwa mtoto huyo kwa tamaa ya kuambiwa ataozeshwa mke. Vile vile watoto hao wanafanyishwa kazi ikiwa kuchota maji atachoteshwa mtoto huyo. Kwa hivyo, hili Mhe. Waziri ayaone yaliyomo majumbani na kwenye vijiji mbali mbali juu ya watoto hawa wenye akili taahiri.

Mhe. Spika, nikija kwenye watoto wa kawaida, watoto wetu waliokuwa ni wazima. Mhe. Spika, hapa wenzangu wamesema kwamba ni maadili ya kimavazi ndio yanayoharibu watoto ni kweli, lakini mtoto wa miaka 3 ana maadili ya kimavazi na anatamaniwa kitu gani mtoto huyo, ana shepu gani ya kumtamani. Mhe. Spika, babu wa miaka 70 ukaweza kumchukulia mwenzako mtoto wa miaka mitatu au minne ukamfanyia vitendo vilivyokuwa havihusiki. Mhe. Spika, mtu kama huyu ni katili wa roho yake na roho za wenzake. Mimi nasema watu kama hao watakapokamatwa basi wapewe adhabu nzito juu ya watoto wadogo.

Mhe. Spika, watoto wanaobakwa na wao ni walemavu wengi ni watoto waliokuwa wana akili taahira waliokuwa hawawezi kupambanua. Hawa na wao wakikamatwa na mtoto huyu na ikistahiki kesi ni kweli basi apewe adhabu nzito kuweza kumtesa kiyumbe yule aliyekuwa hajui kitu chochote.

Mhe. Spika, pia tunataka tupate elimu kwa sababu hawa watoto sasa hivi kuna elimu mjumuisho na imeenea lakini watu wengi hawajui kukaa na watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, mtoto mwenye akili taahira kwanza akupige wewe tu yeye ukimpiga ni kosa. Kwa hivyo, tunaomba katika maskuli ipelekwe taaluma na wao waweze kujua jinsi ya kukaa na watoto wa aina zote wakizidi watoto wenye ulemavu ambao hawajui kitu chochote.

Mhe. Spika, nikiondoka hapa ni kwamba mno inadhuru tusije tukafanya mno tutakuja kudhurika wenyewe kwa sababu yeye atajua mimi nina sheria yangu hii na imeshapitishwa mimi ndiye mimi anaweza akafanya vyengine vyovyote. Mhe. Spika, lazima pawekwe kifungu cha kuwabana na wao watoto kwa sababu mtoto akifika umri wa miaka 17-18 mimi mama yake anaweza akanipiga hata ukija wewe ameshaniuwa, ni lazima tujue hivyo. Mhe. Spika, na sisi walezi majumbani mwetu tuweze kujua kuwa tunakaa na watoto wetu kwa vizuri kwa kuwaelekeza na kuwapa matunzo na mambo mengine yanayohusiana na hayo yote.

Mhe. Spika, pia tuondowe kejeli za watoto kwani mtoto wa mwenzako ni wako, tumeshakwenda mahali mbali mbali mtu anamthamini mtoto wake mtoto wa mwenzake anamuona kama siye mtoto wake, watu walisema mtoto wako na mtoto wa mwenzako ni wako, sio kuwa wewe unamlea mtoto huyu wako wewe

umfanye ni bibi kazi zote umpe yeye akoshe vyombo, afyagie, apike, akutelekee maji ya kukoga na mambo mengine. Mhe. Spika, jambo hilo lisije kuwepo kwa sababu majumbani mna mambo, sisi ndio tunaotembea wanawake.

Mhe. Spika, mwenzangu Mhe. Mwanajuma hapa amesema mambo ya watoto katika michezo. Kweli michezo nayo inaharibu watoto haya mambo ya kubaka wanaona kwenye michezo akifika mitaani na yeye anajaribu kufanya vile vile alivyoona. Kwa hivyo, tunaomba sekta inayohusika iweze kubagua michezo itakayoonekana haifai wasitutilie kwa sababu watoto siku hizi ni wasugu hawataki kuondoka kwenye televisheni. Tunaomba hizi televisheni tunazoziangalia tuwekewe muda, zamani watoto walikuwa wanawekewa muda kwa matangazo, Waziri wa Elimu alikuwa akitangaza ifikapo saa tatu mtoto akikutikana nje atakamatwa ili tusaidiwe ulezi hawawezekani hawa watoto jamani ni masugu. Majumbani tunasema lakini wanajificha, wewe umeshachoka unakwenda zako kupumzika anaifungua televisheni. Sasa labda ufiche vitu vyote hata hiyo tv isiwepo hasa nyumbani.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme tu kwamba kituo chetu cha kulele watoto ni kizuri sana na watoto wetu Mwenyezi Mungu awajaalie wapate afya njema na wote wanaotusaidia, Mwenyezi Mungu awape imani nzuri ya kusaidia. Lakini naona hiki kituo kijengwe na Pemba cha watoto kama hawa tupunguziwe mzigo wa kuja huku tukiomba, kuandikisha mtoto na mambo mengine, kikiwepo kule na sisi tutapunguziwa mzigo. Wale tunaowaona wanafaa kupelekwa kule watakuja kukaguliwa tutawaorodhesha ili tupate ule urahisi wa kupata kituo cha ulezi Kisiwani Pemba.

Mheshimiwa aliyekaa amesema kuhusu kubaguliwa watoto wenye ulemavu hasa wa akili. Hilo si tatizo, lakini hili azimio tulilipitisha wenyewe kwamba tusibaguliwe isipokuwa tu, katika kituo cha kulelea watoto wanaweza wakatengwa pale pale lakini ikawa wanaonana na wenzao ili kupata na wao ile taaluma na zile akili zao kuweza kukaa vizuri. Lakini katika vituo walezi watakaokuwemo muwe na walezi ambao wanajua elimu mjumuisho kuweza kuzungumza na watoto wale wakaelewana. Kwa sababu kwa kuzungumza naye hivi tu haelewi, hata ukizungumza nini haelewi, lakini akipata yule anayejua wanaelewana na akafahamu Mhe. Spika.

Halafu Mhe. Spika, nataka nimuulize Mhe. Waziri, katika hivi vituo vyetu vya kulelea watoto hawa watoto tujue wanaanzia umri gani mpaka watamalizia umri gani. Kwa sababu tuna watoto wanawake na wanaume wote tunawalea katika nyumba moja au watoto wanaume wanalelewa kwao na wanawake wanalelewa kwao? Tunataka kujua hapo.

Halafu katika mafunzo Mhe. Spika, watoto katika mafunzo mimi naomba serikali iweze kutizama sana chuo cha mafunzo kikijengwa kuwe na taaluma mbali mbali, cha hawa awtoto watakaokamatwa mitaani wakaweza kupelekwa kule, kuwe na kama ufundi wa kushona, uwashi na mambo mengine ili wale watoto wakikaa kwa zile siku watakazowekwa kule iwe wanapata taaluma kuweza kupata mafunzo mazuri na wakitoka huko waweze kujiendeleza waondokane na kudhurura ovyo.

Mhe. Spika, mimi nimpongeze tu Mhe. Waziri, juzi katika semina nilitoa sana kilio changu, nimpongeze pamoja na watendaji wake na naunga mkono mswada kwa asilimia mia moja na Mwenyezi Mungu atujaalie apate mafanikio mema kwenye miswada atizamwe sana, kwenye bajeti yake ijazwe mamilioni ya pesa aweze kutukidhia haja zetu katika watoto wetu.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi niendelee kutoa michango kama wenzangu. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu mbele yetu na vile vile nimpe pole kwa majukumu mazito ya wizara hii pamoja na watendaji wake.

Kwa kweli Mhe. Spika, lazima tubadilike katika ulezi wa watoto wetu, kuna msemo usemao kwamba, ‘mimi sigeuki bata nikafuata watoto’, lakini hatujui mfumo wa bata. Mfumo wa bata ni mzuri kwa sababu yeye anakaa nyuma na kutizama kitu gani kitatokea mbele, anawalinda watoto wake, lakini sisi hatujui ile namna ya bata alivyo na tunam-*judge* kwamba labda anafuata watoto na lugha ipo utamsikia anaashiria pale, pengine anawaambia pita huku au huku lakini sisi hatujui lugha ile, lakini ni moja ya mfumo mzuri tuufuate ili tulinde watoto wetu.

Kama walivyokwishasema wenzangu kwamba lazima tubadilike ulezi wa watoto wetu. Sisi wazazi ndio tunaopotosha watoto, tukae kama tulivyopita huko nyuma kwa wazee wetu, mabibi zetu na mama zetu namna walivyolelewa, kulikuwa na ushirikiano wa kulea kwa pamoja. Zamani ilikuwa si mtoto tu kwamba ni wa bwana fulani, lakini analelewa na watu wote, lazima turudi nyuma ingawaje kuna utandawazi na huu ndio ambao unaharibu labda malezi ya watoto wetu kwa kufuata mambo wanayoyaona katika vyombo vya habari na mambo ya nje mengi. Kwa hivyo, ni lazima sisi wenyewe tukae pamoja tulee watoto wetu usione kwamba unalea mtoto wako peke yako, unapomuona mtoto wa mwenzako kafanya jambo basi uwe tayari na wewe mzazi kurudiwa mtoto yule, isiwe kwa nini umekuja kunambia?

Mimi ninapokuja kwako kukwambia juu ya suala la mtoto wako ujue kwamba kiasi fulani nakusaidia na isiwe sababu ya kusema kwamba ah, ndio watoto wa siku hizi hapo ndipo tulipo na ndio tunapoharibu. Mimi nasema isiwe ni watoto wa siku hizi, ulipokee na ulichukulie hatua za kufaa na ujue kwamba mtoto kweli kafanya jambo kamkosea mtu usiseme ndio watoto wote hao, ndio watoto wetu wa kileo, ukisema hivyo ndio unapotosha wale watoto na tutakuwa hatufiki mahali.

Mhe. Spika, anapokuja mwenzio kukwambia jambo ni lazima ukubaliane naye, mimi ulenzi huo ndio mfumo wangu ninaotumia, akija mwenzangu juu ya tatizo la mtoto wangu basi niko tayari hata kuchukua bakora na hilo nimeshalifanya nikampa yule muhusika amrudi mtoto yule, bibi mtu kaja juu akasema atauliwa mjukuu wake, lakini nikamwambia hatauliwa kwa kurudiwa na tangu siku hiyo mtoto wangu kapata funzo na hakufanya tatizo hilo tena wala kumtukana mtu. Kagombwa kwa suala lake mwenyewe lakini alirudi kwa kumtukana yule mtu, basi nilipofanya hivyo hata siku moja hakurudia tena mpaka mtoto yule amekuwa mtu mzima sasa na akili zake. Kwa hivyo, lazima tukae pamoja tulee watoto wetu kwa pamoja.

Mhe. Spika, wale ambao wanachukua watoto wadogo wakawafanya vitendo ambavyo havina mwelekeo kwa kweli ni baadhi ya wenzetu, ndugu zetu, unamchukua mtoto mdogo hana akili kwanza wewe mwenyewe unakuwa na mazingatio gani katika akili yako. Inaonekana sisemi labda kwamba ni hadithi ya kuwa mtu anatokea kuwa na vichwa saba, lakini kichwa kimoja kikishaelekea upande mmoja na chengine kinakosa mazingatipo kabisa. Unamkamata mtoto mdogo unajua kwamba hapa nimemchukua mtoto huyu hata hajafikia umri wa kufanya tendo hili wewe unamchukua tu si unajua kwamba unamharibia maisha yake, wewe utafanya vipi hata usijulikane, lazima patakuwa na kitu ambacho kinajulikana.

Vile vile kuna vyombo vile ambavyo vinapoteza ushahidi wakati mtoto ameshapatwa na tatizo kama lile, lazima wawajibike. Ikiwa kweli mtoto kafanyiwa jambo hili na wewe kwa sababu zako mwenyewe tu za kibinafsi unasema suala hili unalipoteza ushahidi. Kwa hivyo, hili naliomba basi huyo muhusika achukuliwe sheria ya kufaa ili suala hili lisiendelee.

Kama nilivyokwishaeleza kwamba sheria imeeleza mambo mengi tu ndani yake na nampongeza sana Mhe. Waziri. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani nasema sheria hii nimeikubali kwa asilimia mia moja. ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nichukue nafasi hii ya kukushukuru kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia mswada huu, mswada ambao ni muhimu hasa tukizingatia hali halisi iliyopo hivi sasa hapa kwetu.

Kwanza kabisa Mhe. Spika, napenda kuwapa pongezi Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa kazi yao kubwa na nzuri ambayo wameifanya. Kwa sababu ilikuwa ni wajibu wao lakini naamini kwamba wamechukua jitihada ya makusudi kuhakikisha kwamba sasa hivi tunayo sheria ya kumlinda mtoto.

Mhe. Spika, kwa kweli mambo mengi sana yamechangiwa na kwa upande wangu sitakuwa na mengi ya kuchangia kwa sababu tutakuwa tunarudia rudia hayo kwa hayo. Isipokuwa kuna masuala ambayo nimeyaona inabidi niyazungumze nami niweze kutoa mchango wangu kwa hilo.

Mhe. Spika, jana tulizungumzia sana kuhusu suala la umri ambalo tukasema kwamba mtoto akibaleghe kwa dini yetu ya Kiisilamu tayari ameshakuwa mtu mzima. Ni kweli lakini tutizame na mazingira, mtoto wa miaka tisa akibaleghe amekuwa mtu mzima, lakini dini inatwambia kwamba mtu ambaye anaruhusiwa kuolewa au kuowa ni yule ambaye ana akili timamu, ukimchukua mtoto wa miaka tisa na mtu mzima wa miaka 18 kwa sababu mtoto wa miaka 18 angalau kafikia utu uzima, basi yule mtoto wa miaka tisa hawezi kuwa na maamuzi mazuri. Kwa sababu maamuzi mazuri ndio yanayomfanya mtu aonekane kwamba yule ana akili timamu na ni mtu mzima.

Kwa hivyo, tunaposema kwamba tutoe ruhusa sheria iseme kuwa kuanzia miaka tisa basi nina hakika kwanza tunawapa *loop hole* hawa vitangi. Kwa sababu kuna watu wanatumia nafasi hiyo kwa kusema nitaowa baada ya miaka miwili au mitatu ameshamzalisha yule mtoto wa miaka tisa, kumi, kumi na moja au kumi na mbili anamkimbia anakwenda kutafuta mtoto mwengine mdogo, wapo vitangu hao. Je, hiyo ni haki kwa mtoto?

Tunapozungumzia suala la elimu bado mtoto ambaye ana miaka tisa au kumi hajamaliza elimu yake. Sasa sisi tunakaa hapa tunazungumzia kwamba watoto wapewe haki ya elimu, tukishasema watoto waolewe katika umri huo kweli hiyo haki ya elimu wataipata?

Mhe. Spika, mimi nafikiri tuangalie na ubinadamu na mazingira yanakotupeleka. Mazingira yanakotupeleka sasa hivi watoto wetu wote tunataka wawe na elimu tena elimu za juu ili na wao waweze kulijenga taifa lao na kuwa viongozi bora. Mtoto ambaye tutamharakisha kuolewa hasara yake ni kubwa, tena hasara yake sio kubwa kwamba hata anaweza kupoteza maisha.

Hivi sasa kuna kesi nyingi za watoto ambao wameambukizwa maradhi ya UKIMWI kwa sababu wazee wao wamewapa waume wakiwa wadogo, hii ni kweli na wanasema wenyewe. Kuna watoto ambao sasa hivi wanajuta wanasema laiti ningejua wapi wazee wangu wananipeleka ningekataa au ningekimbia nyumbani, tuwaachie watoto wafike kuwa watu wazima ndio waolewe jamani, tusidhulumu jinsia ya kike kwa hilo. Nawaomba waheshimiwa tuwe makini katika maamuzi yetu.

Mhe. Spika, suala la kudhalilishwa watoto. Hivi sasa kumekuwa na tabia kubwa sana ya walimu wa vyuoni (madrasa) kudhalilisha watoto wa kike na wa kiume. Sasa hawa walimu ambao wanadhalilisha wana tabia, watu wenye tabia ya kupenda kudhalilisha watoto wana mbinu zao ambazo wanazitumia nazo ni kujiweka karibu na watoto.

Tulikuwa na kitangi mmoja hapa Unguja alikuwa baskeli yake kaijaza vipambo vyote na mifuko yake imejaa peremende, akawa kila anapopita anafuatwa na watoto, watu walikuwa wanasema anapenda watoto kumbe alikuwa ni kitangi. Sasa na walimu wengine tulionao ni vitangi, mwalimu yule anaweza kuwa yuko Mkwajuni akasomesha baada ya kujulikana kuwa ni kitangi kamharibu mtoto anakuja mjini anasomesha. Nimetoa mfano, anakuja hapa anapewa nafasi ya kusomesha. Sasa naishauri wizara ifanye *police check* yaani lazima walimu wa madrasa wajulikane, wapate vibali maalum kutoka kwa masheha na masheha wawatambue na watoe historia zao. Hilo moja.

La pili, wazazi lazima waelezwe na waweze kumkubali yule mwalimu. Kuna kesi nyingi tu zimeshatokea hapa mjini, mwalimu anaharibu halafu wazazi wanakaa kimya, elimu Mhe. Spika, inahitajika sana kwa wazazi na elimu yenyewe sio tu ya redioni, lazima watambue vitu ambavyo vinaweza kukueleza kwamba huyu kwa kweli ni kitangi na anaharibu watoto. Hata ukiwa ndani ya nyumba yako mzee lazima saa nyengine kama una mwanamme umchunguze, kinamama tuchunguze kwa sababu inaonesha kwama mara nyingi mtoto anaharibiwa na mtu wa karibu, yule mtu wa karibu sio rahisi kum- *suspect*, lakini kinamama mara nyingi wanakuwa aidha hawajui au wengine wana-*take advantage* kwamba hawezi kumfanyia hivyo.

Kwa hivyo, nafikiri wizara yako Mhe. Waziri ina jukumu kubwa sana la kutoa elimu, eliemu ambayo itamfanya mama na baba na watu wote katika jamii kuelewa hawa watu ambao wanadhuru tabia za watu ambao wanawadhuru watoto.

Mhe. Spika, nataka kuzungumzia kuhusu ajira ya watoto, imekuwa ni mchezo sasa hivi wazee hawataki tena majukumu yao, kwamba anaambiwa mtoto nenda kapate samaki ili ujinunulie nguo za sikukuu. Nduo ya sikukuu au ya

skuli ni jukumu la mzee kumnunulia mtoto na hata dini inasema kwamba jukumu hilo ni lake. Sasa leo wazee waekuwa hawataki jukumu hilo na kuwaachia watktk wanakwenda kufanya kazi halafu badala yake watoto wale hawasomi halafu serikali inapata mzigo. Kwa sababu haya yote tunayozungumza mwisho wa mambo ni mzigo wa serikali, pale tutaanza kuilaumu serikali kuwa watu hawakupata elimu, hawana ajira, lakini ukweli unaanza huku chini kwenye jamii.

Kwa hivyo, Mhe, Spika, mimi nasema hata wale wazee, mwenzangu aligusia akasema hata wazee nao wajue wanahukumiwa vipi, lakini hata wale wazee ambao wanawaachia watoto wao kwenda kufanya ajira ambazo wanakuwa walipwa vipesa dijidogo dogo tu shilingi elfu moja au mbili ilimradhi tu aweze kununua fulanna na wale wahukumiwe.

Lamwisho kabisa Mhe. Spika, ninalotaka kusema ni kwamba, wenzangu waliotanguliwa wamesema wazee tuna jukumu kubwa sana. Hili ni kweli, na mengi ambayo yanasababishwa na upotevu wa maadili yetu ni sisi wenyewe. Umefika wakati sasa hivi tujiangalie, turudi nyuma tujiulize tumekosea wapi? Kuna pahala tumekosea na binadamu kuteleza sio kosa, kurejea kosa ndio kosa, tumekosea tujipeleleze, tujitizame pale ambapo tumekosea tujirekebishe. Kwa sababu sasa hivi wazee mtu jirani yako unashindwa kumkanya mwanawe, unaogopa kwa kuona kwamba jirani yako na yeye atakuhasimu na yeye.

Kwa hivyo, mimi naona suala la ulezi kaachiwa mtu mmoja au baba na mama, lakini Mhe. Spika, sio hilo tu, jamani kuna wanawake wengi wametelekezwa humu na watoto inasikitisha Mhe. Spika. Wengi wametelekezwa na watoto wanawake wanalea wenyewe, ndio maana unawakuta wanawake wamebeba masufuria ya mihogo, vyakula wanakwenda kuuza kwa sababu wanawake wanataka kuangalia familia zao, wanataka kusomesha watoto wao na hawana mbinu, ameeshaolewa akiwa na miaka 15 au 16 ameshazalishwa watoto watano, sita ameachiwa peke yake ulezi yeye amekwenda kutafuta mwengine wa miaka tisa wa kwenda kumuowa. Itaendelea mpaka lini hii kama hatukuweka sheria kama hizi?

Mhe. Spika, baada ya hapo na mimi kwa niaba ya UWT naunga mkono mswada huu na ninaiombea Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kila la kheri na Mwenyezi Mungu atawajaalia wataweza kutekeleza lile ambalo wamelikusudia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kupitia kidogo na kuongeza mawazo yangu kwenye mswada wa watoto. Kwanza nampongeza jirani yangu jimboni kwangu Mhe. Waziri kwa mswada wake huu.

Mimi kidogo Mhe. Spika, labda naweza nikatofautiana na wajumbe wengi waliotangulia. Baada ya kuusoma mswada huu na kuupitia kidogo nimepata mawazo kwamba mengi kati ya yaliyokuja tuliyoletewa yanatokana na tamaduni za kimagharibi. Tamaduni ambazo tayari zimeshajijenga kikamilifu kiuchumi na kijamii. Tamaduni ambazo zinajitosheleza kiuchumi tofauti na tamaduni zetu za kiafrika ambazo kaya zetu hazijajitosheleza na ndio tunaomba misaada ya uhakika wa chakula na lishe ili na sisi tuweze kuzitosheleza familia zetu kwa lishe.

Nasema haya kwa maana ya kwamba labda naweza na mimi nikaongeza kwamba, sisi tumetafsiri mtoto kwa lugha moja tu ya Kiswahili, lakini wenzetu wa Kingereza na wa lugha za Kiarabu wakifika miaka 15 wana lugha nyengine wanazozitumia ambazo labda naweza kusema Waingereza wanasema *youth*, wengine waliosoma *psychology* wanaziita *teenage* na Wafaransa wanasema *ressun* na wengine wana lugha zao nyengine Warabu wanasema *Shaabab* na mengineyo wala sio *Wallad.* Sasa katika jamii zetu za Kiafrika hizi mimi kama ni mzazi mtoto akifikia umri wa miaka 17 au 18 anakuwa ni mtegemezi wangu katika jamii au katika koo yangu, kwa maana ya kuwa anakuwa ni msaidizi katika uchumi. Sasa ukiniambia nisimpangie kazi nachelea kwamba baadae tunaweza kuja kugongana na mtoto huyo akarudi nyumbani akakuta labda kwenye sahani yake nimemfunikia jiwe, kwa sababu hakunisaidia katika ushiriki.

Mimi binafsi ninalo gari la ng'ombe Mhe. Spika, ambalo kijana wangu nimempa kwa ajili ya kufanya *topping up* ya maisha yangu mimi na yeye. Sasa labda ningesema kwamba kama umri wa kufika miaka 17, 18 tukamtafautisha na huyu ambaye atakuwa ana umri wa mwaka mmoja mpaka 12. Kwa sababu sisi Afrika utamaduni wetu haukubali hivyo, unatuambia mtoto akifika hivi kimaisha yetu, kiuchumi tayari tunampangia kwamba na yeye baada ya miaka 20 na ndivyo tunavyofikia umri wa kuowa tunakuwa tunamuandaa kimazingira kama hayo. Sasa yeye huyu tungelimtafautisha na huyu wa miaka minane, kazi zetu wanazifanya wao zaidi kwa sababu ya kufanya maisha yetu yaendelee, kinyume chake hatuwezi kukamilisha mlo wa siku bila ya kuwapata wao.

Nasema hivi kwa uthibitisho mwengine wa zao letu la karafuu. Miaka michache iliyopita nyuma serikali ilikuwa inafunga shule inasema tunakwenda kuokoa zao la karafuu, zao ambalo ni hatari sana. unaanguka unakufa, unaanguka unaumia kiungo chochote cha mwili. Sasa nina wasi wasi wakati wowote zao hili linaweza likawa jingi tukafunga skuli kwenda kuwapeleka wanafunzi wetu kwenda kuchuma zao hilo la karafuu, hiyo ni ajira ngumu sana.

Lakini katika zao hili hili ndio tegemezi kubwa kwa mfano, sisi tulioko katika visiwa ambavyo zao hili linapatikana, kule bila ya kwenda kuchuma karafuu huwezi ukapata pesa ya kununua shati yako, huwezi ukapata pesa ya kununua mabuku, huwezi kupata pesa ya kuweka kwa ajili ya safari wakati itapofungwa skuli. Sasa tukisema mtoto wa miaka 17 ambaye tayari tunamwita *shaabab* asiende kwa sababu hiyo ni kazi ngumu itakuwa kiutamaduni wetu ni kosa. Nafikiri hapo wizara ingeangalia je, huyu aliye na miaka 16 na yeye asiingie katika mfumo kama huu?

Twende katika suala la wasichana, na wasichana na wao ni hivyo hivyo. Kule Ulaya wenzetu wana *facility* moja ambayo sisi huku hatuna, sasa *psychologically* inaweza ikatusumbua ukakuta pengine msichana huyu amekwenda kujitundika kwa sababu *psychologically* mtoto akifika miaka 16 au 17 tayari ameshafikia *maturation period* anatakiwa aolewe. Sasa sisi huku tunasema kwamba aa huyu asiolewe na yeye atakuwa anayo haki yake ya msingi, haki ya binadamu, anaweza akampeleka baba yake mahkamani akamwambia baba kwa nini huniozeshi? Wakati huo baba na mama pengine wameachana tunaweza tuka-*create conflict* baba na mama pengine wakaachana kwa sababu mtoto wao mmoja hakukubaliana na yeye kwamba mtoto huyu aolewe.

Sasa sisi Ulaya au wale wa Ulaya bahati nzuri niliwahi kuishi kidogo, wao wana *boy and girl friend*, wanazo zile ambazo zinaruhusu baadhi ya mambo kuyapata, nafikiri mnanifahamu lakini hapa kwetu hayapo.

Kwa hiyo, *psychological* unaweza ukakuta pengine mtoto yule kishaathirika hata huko skuli ukimpeleka asisome. Mhe. Spika, Dk. Sira Ubwa Mamboya yupo hapa nafikiri ataniunga mkono. Madaktari wengine tukenda hospitali wanatushauri wanatwambia ongeza mke wewe kwa sababu akili yako haijatulia, au wewe mwanamke unahitajika uolewe kwa sababu hujapata mume.

Sasa tamaduni hizi tofauti, mazingira haya yanatufanya sisi tuwe tofauti na wale watu walioko Ulaya. Kwa hiyo, tungewaruhusu wakaweza kufika miaka 17 basi haya wakaolewa yasije yakatokea mengine. Hizi kaya zetu zinaweza zikatengana kwa sababu ya masuala kama haya. Inawezekana pengine mmoja kati ya wazazi akawa ni *layman* hajui chochote mwengine akawa anafahamu lakini katika kufahamishana wasifikie suluhisho. Pengine katika familia watu wanne tayari wameshafika kidato cha pili ikawa ndio mwisho, mmoja kati ya wazazi akawa anamwambia mwenzake hapana katika hili utanisamehe kwa sababu fulani kashindwa. Kwa hiyo, hii inaonesha kwamba kutokana na hivi huyu itabidi tumpe mume asije akatuharibikia. Sasa wakigongana hapo unaweza ukakuta ugomvi katika kaya umeshajitokeza.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba Mahakama zetu lazima nazo tuziangalie. Mhe. Spika, hivi sasa tatizo tulilonalo kubwa Mahakamani ni mrundikano wa kesi zinazobakia miezi miwili, mitatu, sita mpaka mwaka. Sasa sisi hapa tunakwenda na sheria tunasema mtoto miaka 18. Tuangalie kesi zetu, kama tunaanzisha Mahakama ya Watoto basi tuangalie zaidi. Inaweza ikafika mtoto au huyu kijana kashtakiwa akiwa na umri kabla ya miezi sita au mitano ya kufika miaka 18, lakini ndani ya miezi sita kesi haijamalizika akafikia umri wa miaka 18 ikawa labda tutamuondoa katika kundi la utoto.

Sasa sheria isije ikagongana ikawa huyu tumhukumu katika kundi gani. Kundi la kwamba tayari ni mtoto au kundi la kuwa ameshapitia huyu utoto wakati alipotenda kosa alikuwa ndani ya umri wa miaka 18. Kwa hiyo, ucheleweshaji huu wa kesi uondoshwe ndio suala la kuangalia.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo kutufikisha hapa leo. Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu leo. Tatu namshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu mzuri tu ambao utatusaidia sisi pamoja na watoto wetu.

Mhe. Spika, wenzangu waliotangulia wamezungumzia mengi sana lakini mimi nitazungumzia kuhusu udhalilishaji wa kijinsia. Mhe. Spika, nchi yetu tunasema kwamba waislam 99 *fil* 100. Mhe. Spika, ninavyoamini mimi waislam wote wameletewa kitabu cha kur-an. Kur-an imetuongoza na ikatupa sheria zote, lakini waislam sisi tumeacha kukifuata kitabu cha Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, udhalilishaji wa kijinsia hautomhusisha mwanadamu yeyote madhali hakufuata sheria ya dini ya kiislam. Kwa sababu waheshimiwa wengi wamesema hapa kwamba watu waoe wake wanne lakini hawa wanaodhalilisha kijinsia wanadhalilisha watoto wa miaka mitatu. Je, aozeshwe mtoto wa miaka mitatu kwa sababu ana hamu nyingi. Kwa hivyo, kukosa sheria zinazomfanya mwanadamu awe na hofu ndio udhalilishaji wa kijinsia umetuzidi Zanzibar. Mhe. Spika, ningeliomba zitumike sheria ambazo zitamfanya mtu awe na hofu hasa kwamba nikifanya jambo hili mimi nitashika adabu yangu.

Mhe. Spika, sisi hapa tuna Chuo cha Mafunzo ukimpeleka mtu aliyemdhalilisha mtoto wa miaka mitatu ndio unakwenda kumfunza aje tena. Kule chakula chake anapigwa supu basi, anafungwa muda wa miaka mitano akija huku anaanza kudhalilisha watoto wadogo na watu wazima.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ningeomba iwekwe sheria hasa ambayo itamfanya mtu aogope hata kumdhalilisha mtoto mdogo mpaka mkubwa.

Mhe. Spika, tuna Mahakama zetu tumeziweka makaazi ya kiislam, sasa makaazi ya kiislam watakuwa wanahukumu sheria ya kiislam au sheria gani.

Mhe. Spika, udhalilishaji sasa hivi unazidi kupita kiasi. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri wakati mswada huu ni mzuri basi atazame na sheria zaidi ambazo zitakazotufanya sisi tuwe na hofu. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ametuletea kitabu cha kur-an na akatutilia zile sheria kwamba baadae kule atakwenda kutuuliza "Je, wanadamu wangu nyie nilipokuwekeni katika dunia ile mmezitumia sheria zangu?" Hazikutumika.

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti, alizungumza kwamba jamani tumekosea nini? Mhe. Spika, tukumbuke, tulilokosea waislam wa Zanzibar hatutumii sheria za kiislam kama zilivyoletwa na Mwenyezi Mungu. Kwa sababu sheria hizi za Mwenyezi Mungu ndio chombo cha muislam. Leo tunasema sisi waislam asilimia 99 lakini hakuna sheria hata moja ya Mwenyezi Mungu tunayoitumia. Je, Mwenyezi Mungu atakuwa radhi na sisi?

Mhe. Spika, waheshimiwa wengine wamesema kwamba hivi sasa tunatumia sana tabia za magharibi, lakini sisi tabia za magharibi hatujaona hata siku moja ndani ya televisheni mzungu kumdhalilisha mtoto wa miaka mitatu. Isipokuwa sisi waislam wa Zanzibar hivi sasa ndio tumezidi kudhalilisha watoto wa miaka miwili au mitatu kwa sababu ile sheria tumeikosea hatuifuati. Kwa hivyo, ningeliomba zitungwe sheria ambazo zitaweza kututia hofu sisi waislam wa Zanzibar tuliozidi kudhalilisha.

Mhe. Spika, mzee wa miaka 60 anamdhalilisha mtoto wa miaka mitatu anakwenda kuwekwa Chuo cha Mafunzo mtoto ameshakufa huku. Kweli Mhe. Spika, tutaendelea hivi.

Mhe. Spika, mimi sitaki kuchukua muda mkuwa isipokuwa namshukuru Mhe. Waziri kwa mswada wake huu na mimi naunga mkono pamoja na wananchi wangu wa Matemwe mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru na kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya. Lakini pili nichukue fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia angalau kidogo mswada huu. Tatu pia nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa mswada huu waliotuletea hapa ambao utamlinda mtoto wetu na kumpatia haki zake.

Mhe. Spika, nichangie kidogo tu kwa sababu wenzangu wote waliotangulia wamechangia vizuri na niseme mengi wameshayasema. Lakini na mimi naona nichukue fursa hii niweze kuchangia machache.

Mhe. Spika, mchango wangu utakuja kwenye sehemu ya pili kwenye Maslahi Bora na Haki za Mtoto. Mhe. Spika, maslahi bora na haki za mtoto niseme sisi wenyewe wazazi tujipange vizuri ili tuweze kuona mtoto wetu anapata maslahi bora na zile haki zake. Nikisema hivyo, niseme sisi wenyewe wazee tuna tabia ya kuwaachia watoto wetu bila ya kufuatilia nyendo zao mapema mpaka pale ambapo athari imeshatokea juu ya mtoto hapo sasa zinaanza kuja lawama za kulaumiana sisi wazazi kwa wazazi.

Hili Mhe. Spika, niombe sisi kama wazazi tuweze kuchukua hatua hizi mapema za kuweza kushughulikia nyendo za watoto wetu mapema ili kujikinga na hizo athari zisije zikatokea. Nalisema hili kwa sababu niende kwenye lawama kidogo kwa baba zetu. Athari ikitokea tuseme ya mtoto amepata ujauzito, basi utalaumiwa mama, utashambuliwa na pengine hata talaka utapewa.

Lakini hatuangalii ule wakati ambapo mtoto yupo katika nyumba baba akirudi kazini haulizi kama jamani watoto wangu wako wapi sasa hivi na wanafanya nini huko waliko, ili akaweza kujua kama wanangu wamekwenda skuli au wako chuoni au *tuition*. Hii itamjenga mama kwanza kuwa na hofu ya kuweza kujua kwamba akija baba yenu atauliza kama hakuoneni. Kwa hivyo, watoto saa hizi muweko nyumbani kama hamna kazi nyengine huko nje. Hata na mtoto mwenyewe ataweza kujenga hofu kwamba tayari wale wazazi wake wanamfuatilia kila wakati kujua taratibu zake na wapi anapokuwa.

Mhe. Spika, jengine nililete tena kwa baba zetu talaka zile zisizokuwa na mpangilio, talaka zinatoka kiholela holela, hizi nazo zinasababisha watoto wetu kukosa maslahi bora na haki zao. Kwa sababu tunapoachana watoto wanayumba, pengine watachukuliwa na mama lakini hana uwezo wa kuwaendesha pengine yeye mwenyewe hana kazi.

Mhe. Spika, mwenzangu Mhe. Mgeni Hassan Juma amesema pale kama utaona sasa mama amejitwika sufuria anakwenda huku na huku ili ahakikishe watoto wake wanaweza kupata elimu. Hili kinababa wanatuachia sana na hapo ndipo tunapopata wimbi la watoto hata wale wa mitaani kwa kuonekana wanazurura na hata kufanya kazi zile ambazo bado wao hawajafikia kuzifanya.

Mhe. Spika, pia nimuombe Mhe. Waziri kwa mswada huu aliotuletea ili sheria hii iweze kutufaa itakapopita na aweze kutusaidia kutupatia nakala pale ambapo itakuwa imeshapita kuwa sheria, ili na sisi kama viongozi kuwa na nakala ambazo zitatusaidia wananchi wetu wanapopatwa na matatizo kule

vijijini. Wakati anapokukimbilia wewe kama kiongozi wake aweze kupata ushauri, kwa hiyo na wewe unaweza kuwa na kitu cha kuweza kumsaidia kwa kosa hili ambalo limetokea basi hatua hii na hii ichukue. Hii inaweza ikatusaidia sana na wananchi wetu wakaweza kuwa na pahala pakukimbilia na kupata mwelekeo.

Mhe. Spika, nije sehemu ya tatu ambayo hapa imeeleza kuna Mahakama ya Watoto. Mhe. Spika, kwanza tunashukuru na tunasema pamoja na kuwa huwa hatuombi yale madhara watoto yawatokee ili waweze kufikishwa Mahakamani. Lakini iwapo pia itapatikana Mahakama ya Watoto itakuwa ni bora kuwepo kuwatenganisha wao na watu wazima.

Lakini ndani ya Mahakama hizi Mhe. Spika, kuna *assessors* mimi ningeomba wapatiwe mafunzo ili waweze kwenda sambamba na yale ambayo yanakusudiwa pale. Maana *asseesors* wanakwenda pale kwa sababu ya kumtetea mtoto lakini hajui sheria wala kipengele hata kimoja ambacho kinaweza kikamtetea mtoto, anatumia busara zake tu na hekima ya ule utu uzima wake.

Mhe. Spika, nije kwenye udhalilishaji wa watoto. Mhe. Spika, kwa kweli jambo hili mimi mwenyewe binafsi au hata niseme hili Baraza lako tukufu lote linasikitishwa na vitendo hivi vya unyanyasaji wa watoto. Kusema kweli udhalilishaji huu wa watoto kijinsia mimi nazidi kukereka sana hasa ninapoona hili wimbi kubwa liko katika Mkoa wangu wa Kaskazini Unguja. Kila habari zikitajwa hapa za udhalilishaji wa watoto basi unaambiwa mkoa wangu unaongoza, ni kitu ambacho kinanipa masikitiko makubwa sana.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kuwahamasisha wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wasiogope kutoa ushahidi pale ambapo jambo limethibitika kuwa kweli limetokea ili wale wahusika waweze kupata adhabu kali za kisheria. Hili wimbi ni kubwa na baya ingawa linatokea kote lakini kwa kuwa linasemewa sana kwangu na mimi linaniuma.

Mhe. Spika, niwaombe hata Masheha kuweza kulitilia mkazo au kuwaelimisha wananchi wa ndani ya shehia kuhusu jambo hili ili tuondokane na suala hili baya lenye uchafu mkubwa.

Lakini Mhe. Spika, ndani ya udhalilishaji huu kuna ule ambao umesema wale watoto wadogo sana hichi kitendo mimi ninakiita cha ukatili. Kwa sababu kumfanyia ukatili mtoto wa miaka mitatu au minne mtu mzima ambaye una miaka 60 ni kitendo cha ukatili. Hili la watoto wa miaka mitatu mpaka minne na wale ambao wanawabaka watoto wao waliowazaa, hichi ni kitendo kibaya, cha aibu na cha kinyama kabisa. Lazima itakapopita sheria hii na mtu

atakayebambwa na kosa kama hili basi mimi nasema adhabu yake iwe kubwa zaidi ili iwe funzo kwa wale watu wengine wasifanye makosa kama haya.

Mhe. Spika, kwa kuwa wenzangu wameshazungumza sana juu ya matatizo haya na wameeleza vya kutosha basi na mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja niunge mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia na *inshaallah* Mwenyezi Mungu ataujaalia utapita kwa vizuri tu. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia mawili matatu yanayohusiana na mswada huu wa sheria inayohusiana na watoto.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku hii ya leo kuwepo hapa kwa ajili ya kujadili Mswada wa Sheria ya Mtoto Itakayotoa Haki na Maslahi Bora ya Mtoto na mambo mengine yanayohusiana nayo.

Lakini pili nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuwasilisha mswada huu mbele ya Baraza hili mswada ambao hakuna atakayebisha kwamba ni mswada muhimu na kwa sababu umezingatia zaidi maslahi ya watoto wetu.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe lakini na mimi kama mzazi mwenye watoto nimeona niweke mchango wangu kwa niaba ya wananchi wangu ili kuonesha kuunga mkono kwangu kwa mswada huu.

Mhe. Spika, kama madhumuni ya mswada huu yalivyoelezwa kwamba ni kupendekeza au kutungwa kwa Sheria ya Watoto ya mwaka 2011 kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za watoto unaoendelea hapa nchini. Aidha, sheria nyingi zinazohusiana na watoto zimesambaa katika sheria mbali mbali hivyo inakuwa ni vigumu kuweza kushughulikia masuala ya haki ya watoto kwa umakini.

Mhe. Spika, madhumuni ya mswada huu ni mazuri na sote tunakubaliana nayo lakini matatizo yanakuwepo wakati wa utekelezaji wa sheria. Mhe. Spika, Baraza lako hili tukufu limekuwa likipitisha sheria mbali mbali na ndio kazi yetu na ndio jukumu letu, lakini tatizo linakuwa katika utekelezaji wa sheria. Nimuombe sana Mhe. Waziri sheria itakapopitishwa na tunaamini Waheshimiwa Wajumbe wengi wataipitisha kwa sababu ni wazazi, basi iweze kutumika ipasavyo na kwa mujibu wa sheria iliyopo na kwa sababu Wizara hii ya Ustawi wa Jami, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ndio itakuwa msimamizi mkuu wa sheria hii.

Mhe. Spika, tumeshuhudia vitendo vingi vinavyofanyika katika jamii zetu, vitendo ambavyo kwa kweli vinasikitisha. Lakini cha kusikitisha zaidi ni pale ambapo huoni hatua yoyote inayochukuliwa juu ya vitendo ambavyo vinatokea.

Mhe. Spika, hivi karibuni katika jimbo langu la Magomeni nadhani wengine mmesikia kwenye kipindi cha mawio, kwenye magazeti kumekuwa na vitendo vya udhalilishaji vya aina hii vinavyotokea. Kuna Maalim kwenye madrassa fulani alikuwa amezoea kufanya vitendo vya kuwadhalilisha watoto wa kiume, lakini cha kusikitisha mtu yule hukumu yake amefungwa miezi mitatu na asingefungwa kama kusingekuwa na ushahidi. Lakini hakimu inaonekana ameridhika na ushahidi uliotolewa na ndio maana amemfunga mtu yule kwa miezi mitatu tu. Inasadikika mtu huyu ni mzoefu, amezoea na amekuwa na tabia hiyo, lakini wanasema eti huyu mtu ana mashetani ambayo ndio yanayomfanya awe hivyo jambo ambalo halikubaliki.

Mhe. Spika, sheria hii imeeleza mambo mengi na tukianza kuyataja moja baada ya moja basi hatuwezi kuyamaliza. Lakini mengi inaonekana ni yenye umuhimu kwa wakati wetu. Pamoja na kwamba sheria hii chimbuko lake kama alivyoeleza Mhe. Waziri linatokana na mkataba ulioridhiwa na Tanzania na baadhi ya wajumbe wamesema kwamba limeelekezwa zaidi katika tamaduni zile za kimagharibi.

Lakini mimi naamini kwamba pamoja na yote ambayo yameelezwa mswada huu kabla ya kuletwa hapa umepita katika maeneo mbali mbali. Mhe. Waziri ametufanyia semina ametueleza katika maeneo ambayo wamegusia na kwa sababu mswada huu una mambo yanayohusiana na dini yetu ya kiislam basi hata mashekhe na wao wameweza kuweka *input* zao.

Sisi Mhe. Spika, sio mashekhe na wengine sio wanasheria lakini tunajaribu kila wakati kutumia maarifa yetu, akili zetu, uwezo wetu na busara zetu ili kuona kwamba sheria hizi tunazozipitisha hapa hazina athari kwa dini yetu na katika jamii zetu. Ninaamini katika kufanya hilo na kwa nia safi basi Mwenyezi Mungu atatusamehe katika yale yote ambayo tunayafanya hapa.

Mhe. Spika, kifungu cha pili cha mswada huu kimezungumzia ufafanuzi kwa neno la mtoto ambapo Mswada wa Sheria unasema “Mtoto ni yule mwenye umri usiozidi miaka 18”. Kwa kweli Mhe. Spika, kumekuwa na mawazo tofauti kutoka kwa wajumbe. Lakini si wajumbe tu hata hii sheria yenyewe ukiingia ndani kuna baadhi ya matendo yanakubaliwa na watu wenye umri wa miaka 15, kuna baadhi ya matendo sheria imewaruhusu watu wenye umri wa miaka 16 halikadhalika na mambo mengine.

Kwa mfano, sheria imemruhusu mtoto wa miaka 15 kufanya kazi lakini imeeleza kazi anazotakiwa kuzifanya zile ambazo hazioneshi mazingira magumu na ikatajwa kama kwenye migodi na mambo mengine. Lakini kuna vifungu vyengine vya sheria vimezungumzia mambo yanayohusu watoto wa umri wa miaka 14 ambayo sheria imewaruhusu. Kwa hivyo, inaonekana bado tafsiri hii haijawa vizuri.

Mhe. Spika, mimi kwa maoni yangu nahisi basi umri wa miaka 15 uwe ndio kipimo cha mtoto, atakapozidi zaidi ya miaka 15 basi hapo achukuliwe tena kuwa ameshaanza kuwa mtu mzima.

Mhe. Spika, katika mswada huu pia kumekuwa na baadhi ya maneno ambayo yanahitaji kuwa na tafsiri. Kwa mfano, mateso. Neno "mateso" linahitaji tafsiri na kwa sababu mbele yake kuna kifungu huko, mtu atakayemtesa mtoto atakwenda Chuo cha Mafunzo. Sasa hili neno "mateso" linahitaji kuwa na tafsiri, ili wenzetu watoa hukumu waweze kujua nini nilichokusudiwa hapa. Lakini kuna neno "kuwarudi watoto". Nini kumrudi mtoto, hili nalo linahitaji tafsiri. Sisi tunajua kumrudi mtoto mara nyingi ni kumpiga, lakini inaweza kutokezea maneno mengine ya kumrudi mtoto.

Kwa hivyo, neno "kumrudi mtoto" linahitaji kuwekewa tafsiri, kwa sababu kuna kifungu hapa cha 14(2) kama sikosei kinazungumzia juu ya wazazi wanaweza kuwarudi watoto wao katika hali ambayo haitomzuia mtoto ustawi wake wa kimwili na kiakili. Sasa neno "kuwarudi watoto" nahisi linahitaji kufanyiwa ufafanuzi.

Kuhusu neno "kutelekeza mtoto". Mhe. Spika, neno hili nalo lina aina nyingi na linahitaji tafsiri. Kwa sababu siku hizi kumezoeleka ama kwa wazazi wa kiume au wazazi wa kike pale wanapofika pahala wakaachana na yule mama ana mtoto pengine mdogo wa miezi sita, saba, miaka miwili au miaka mitatu basi wakishaachana tu kutokana na hasira zake, basi anaweza kumuachia baba yule mtoto, pengine ni mtoto mchanga na hiyo ni kwa nia ya kumkomoa. Mama yule anafunga virago vyake anaondoka pale na kumuachia baba yule mtoto mchanga, anajua hana la kumfanya, pengine mtoto yule ananyonya. Sasa sijui katika tafsiri hii juu ya kumtelekeza mtoto inakuja katika sura hii kwamba mzazi atakayefanya kitendo kama hicho cha kumuacha mtoto mchanga kwa baba yake, eti kwa sababu kaachwa, kwa hivyo huyo atakuwa ametenda kosa. Kwa hivyo, neno "kutelekeza" nalo litahitaji lipate tafsiri, ili watoa hukumu wapate nafasi nzuri ya kutoa hiyo hukumu.

Mhe. Spika, hata kina baba na wao wana desturi ya kutelekeza. Unaweza kumuacha mama na watoto ukawa huwashughulikii kwa chochote nap engine mtoto yule bado yuko kwenye umri wa kutaka kushughulikiwa na hii nayo

inaweza kuwa ni kutelekeza. Lakini kuna kutelekeza kwengine mtu anaweza kumchukua mtoto akamtupa pahala na akaondoka akaenda zake, na yeye anakuwa amemtelekeza. Kwa hivyo, neno "kutelekeza" lina tafsiri pana, linahitaji kutolewa ufafanuzi kuwa limekusudia nini au limekusudiwa vipi katika sheria hii.

Mhe. Spika, katika hali ya malezi ya mtoto, sheria hii naona imewasahau walimu. Walimu wetu wana nafasi kubwa sana ya ulezi wa watoto wetu na kwa sababu karibu nusu ya siku watoto wale wanakuwa chini ya milki ya walimu. Mhe. Spika, mimi nina mtoto wangu anasoma darasa la saba katika skuli ya Al Haramain, basi anatoka nyumbani saa 12:30 anarudi nyumbani saa 11:30 za jioni. Sasa utakuta muda wote karibu masaa 12 yuko skuli chini ya dhamana ya skuli sio dhamana yangu. Lakini sheria hii haijazungumzia chochote juu ya mwalimu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri aje atuambie je, walimu hao hawaruhusiwi kuwarudi watoto, sheria hii imewafunga kuwarudi watoto kwa maana ya ilivyokusudiwa humu, kuwarudi watoto katika hali ambayo haitomuumiza mtoto ustawi wake, kimwili na kiakili na kwa sababu hapa pamezungumziwa wazazi na katika tafsiri ya wazazi walimu na wao hatukuwaweka kama ni sehemu ya wazazi au walezi. Kwa sababu sheria hii kama wenzangu walivyotangulia kusema kuwa imechukua zaidi zile silka na tamaduni za Kimagharibi kwa wenzetu wazungu kwa hapa kwetu. Kule mtoto hapigwi hata akifanyaje.

Mhe. Spika, sasa tulinganishe hali ya wenzetu na tulinganishe na hali yetu sasa hivi. Kama mtoto itakuwa hakuna tabia ya kumrudi rudi anapofanya makosa na jinsi atakavyokuwa. Sidhani kama tutaweka utaratibu kama huu watoto wetu watakuwa katika zile silka nzuri ambazo sasa hivi tunasema kwamba watoto wako katika, Mhe. Spika samahani, ukifananisha watoto wa kizamani na watoto wa leo. Sisi tulipokuwa tukilelewa huko zamani ilikuwa wazee wetu wanaturudi, ukienda skuli ukifanya matatizo unachapwa viboko. Tulikuwa tunaamini kwamba njia ile ndio inayomuweka mtoto katika njia nzuri, lakini kwa utaratibu mzuri. Lakini mtoto akishafahamu kwamba hakuna utaratibu wowote wa kumuwezesha yeye kumrudi, basi kwa tabia ya watoto wetu wanaweza kufanya vinginevyo vyovyote vile anavyotaka.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nahisi wenzetu wasiingie zaidi katika tamaduni za Magharibi, watizame na sisi tabia zetu, silka zetu na utamaduni wetu tuliokuwa nao na tulinganishe na hali yetu tulionayo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda umebakia mdogo sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, kwa kuwa muda umemalizika na mimi tayari nimeshachangia hapa. Kwa hivyo, mimi naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri. Kama nilivyotangulia kusema kwamba sheria hii Mhe. Waziri aisimamie vizuri na kwa sababu vyombo anavyoshirikiana navyo katika kutekeleza sheria hizi, kama vile Polisi na Mahakama, kwa kweli tunawahisi hawajawa tayari na kwa sababu kunakuwa na mambo ambayo utayakuta yana ushahidi wa moja kwa moja, lakini inakuwa utekelezaji wake au hukumu zake zinakuwa sio barabara. Kwa hivyo, ni lazima wizara iwe makini katika kulisimamia hili, na kwa sababu ni jambo ambalo linatudhalilisha, sio watoto tu. Sisi tunazungumzia suala la kuwadhalilisha watoto, lakini hata watu wazima tunadhalilika na suala kama hili.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja ili sheria hii ipite na iwe sheria kamili na iweze kuchukua hatua, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Salmini Awadh Salmin, kwa mchango wako huo. Kuna matangazo mawili. Moja tunategemea Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atarudi kutoka safari ya Iran kwenye saa 11:00 jioni leo. Government Chief Whip ataweka utaratibu kwa wale ambao wachache watakwenda pale kwa ajili ya kumlaki, wengi tubaki kuendelea na shughuli zetu hizi.

Pili, leo ndugu zetu wa AZAKI tutawafungia maonyesho waliyokuja kutuonesha hapa nje. Kabla ya hapo ilikuwa imepangwa iwe mara baada ya kikao hiki, lakini kuna mabadiliko kidogo kwamba shughuli hiyo itafungwa mnamo saa 9:00 kamili leo. Hili jambo la maonyesho ni letu, tumeletewa sisi Waheshimiwa Wajumbe, kwa hivyo tunaombwa tuhudhurie ingawa wakati umekaa vibaya kidogo. Lakini tuhudhurie wakati wa ufungaji wa maonyesho hayo leo saa 9:00 jioni hii.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo machache, jioni tutaendelea na uchangiaji kidogo na baadae kumuomba Mhe. Waziri aje afanye majumuisho. Wapo Waheshimiwa Mawaziri wawili au watatu ambao wanataka kumsaidia Mhe. Waziri katika kutoa michango yao, basi wafanya hivyo wakati wa jioni.

Baada ya hayo machache Waheshimiwa Wajumbe, naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(saa 7:00 Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni leo)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea, kuna wachangiaji wachache ambao wamebaki, tuepuke kurudia rudia na kwa wachangiaji hao tupate na muda wa kutosha ili tumpe nafasi Mhe. Waziri afanye majumuisho. Kwa hivyo, tutumie dakika kumi kumi na wachangiaji niliokuwa nao wananitosha sana, hasa kutokana na kazi kubwa ambayo tayari Waheshimiwa Wajumbe wameifanya ya kutoa michango mizito kwa mswada huu. Tunaendelea.

Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Haji Faki Shaali hayupo, Mhe. Said Ali Mbarouk Waziri wa Mifugo na Uvuvi hayupo, Mhe. Abdillah Jihadi Hassan Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo hayupo, Mhe. Hamza Hassan Juma hayupo, Mhe. Hassan Hamad Omar hayupo. Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake na Watoto karibu.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa mara yangu ya kwanza nashukuru sana kupata nafasi hii ya kutoa ufafanuzi wa mswada tuliouleta hapa wa sheria ya mtoto. Naomba Mhe. Spika, kama itatokea kasoro basi utanisamehe sana.

Mhe. Spika, naomba kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu waliochangia na wasiochangia huu Mswada wa Sheria ya Mtoto. Naomba kutoa shukrani kwa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa michango yao, pamoja na kazi kubwa walioifanya ya kupitia vifungu vyote vya sheria hii, pamoja na marekebisho waliyoyafanya kwa ujumla ambayo yameifanya sheria yetu iwe nzuri zaidi.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri mswada wetu wa sheria umechangiwa na wajumbe 26 na wawili wamechangi kwa maandishi. Naomba niwataje hao wajumbe:

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mwenyekiti wa Kamati
2. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
3. Mhe. Subeit Khamis Faki
4. Mhe. Mussa Ali Hassan
5. Mhe. Hija Hassan Hija
6. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
7. Mhe. Abdalla Moh'd Ali
8. Mhe. Dk. Sira Ubwa Mamboya
9. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
10. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
11. Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum)
12. Mhe. Ismail Jussa Ladhu

13. Mhe. Waziri wa Afya
14. Mhe. Assa Othman Hamad
15. Mhe. Ussi Jecha Simai
16. Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi
17. Mhe. Mohammed Haji Khalid
18. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
19. Mhe. Raya Suleiman Hamad
20. Mhe. Fatma Ali Said
21. Mhe. Mgeni Hassan Juma (Mwenyekiti wa Baraza)
22. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
23. Mhe. Abdi Mosi Kombo
24. Mhe. Panya Ali Abdalla
25. Mhe. Salmin Awadh Salmin

Mhe. Spika, na waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Salma Mohammed Ali na
2. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman

Mhe. Spika, naomba kutoa shukrani na pongezi za dhati kwa Mhe. Mansour Yussuf Himid, Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Dk. Sira Ubwa Mamboya kwa ufafanuzi mzuri ambao umesaidia kufahamisha baadhi ya vifungu vya mswada huu.

Mhe. Spika, kwa heshima na taathima sasa naomba kutoa ufafanuzi wa baadhi ya maswali ya wajumbe yaliyojitokeza katika mjadala huu kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwanza naomba nianze na umri wa mtoto.

Mhe. Spika, Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Ismail Jusa Ladhu na Mhe. Abdalla walipendekeza umri wa mtoto uwe chini ya baleghe, yaani akifika mtoto miaka tisa iwe tayari yeye sio mtoto tena awe keshaanza kuwa mtu mzima.

Mhe. Spika, suala hili litakwenda kinyume na katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, ambayo ndio sheria mama ya nchi, inatambua kwamba mtoto ni mtu yeyote ambaye ana umri chini ya miaka 18. Ndio maana hata haki ya kupiga kura imetambua kuwa mtu yeyote chini ya miaka 18 basi hatoruhusika kupiga kura kwa kuwa anahesabika kuwa ni mtoto, hata kwenye sheria ya vitambulisho inatambua kuwa utu uzima unaanzia miaka 18.

Aidha, tafsiri ya mtoto imezingatia umri wa ukubwa, yaani *age of majority*, ambapo kiwango cha juu cha ukomavu wa mtoto ni miaka 18. Sheria ya umri

na ukubwa wa sura ya 53 *age of majority decree paper 53,* inatambua umri wa mtoto ni chini ya miaka 18 katika kifungu cha 4.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, naomba tufahamu kwamba suala la baleghe halitegemei umri, kwani kila mtoto anabaleghe katika umri wake kiafya, kiakili na hata kiutulivu. Mtoto mwenye umri mdogo anapoolewa hukabiliwa na matatizo mengi katika maisha ya ndoa, ikiwemo hasa wakati wa kujifungua basi watoto wanapata shida. Huachwa huku wakiwa wanawatoto wachanga.

Mhe. Spika, pamoja na hayo Waislamu tumefaradhishiwa kutafuta elimu kwa wanawake na wanaume. Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe tulipe uzito zaidi suala la kuwapa elimu watotowa kike ili watowe mchango katika taifa, kuliko kuwaozesha waume mapema, wakazaa na kuachwa, wakatelekezwa na watoto na baadae kuwa na kundi kuba la vijana lisilokuwa na mwelekeo katika taifa letu, hayo ni matatizo.

Vile vile Mhe. Spika, sheria ya tafsiri nambari 7 ya mwaka 1984 ya Zanzibar imetoa tafsiri ya mtoto ni mtu chini ya miaka 18.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameeleza kwamba sheria imelenga zaidi utekelezaji wa mikataba ya kimataifa. Naomba kulijulisha Baraza lako tukufu kwamba chimbuko la sheria hii ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, ambazo zote zinatambua kwamba binadamu wote ni sawa, pamoja na kuzingatia mikataba ya kimataifa ambayo yote inatambua haki za binadamu pamoja na hifadhi ya mtoto.

Naomba kuwathibitishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba hakuna shindikizo la Shirika la Kimataifa wala mikataba ya kimataifa katika kuundwaji wa sheria hii.

Dhamira kubwa ya uundwaji wa sheria hii ni kuweka mazingira mazuri na bora ya kumlinda mtoto wa Zanzibar. Ndio maana katika uundwaji wa sheria hii wadau wengi walishirikishwa kutoa michango yao ili kuwa na sheria inayofuata mila na silka za Kizanzibar.

Mhe. Spika, mikataba yote ya kimataifa inayozungumzia mtoto, zaidi imelenga kupatiwa malezi mazuri, ikiwemo elimu, michezo, afya bora na kinga dhidi ya uzalilishwaji ambayo ni misingi mikuu ya hifadhi ya mtoto.

Mhe. Spika, suala la kuasili lilipata nafasi kubwa katika kikao hiki Mhe. Spika. Suala la kuasili ni kwa jamii ya Wazanzibar wasiokuwa Waislamu, na Zanzibar

wapo watu waliokuwa sio Waislamu ambao hao ndio wameekewa utaratibu huu. Aidha Wizara imechukua mapendekezo ya wajumbe kwamba kafala itafanywa na Mzanzibari Muislamu tu na maombi hayo yatapelekwa katika mahakama ya kadhi.

Kuhusu wazee watakaoona kwenye dini tofauti, mtoto atakwenda wapi. Mhe. Spika, itazingatia mzazi mwenye maslahi bora kwa mtoto. Lakini suala hili Mhe. Spika, la kufuata dini atakayo mtoto, basi litaamuliwa na mwenyewe mtoto hasa akifikia umri wa miaka 16 ambapo sheria hii mtoto imempa uwezo wa kufanya maamuzi yanayomuhusu.

Kwa mfano, katika maamuzi ya kufanyiwa upasuaji. Mtoto hawezi kufanyiwa upasuaji hadi akubali yeye mwenyewe, katika masuala ya kupimwa ukimwi ni hadi akubali yeye mwenyewe na suala la kufuata dini ipi aipendayo ni lake yeye mtoto mwenyewe. Naona nimejieleza Mhe. Spika.

Mhe. Spika, tumepokea pongezi za Waheshimiwa Wajumbe kwa wizara yangu, waziri pamoja na watendaji wake na hasa kwa kuanzisha kituo rafiki, yaani *onestop center* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, ambayo nia yake kuu ni kutoa huduma zote kwa watoto watakao kumbwa na kadhia ya kudhalilishwa kijinsia. Tunaahidi Mhe. Spika, kwamba tutakiendeleza kituo hicho, ili kutoa huduma nzuri zaidi. Vile vile tutakiharakisha kile kituo cha Pemba katika Hospitali ya Chake Chake pamoja na kuangalia hatua ya kuanzisha vituo vyengine katika hospitali kubwa za Mikoa na Wilaya.

Mhe. Spika, wajumbe wako waliitaka wizara yangu kujenga vituo vya marekebisho ya tabia za watoto. Mhe. Spika, sasa hivi tutaanzisha vitu vya marekebisho. Huko nyuma tulikuwa na vituo vya manunda, hivi sasa tunataka kuanzisha vituo vya marekebisho ya mtoto. Mhe. Spika, wizara inalichukua suala hili na litafanyiwa kazi na wizara nzima ya ustawi wa jamii, ili tuhakikishe vituo hivyo vinapatikana.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wengi walihimiza kuhusu utekelezaji wa sheria hii, ili iweze kutumika ipasavyo. Wizara yangu imejipanga kufanya yafuatayo. Kutoa taaluma kwa wahusika wote wa utekelezaji wa sheria hii wakiwemo Polisi, Mahakama, Mwendesha Mashtaka, Madaktari, Mahakimu na Maafisa wa Ustawi wa Jamii.

Pia kuitafsiri katika lugha nyepesi na kutoa vipeperushi kwa lengo la kufahamika zaidi, pamoja na kuandaa kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hii. Sheria hii Mhe. Spika, tutaiendea mbio, ili iweze kufanya kazi bara bara.

Mhe. Spika, naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Baraza hili pamoja na jamii yote, tutowe mashirikiano katika utekelezaji wa sheria hii, kwa sababu kadiri tutakavyofanyakazi, kama hatukushirikiana basi jambo hili halitoweza kufanikiwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa ufafanuzi kwamba sheria hii ya mtoto haikuzingatia tu haki za mtoto, bali na wajibu pia katika kifungu cha 17 cha mswada huu, upo na umeelezwa kikamilifu naomba tuuangalie vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu mswada huu kuondoa suala la mabaa katika makaazi ya wananchi. Mhe. Spika, naomba kulieleza Baraza hili kwamba hata sisi Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto tuna hakika kwamba baa hizi zinachangia balaa. Kwa hivyo, na sisi tunaungana na wajumbe wako wote ili kuona kwamba baa hasa zisiendelee kujengwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nakuhakikishia kwamba suala hili litashughulikiwa hata katika hivi vikundi vya video, kwa sababu navyo vinachangia kuharibu watoto. Mhe. Spika, wanaonesha mambo ambayo hayastahiki kuoneshwa kwa watoto na watoto huwa wanapendelea kwenda kuyaona. Kwa hivyo, yeyote atakayeonesha video hizo basi atachukuliwa hatua zinazofaa.

Mhe. Spika, naomba kwa niaba ya *ZAYADESA*, kupokea pongezi zilizotolewa na wajumbe na ninaahidi tutazifikisha kwa Mwenyekiti, Mhe. Mama Shadya Karume, kwa kuwapatia watoto yatima matunzo ya nyumba bora.

Mhe. Spika, wakati nilipokuwa najibu swali la kuhusu makaazi ya watoto, basi wengine walihusu kwamba baa! Mhe. Bi Zaynabu anajibu kisiasa tu. Lakini Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ni shahidi tosha, kwamba watoto sasa hivi wamepata nyumba nzuri, wanakaa na wana matunzo mazuri. Watoto wanawake wako katika sehemu zao na watoto wanaume wako katika sehemu zao, humo humo katika nyumba hiyo kuna chuo na kuna mambo ya mafundisho mengine ya kawaida. Kwa hivyo, pale ulezi umetimia hakuna tatizo lolote. Kwa hivyo, tumpongezeni sote Mama Shadya Karume kwa kazi nzuri aliyoifanya.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kwa walezi na wazazi, tuna walezi wanaowataka watoto wao wenyewe, wakishawafikisha majumbani wanaanza kuwafanyia mateso watoto. Kwa hivyo, tunalaani vitendo hivyo vya watoto kufanyiwa mateso na wakati mtu amemtaka mwenyewe mtoto yule.

Vile vile wazazi wajitahidi kulea watoto wao wenyewe. Kwa kweli mtoto kumchukua na kumpa mtu mwengine ni huo unyonge tu hatuna la kufanya,

lakini inavyotakiwa mtoto akae na baba na mama. Suala la kuachana tumeshasema kwamba sio suala zuri, tusiachane. Labda tena iwe hapana budi, lakini hasa mkishaungana na mkiwa na watoto wenu basi ni mapenzi juu ya mapenzi kuna tatizo gani tena.

Mhe. Spika, tujitahidi kulea watoto wetu katika maadili mazuri. Mhe. Spika, naomba niseme tena. Tujitahidi kulea watoto wetu katika maadili mazuri, kwa sababu katika michango iliyotolewa hapa, inaonekana kwamba kuna baadhi ya wazazi wenyewe wanachangia kuwapotoa watoto.

Mhe. Spika, umetolewa mfano hapa kwamba mtoto anaanza kuvaa gauni la Shs.100,000/=, mama mtu anamuona na baba mtu anamuona mwanawe, nguo iliyokuwa haina mikono, haina hifadhi yoyote anatoka na kujitia vininja, lakini akifika huko barabarani anavivua vininja na kukaa hivi hivi kutafuta soko. Kwa hivyo, tufuatilie kwa makini nyendo za watoto wetu.

Mhe. Spika, wasimamizi wa nyendo za watoto wetu ni sisi wenyewe, kujenga taifa lililoimara kwani ulezi ni jukumu la kila mzazi. Tumesema kwamba siku hizi hatusaidiani kulea na utamaduni wetu ulikuwa tunasaidiana kulea, mtoto wa huyu anamlea huyu na mtoto wa huyu anamlea huyu. Lakini sasa hivi ukimgusa mtoto wa mwenzio basi mzazi anaweza kwenda kukushtaki. Nadhani baada ya kupita mswada huu wa sheria ya mtoto, wazazi, walezi na wengineo basi tutakuwa shauri moja ili kumtetea huyu mtoto.

Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Mohammed Ali na Mhe. Salmin Awadh Salmin wameonesha wasi wasi wao kwamba sheria hii imejikita zaidi katika haki za watoto, lakini wajibu umesahauliwa. Nimeshasema kwamba wajibu umo, tuuangalie vizuri huu mswada wetu. Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kulithibitishia Baraza lako tukufu kwamba sheria hii inajikita zaidi kwenye mila, silka, desturi na utamaduni wa Mzanzibari. Ndio maana uundwaji wa sheria hii umeanza tangu mwisho wa mwaka wa 2008 na wadau mbali mbali wa Zanzibar wamepata fursa ya kuupitia mswada huu na kutoa marekebisho ya vifungu mbali mbali. Haya yote yamefanywa na mshauri mwelekezi ambaye kwa hivi sasa ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kushirikiana na wanasheria wa wizara yangu.

Mhe. Spika, Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Subeit Khamis Faki wamependekeza kuwepo tafsiri ya baadhi ya maneno. Naomba kuwahakikishia kwamba ushauri wao tunauchukua na tutaufanyia kazi kikamilifu.

Mhe. Spika, naomba kuwahakikishia wajumbe kwamba mapendekezo yote ya kufanya sheria hii iwe na utekelezaji mzuri, basi tutayachukua na kuyafanyia

kazi, ili tuhakikishe watoto wetu wanapata malezi mazuri, wanapata makaazi mazuri, chakula

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mnaotoka nje, sio muda mrefu kuanzia sasa tutapitisha hoja hii, kwa hivyo mkumbuke kurudi haraka. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake na Watoto: Kuangaliwa haki zao na pia kujua wajibu wao kwa wazazi na taifa lao.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Ussi Jecha Simai nakushukuru, kwa kutekeleza na kutii amri niliyoitoa sasa hivi umerudi. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale waliokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2011

(Kusomwa kwa Mara ya Pili*)*

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza zima, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2011

Sehemu ya Kwanza
Utangulizi

Kifungu cha 01 Jina fupi na kuanza kutumika.
Kifungu cha 02 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Pili
Maslahi Bora na Haki za Mtoto

Kifungu cha 03	Maslahi bora ya mtoto.
Kifungu cha 04	Uamuzi wa maslahi bora ya mtoto pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 05	Ushiriki wa mtoto na maoni yaliyotolewa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 06	Kutobaguliwa.
Kifungu cha 07	Haki ya kuwa na jina na utaifa.
Kifungu cha 08	Haki ya kuandikishwa kuzaliwa.
Kifungu cha 09	Haki ya kuishi pamoja na wazazi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 10	Haki ya kupatiwa baadhi ya mahitaji ya maisha.
Kifungu cha 11	Watoto wenye ulemavu.
Kifungu cha 12	Dhamana na majukumu ya mzazi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 13	Haki katika mali ya mzazi.
Kifungu cha 14	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nithibitishiwe tu kwamba katika michango yetu tulipendekeza maneno ya kuingizwa tafsiri ilikuwa ni neno la kuwarudi watoto lililotumika katika kifungu hiki. Kwa hivyo, nataka nithibitishwe tu kuwa nayo yataingizwa katika tafsiri, ili tuweze kujua inapokusudiwa mzazi kumrudi mtoto inakusudiwa nini katika sheria hii. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Mjumbe arudie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba urudie kwa taratibu, ili Mhe. Waziri apate kufahamu vizuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwenye michango yetu tulizungumzia haja ya kuwa na tafsiri ya baadhi ya maneno ambayo yametumika katika sheria hii hasa yanayohusu haki na wajibu kama huu. Sasa kwenye majumuisho yake Mhe. Waziri alituambia kijumla kwamba mapendekezo yetu yamepokelewa.

Kwa hivyo, nataka uhakika kwenye hayo mapendekezo katika kifungu hiki cha 14 (2) kumetumika maneno juu ya wazazi kuwarudi watoto. Kwa maana hiyo, nataka kuthibitishiwa kwamba hili la kuwarudi watoto, kwa sababu pia tulilichangia kuwa litafsiriwe kwamba litakuwemo katika jumla ya maneno

ambayo yanataka kutolewa ufafanuzi kwenye kile kifungu cha awali pale. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, inawezekana wakati nilipokuwa kutoa ufafanuzi au majumuisho Mhe. Mjumbe alikuwa hajafika. Lakini nimeeleza vizuri kuhusu haki na wajibu na nilisema kwamba tuangalie kifungu cha 17 ambacho kinaeleza vizuri. Sasa sijui ndivyo nilivyomueleza au hakukusudia hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, anachohitaji Mhe. Mjumbe ni kuna maneno yalipendekezwa yapewe tafsiri na mengine aliyasema yeye, pia nakumbuka hata Mhe. Salmin Awadh Salmin alisema na Mhe. Mjumbe alisema kwamba wewe ulisema kwa ujumla. Je, katika ujumla ulivyotoa majibu kuwa yatazingatiwa na kutolewa tafsiri ni pamoja na hili ambalo amelizungumza yeye.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani neno hili la kumrudi mtoto linahitaji tafsiri. Kwa hivyo, tutaliingia katika tafsiri ya mswada huu. *(Makofi)*

Kifungu cha 14 Kinga kutokana na kuteswa na adhabu za kudhalilisha
Kifungu cha 15

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia mswada huu niliunga kimsingi jinsi mtoto tutakavyomtetea katika udhalilishaji wa kingono. Lakini kadri ninavyousoma mswada huu pamoja na Waheshimiwa Wajumbe walivyochangia walikuwa wakimuangalia mwanamme tu ndio mwenye kudhalilisha.

Kwa hivyo, nilipendekeza kwamba wapo wanawake ambao wanafanya vitendo vibaya karibu ya hiyo ngono. Sasa sheria ingesema kwamba adhabu hizi na wala sina haja ya kuzitaja kwa sababu Mhe. Waziri anazifahamu nakusudia nini, kwamba wanawake nao

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, makofi hayo kwa ajili ya kumkaribisha Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na karibu sana. Kwa hivyo, Mhe. Hija Hassan Hija endelea.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ninachokusudia kusema ni kwamba sheria hii ni vyema ikataja wazi wazi pamoja na hivi vitendo ambavyo baadhi ya wanawake huvifanya kwa ajili ya kuwafanyia watoto wetu.

Kwa kweli wasiwasi wangu ni kwamba tunaweza kuwadhibiti wanaume kuwa wasifanye vitendo vya ngono na watoto wetu, lakini watoto wetu hushawishiwa na wanawake wengine wakatili wakawafanyia vitendo ambavyo vinalingana na hivi. Kwa hivyo, sheria ingesema pamoja na adhabu zile, basi na makosa yale pia yashughulikie adhabu hizi.

Mhe. Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kuwa wanaume tukiwadhibiti wataacha kufanya matendo ya kuwashawishi watoto wetu, lakini wanawake watawachukua na kuwafanya matendo ambayo si mazuri. Kwa maana hiyo, lazima sheria iseme kwamba adhabu hizo zipo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi mara nyingi huwa nasikia kwamba watoto wetu wanawake wanabakwa na wanaumizwa. Lakini sijapata kusikia hawa wanawake wanaofanya vitendo hivi, yaani sijasikia kabisa labda wanafanya kwa siri kubwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, inawezekana Mhe. Waziri hajasikia au hawajaona. Lakini matokeo haya yanaonekana na jina lake sijui linaitwa vipi, isipokuwa naamini kwamba Waheshimiwa Wajumbe wengi wanajua matokeo haya yapo Unguja na Pemba na zipo nyumba maalum ambazo watu wanafanya biashara hii ya kuwachakachua watoto wa kike. Kwa hivyo, nadhani sheria iseme kwamba wasiangaliwe wanaume tu, lakini na wanawake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unaturuhusu tuendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sijaruhusu mpaka nione kwamba sheria inaangalia pande zote mbili, kwa sababu wasiwasi wangu ni kwamba wanaume watapata adhabu zaidi, lakini wanawake wataongeza matatizo na unapomfanya mtoto wa kike mambo kama hayo unamuathiri *psychological* ambapo mswada unakataza. Kwa hivyo, tusiendelee mpaka nipate ufafanuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani hicho kifungu kinajieleza, kwa sababu kimesema ni mtu yeyote awe mwanamke au mwanamme. Kwa hivyo, nafikiri imejumuisha watu wote, yaani ikiwa mwanamke au mwanamme na sheria tayari imeshamzungumza na wala hakuna haja ya kusema kwamba hii ya mwanamke na ile ya mwanamme naona sheria iko wazi. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilichokuwa nikikitafuta mimi ni kwamba *Hansard* itambue kwamba wanawake nao wanaathiri. Kwa hivyo, tuendelee.

Kifungu cha 15 Udhalilishaji wa mtoto pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 16 Adhabu kwa kwenda kinyume.
Kifungu cha 17

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia mswada huu nilikigusia kifungu hiki nikitambua maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri katika majumuisho yake kwamba ndicho kinachozingatia kuwa kinataja wajibu wa mtoto.

Lakini *concern* yangu jana na ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kuwa aturidhie ni vile jinsi kilivyoandikwa na wala sina pingamizi yale yaliomo kwamba ni wajibu, lakini vile kilivyoanza. Mhe. Mwenyekiti, naomba nikinukuu kifungu hicho.

Kifungu cha 17 kuhusu majukumu ya jumla ya mtoto kinasema hivi:-

> "Katika matumizi ya sheria hii na katika mwenendo wowote, vitendo na maamuzi ya chombo chochote cha umma kuhusu mtoto vitaangalia dhamana na majukumu ya mtoto ya …"

Sasa *concern* yangu Mhe. Mwenyekiti ni kwamba huku juu katika haki tumetaja haki kama ilivyo kwenye Katiba yetu tunavyotaja Haki ya Raia au Haki ya Binadamu, yaani haki inatawa tu. Kwa hivyo, hapa sheria ime-*qualify* kwamba haya yatazingatiwa tu, katika maamuzi ya chombo chochote cha umma kuhusu mtoto.

Kwa maana hiyo, hofu yangu ni kwamba hii tunafanya *only* ni *issue Judiciary matter*, kwamba labda panapotokezea kesi au mtoto amelalamika, kwa hiyo mzazi naye akitoa malalamiko yazingatiwe. Lakini haisemi kwa uwazi moja kwa moja kwamba huu ni wajibu wa mtoto kama vile vifungu vinavyozungumzia haki vinavyoeleza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwamba bila ya kuandika maneno haya tuseme tu hapa kwenye hiki kifungu. Nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu anaweza kutusaidia vizuri, kama ilivyo katika haki wajibu wa mtoto kwa wazazi na jamii utakuwa kama ifuatavyo kama vile 1, 2, yaani inakuwa inatumika katika mazingira yote ikiwa kesi au chombo cha kufanyia maamuzi na hata kwa jumla wajibu wa mtoto kwa wazazi na jamii.

Kwa kweli kama ilivyo katika zile haki zake ambazo wazazi pamoja na jamii wanapaswa wamuhakikishie, ili tuipate ule usawa wake. Hiyo ndio *concern* yangu na ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba atukubalie.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye na wala sina matatizo yoyote. *(Makofi)*

Kifungu cha 17 Majukumu ya jumla ya mtoto pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, marekebisho ya hapa ni kuweka uwazi majukumu ya mtoto.

Sehemu ya Tatu
Mahakama ya Watoto

Kifungu cha 18 Kuanzishwa Mamlaka, uwezo wa Mahakama ya Watoto na Rufaa pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Nne
Matunzo na Kinga ya Mtoto

Kifungu cha 19 Maana ya matunzo ya mtoto na kinga na sababu za amri ya matunzo.
Kifungu cha 20 Jukumu la kuripoti uvunjwaji wa haki za mtoto.
Kifungu cha 21 Hatua za kuchukuliwa na Afisa Ustawi.
Kifungu cha 22 Amri ya kinga ya dharura pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 23 Amri ya usimamizi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 24 Amri ya matunzo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 25 Amri ya kuzuia.
Kifungu cha 26 Amri ya ziada pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 27 Ripoti ya uchunguzi wa kijamii pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 28 Majukumu ya Afisa Ustawi.
Kifungu cha 29 Kutembelea majumbani.
Kifungu cha 30 Kuondoa amri.
Kifungu cha 31 Uwezo wa mahakama kutoa amri ya kuchangia.
Kifungu cha 32 Dhamana ya uzazi kwa meneja wa nyumba iliyoanzishwa au wazazi walezi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 33 Hapana ruhusa ya kuchapisha taarifa au picha ya mtoto.
Kifungu cha 34 Kanuni za matunzo na kinga za watoto.

Sehemu ya Tano
Watoto Walio na Matatizo na Sheria

Kifungu cha 35 Umri wa dhima ya jinai.
Kifungu cha 36 Kuangalia umri.
Kifungu cha 37 Kukamata.
Kifungu cha 38 Kuwajuilisha watu juu ya kukamatwa mtoto.
Kifungu cha 39 Mwachano kwa polisi kumuonya na dhamana ya watoto waliokamatwa na polisi.
Kifungu cha 40 Dhamana ya watoto ambao hawakupewa dhamana baada ya kukamatwa.

Kifungu cha 41 Tathmini ya watoto waliofanya makosa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 42 Mwachano wa mambo yanayohusu makosa madogo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 43 Taratibu za Mahakama ya Watoto.
Kifungu cha 44 Kubagua au kuweka pamoja mwenendo na kuwapeleka watoto katika mahakama.
Kifungu cha 45 Dhamana ya watoto mahakamani pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 46 Mtuhumiwa kutakiwa atoe sababu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 47 Mbinu za kushughulikiwa watoto walioshakiwa kwa makosa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 48 Kukataza uchapaji wa taarifa.
Kifungu cha 49 Mashahidi watoto.
Kifungu cha 50 Masharti ikiwa mtoto ameshindwa kufuata maelekezo au masharti ya amri.
Kifungu cha 51 Mahakama ya Watoto kumaliza kesi bila ya kuchelewa.
Kifungu cha 52 Kufuta kumbukumbu za jinai.
Kifungu cha 53 Kuwajumuisha watoto katika kosa la jinai kuchukuliwa ni mazingira yanayoongeza kosa.
Kifungu cha 54 Kanuni.

Sehemu ya Sita
Uzazi, Ukaazi, Ulezi, Kumuona na Matunzo

Kifungu cha 55 Ombi la kuwa mzazi.
Kifungu cha 56 Uthibitisho wa uzazi.
Kifungu cha 57 Kipimo cha kidaktari.
Kifungu cha 58 Ukaazi pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 59 Ulezi.
Kifungu cha 60 Fursa ya kumuona pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 61 Uzingatiaji wa utunzaji, ulezi na fursa ya kumuona pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 62 Kumuondoa mtoto kinyume na sheria pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 63 Jukumu la kumtunza mtoto.
Kifungu cha 64 Ombi la amri ya matunzo.

Kifungu cha 65 Amri ya matunzo dhidi anayeshukiwa kuwa baba wa baiolojia.
Kifungu cha 66 Mazingatio katika amri za matunzo.
Kifungu cha 67 Ombi la ripoti ya uchunguzi wa kijamii.
Kifungu cha 68 Kumaliza muda wa amri ya matunzo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 69 Kushindwa kufuata amri ya matunzo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 70 Haki za mtoto ikiwa wazazi wametengana.
Kifungu cha 71 Makosa chini ya sehemu hii.

Sehemu ya Saba
Matunzo Kutoka kwa Wazazi Walezi

Kifungu cha 72 Watu wanaoweza kulea.
Kifungu cha 73 Masharti ya matunzo kwa wazazi walezi.
Kifungu cha 74 Kanuni za matunzo kwa wazazi walezi pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Nane
Kafalah na Kuasili

Kifungu cha 75 Kafalah pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 76

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia mswada huu nilionesha wasiwasi wangu kuhusu kifungu hiki cha kuasili na nilieleza vizuri hapa. Kwa kweli, kuasili kwa mujibu wa tafsiri ya kuasili ni kumchukua mtoto kutoka kwenye familia moja, yaani ukamhamisha pawa na miko kwenda kwenye familia ya pili, ambako huku anakohama anaacha haki zake zote na kule anakokwenda anapewa haki ambazo si zake kwa mujibu wa mila zetu za Kiislamu.

Kwa hivyo, nilisema mimi kama Muislamu *committed* kifungu hiki sikikubali, kwa sababu nitakaporidhia kipitishwe, basi madhambi yatakayochumwa kule na mimi nimo. Kutokana na hali hiyo, nilisema kwamba sikubaliani na kifungu hiki na niliomba kifutwe, ambapo kifungu hiki cha kuasili kimeanzia kifungu cha 76 mpaka 82. Kwa maana hiyo, bado naendelea kushikilia msimamo wangu kwamba vifungu hivyo vyote vifutwe.

Mhe. Mwenyekiti, tukizingatia madhumuni ya mswada ni kulinga haki za mtoto na kifungu cha Kafalah kinabeba dhima ya mtu kuweza kumsaidia ulezi mwenzake. Kwa hivyo, kifungu hiki kikitolewa hakiathiri *concept* iliopo. Mhe. Mwenyekiti, naomba vifungu hivyo vyote vifutwe.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 76 naomba tukisome vizuri, naomba kukinukuu.

Kifungu cha 76 (1) kinasema hivi:-

> "Masharti ya sehemu hii hayatawahusu watu wanaofuata Dini ya Kiislamu".

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji ambaye ametoa hoja hivi sasa alisema kwa mujibu wa mila zetu na kwa sababu yeye ni Muislamu, ina maana ni kwa mujibu wa mila zetu za Kiislamu na mimi nakubaliana naye. Lakini hapa vifungu hivi vinavyofuata sisi Waislamu havituhusu, isipokuwa hivi vinahusu wale watu ambao wanafuata dini ambayo si Uislamu.

Kwa mfano, Dini ya Kikiristo inaruhusu *adoption*. Kwa hivyo, hii ni sawa na inakwenda kwa mujibu wa utaratibu wa *adoption* kwa Dini ya Kikiristo na wala sisi hatuingilii Dini ya Kikiristo hapa. Kwa upande wa Dini ya Kiislamu inazungumzia masuala ya Kafalah ambayo hiyo ndio sehemu hasa ambayo sisi mila zetu zinazingatiwa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, mawazo ya Mhe. Waziri ni mazuri na mimi nayaheshimiwa sana. Lakini kwa mujibu wa maelezo tuliopewa sisi Mtume Muhammad (S.A.W) anatwambia "kama mtu ataajiriwa katika duka la kuuza ulevi hata ikiwa yeye halewi, lakini kile kitendo cha kukubali kutoa huduma za ulevi na yeye anaandikiwa sawa kama yule mwenye kunywa ulevi".

Kwa hivyo, mimi ni Muislamu lakini natunga sheria kwa watu wengine tena najua athari ipo kwa mujibu wa mila zetu, sasa hata kama mimi simo mule basi madhambi nitapata Mhe. Mwenyekiti na kwa *concept* hii ndio nikasema sikubali.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana naye Mhe. Mjumbe kwa suala la kidini. Lakini hapa hatupo katika utaratibu huo tupo katika suala la kutunga sheria inayohusu jamii yote ya Zanzibar.

Sasa kwa sababu inahusu jamii yote ya Zanzibar kama ni serikali, basi lazima tutizame maslahi ya jamii yote wale ambao wako katika misingi ya Kiislamu na wale walioko katika misingi ya Kikiristo na wale walioko katika misingi ya dini nyengine. Kwa hivyo, kama ni serikali hatuwezi kusema tutunge sheria inayohusu Waislamu tu, hivyo itakuwa tunakwenda kinyume na Katiba ya Nchi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Mjumbe alikula yamini hapa mbele yako kusema kwamba atatetea Katiba ya Zanzibar pamoja na kuilinda. Kwa hivyo, kufanya hivi ndio tunalinda hiyo Katiba yetu ya Zanzibar ambapo sote tulikula kiapo kwamba tutaitetea na kuilinda, kwa maana hiyo tunailinda jamii yote, yaani iwe ni Muislamu au Mkiristo ama Mpagani au mtu mwengine yeyote, lakini ni lazima kuwalinda. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unasema je sasa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, kama pangekuwa na Mufti hapa kwa sababu sikubali, basi nyinyi mkipitisha dhambi mimi nitakuwa simo ningekuwa sina tatizo. Lakini nadhani Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria maneno yake ni mazito kwamba nilikula kiapo na kama si hicho Mhe. Mwenyekiti ningekuomba sana uvifute au uniruhusu nitoke nje wakati wa kupitisha sheria hii kwa sababu ya hilo, lakini naheshimu hicho kiapo. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi zaidi, kwa sababu sisi jamii ya Waislamu wakati mwengine tunakuwa tunachanganyika. Kwa mfano, mimi ni Muislamu naweza kupata mwanamke wa Kikiristo na kuniambia mimi nitasilimu, basi nikakubali na nikamsilimisha kwa muda fulani kikamuoa na baadaye tukapata watoto, lakini baada ya kukosana kidogo mbili tu pengine nikamuacha anarudi tena kwenye dini yake ya ukiristo, au pengine mwanamume inakuja kinyume chake hivyo hivyo anapata mwanamke wa kiislam akakubali, mimi nitakufuata dini yako nitasilimu akakubali kusilimu siku mbili akamuoa mwanamke wakazaa watoto wawili, siku mbili tatu tayari wameshatengana. Sasa mtoto wakati mwengine anakwenda huku na wakati mwengine anakwenda huku.

Sasa je, ikiwa mtoto ana pande mbili yuko kwenye ukiristo au yuko kwenye uislam hapa tunataka ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema mjumbe kwamba kama yeye amempenda mwanamke ambae ni wa kikristo na akamsilimisha wakaowana kwa hivyo wanapoowana wanaowana kwa dini ya kiislam. Kwa hivyo kizazi chao chote kitakachopatikana wakati ule itakuwa ni kizazi cha kiislam, kwa sababu ni kizazi cha kiislam itakayo-*apply* sio kifungu cha 76 itakayo-*apply* ni tafala kwa sababu wote ni waislam.

Sasa kwa bahati ikiwa yule mtoto awe mwanamke au mwanamme kwa vyovyote itakavyokuwa ametoka akaingia katika dini yake ya zamani hilo ni suala jengine, lakini hapa lazima Mahakama iamuwe kwasababu kuna *welfare fee* ya mtoto, mtoto anapokuwa na umri wa mwaka mmoja mpaka miaka fulani Mahakama inaamua kwamba mtoto yule aweko kwa mama au aweko kwa baba sasa inategemea Mahakama itaamua vipi, na pia inategemea yule mtoto hapo alipo ana dini gani kakubaliana na baba mtu na mama mtu ikiwa dini ni ya Kiislam haito-*apply* hii, ikiwa baba mtu kakubali mtoto wake aingie dini ya kikristo kwa hivyo hii ita- *apply* sasa inategemea mazingira ya ile kesi yenyewe hatuwezi kuamua hapa na kesi hiyo itaamuliwa na Mahakama kutokana na utaratibu wetu wa kesi katika Mahakama.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, unajua tunaloling'ang'ania hapa hii ni sheria na tunaipitisha na tukishaipitisha tayari ishakuwa sheria, kwa maana hiyo Mahakama na wao wanaangalia kwa mujibu wa sheria za nchi zinavyokwenda, sasa mimi ninavyoangalia nataka tuweke sehemu ambayo kuwa ina-*apply* litakapokuja kutokea tatizo kama hilo iwe pana njia ya kupita.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Pengine labda Mhe. Subeit sijamfahamu lakini likitokeza tatizo kama hilo inategemea ile ndoa ilikuwa ya kikristo ilikuwa ya kiislam au ilikuwa ya dini nyengine, sasa kama ilikuwa ni ya kikristo chochote kitakachopatikana pale kile kizazi kitakuwa ni cha kikristo na kama ni ya kiislam kile kitakachopatikana kizazi ni cha kiislam, kwa hivyo ikiwa kizazi ni cha kiislam ita-*apply* Kafala. Ikiwa kizazi cha kikristo wata-*apply* kifungu cha 76 ambacho ni kuwasili kwa hivyo hapo hapana matatizo na Mahakama itakuwa inatizama ile harusi ni ya namna gani, harusi ya kiislam wote ni waislam au harusi ya kikristo wote ni wakiristo ni rahisi. Kwa hivyo ni rahisi ukishakujua hivyo unajua kifungu gani cha sheria u-*apply* ili kuhusiana na kuwasili ama kafala, kwa hivyo haina matatizo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Zaidi yangu kuna mambo mawili hapa, kuna mwengine pengine hakuolewa kabisa kazalishwa tu mtoto ni mkristo tana

anamkimbia, kwa hivyo kuna mambo mawili hayo, atakuwa ni muislam kazalishwa na mkristo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwa misingi yetu ya kiislam ninavyofahamu mimi ikiwa hukuowa yule mtoto sio wako, kwa hivyo kama sio wako kwenye kafala huku atakuwa haingii itabidi mkubaliane sasa mama mtu na baba mtu kwa sababu sio wako kisheria kwa hivyo mtakavyokubaliana ndio itakavyokubalika.

Mhe. Spika: Yaani hapa ndio yule baba *biological.*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Haya Mhe. Mwenyekiti, ikiwa tunaona sheria zimekaa sawa tuendelee. *(Kicheko)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahasante Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hapo tuweke sawa kwa pande zote mbili, kwa mujibu wa sheria ya kiislam mtoto anayezaliwa hata kama wazazi wake wote ni waislam hawezi kuwa mkiristo, au hata kama wote ni waislam au wakiristo kizazi kinachozaliwa kwa mujibu wa kiislam kinakuwa ni cha kiislam, kama ni wakristo mpaka pale anapobatizwa na kupewa kipaimara.

Kwa hivyo suala hili lazima tulizingatie vizuri kwa sababu wanaweza kuwa wote ni wakristo, kwa sababu Mhe. Waziri amesema kwamba inategemea wale watu kama walikuwa waislam au wamekuwa wakristo, lakini kwa mujibu wa sheria ya kiislam watoto wote wanazaliwa waislam kama ni wakristo mpaka pale atakapobatizwa yule mtoto. Kwa hivyo pengine yule mtoto alikuwa hajabatizwa ni mdogo kwa hivyo tunapoiachia Mahakama iamue sijui itaamua vipi, kw sababu watoto wote wanaozaliwa kwa mujibu wa sheria za kiislam ni waislam.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri Mhe. Salmin Awadh alichosema ni sawa sawa na mimi sikwenda kinyume ya hicho, ikiwa watoto waliozaliwa au mtoto aliyezaliwa ni muislam hapa hatuchuki baba yake yule ni halali au sio halali ishu inayokuja ni muislam na hapa ndio kifungu kilivyosema. Masharti haya ya sehemu hii hayatahusu watu wanaofuata dini ya kiislam, sasa yule mtoto anayezaliwa tusahau wazee wake kama wameowana au hawakuowana lakini madhali ni waislam hapa hai-*apply* kwa sababu na yeye ni muislam. Lakini hapa ita-*apply* ikiwa wale ni wakristo au dini nyengine.

Kwa hivyo hiyo ni sawa sawa nakubaliana nae Mhe. Salmin Awadh Salmin hakuna matatizo ya kifungu hiki.

Kifungu cha	76	Uwezo wa kutoa amri ya kuwasili pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	77	Ombi la kuwasili
Kifungu cha	78	Ridhaa ya wazazi na walezi
Kifungu cha	79	Ridhaa nyengine
Kifungu cha	80	Masharti ya Amri ya Kuasili
Kifungu cha	81	Amri ya kumuweka mtoto kabla ya kuasili pamoja na marekebisho Yake.
Kifungu cha	82	Uelewa wa mtoto juu ya kuasili
Kifungu cha	83	Ombi la asiyekuwa mkaazi wa Zanzibar
Kifungu cha	84	Watoto ambao wamestahili kuasiliwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	85	Athari ya kuasili kwanye haki za uzazi pamoja na mrekebisho yake
Kifungu cha	86	Uhaulishaji mali baada ya kufariki bila ya wasia
Kifungu cha	87	Uhaulishaji kutokana na wasia
Kifungu cha	88	Masharti ya ziada juu ya kuhaulisha bila ya wasia na kwa wasia
Kifungu cha	89	Amri ya kuasili na taratibu za kimila
Kifungu cha	90	Daftari la watoto walioasiliwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	91	Marekebisho ya amri na kufutwa ndani ya madaftari
Kifungu cha	92	Kukatazwa kulipa na kutoa zawadi kwa kuasili pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	93	Taarifa itolewe ya kupeleka mtoto nje ya nchi
Kifungu cha	94	Uasili kwa wageni
Kifungu cha	95	Kanuni za kuasili
Kifungu cha	96	Matangazo yanayokatazwa pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA 9 HATUA MAALUM ZA KINGA KUHUSIANA NA WATOTO

Kifungu cha	97	Ajira ya mtoto
Kifungu cha	98	Haki ya Mtoto kufanya kazi
Kifungu cha	99	Kukataza ajira za kumtumia pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	100	Kukataza ajira za hatari
Kifungu cha	101	Haki ya Malipo
Kifungu cha	102	Kukataza ajira za shuruti pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	103	Matumizi

Kifungu cha	104	Usajili wa mtoto katika viwanda pamoja na mrekebisho yake
Kifungu cha	105	Utuliaji Nguvu
Kifungu cha	106	Adhabu kwa kwenda kinyume
Kifungu cha	107	Mafunzo ya Amali
Kifungu cha	108	Makosa kuhusiana na majengo yenye leseni na uuzaji wa vitu Vyenye madhara kwa watoto
Kifungu cha	109	Usalama wa mtoto katika sehemu za michezo na mapumziko Pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha	110	Kukataza utumiaji wa ngono pamoja na mrekebisho yake

SEHEMU YA 10 RIDHAA YA UTIBABU KWA KIDAKTARI NA UPIMAJI VVU

Kifungu cha	111	Ridhaa ya utibabu wa kidaktari na uperesheni wa upasuaji
Kifungu cha	112	Upimaji wa VVU pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	113	Nasaha kabla na baada ya kupima VVU pamoja na marekebisho Yake
Kifungu cha	114	Taafira ya hali ya mtoto kuhusu VVU / UKIMWI kuwa siri

SEHEMU YA 11 SKULI YA MAREKEBISHO

Kifungu cha	115	Skuli ya Marekebisho pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	116	Uteuzi wa bodi ya wakaguzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	117	Kazi za bodi na marekebisho yake
Kifungu cha	118	Amri zinazokubalika Skuli
Kifungu cha	119	Usitishaji wa amri za skuli za marekebisho
Kifungu cha	120	Uwezo wa Meneja kumpeleka mtoto Mahakamani
Kifungu cha	121	Kumtoa na kumhamisha mtoto kutoka skuli ya marekebisho
Kifungu cha	122	Uwezo wa kutunga kanuni pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA 12 UANZISHAJI WA MAAKAZI NA MAKAZI NA MATUNZO YA KUTWA

Kifungu cha	123	Ruhusa ya kuanzisha makaazi pamoja na

		marekebisho yake
Kifungu cha	124	Usimamizi wa nyumba za makaazi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	125	Kuanzishwa kwa Kamati pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	126	Ukaguzi wa nyumba za makaazi
Kifungu cha	127	Kupokea watoto katika nyumba za makaazi
Kifungu cha	128	Ufutaji wa nyumba za leseni za makaazi zilizoruhusiwa
Kifungu cha	129	Ombi la kuendesha kituo cha matunzo ya kutwa
Kifungu cha	130	Daftari la vituo vya matunzo ya kutwa
Kifungu cha	131	Ukaguzi wa vituo vya matunzo vya kutwa pamoja na marekebisho Yake
Kifungu cha	132	Kukataza baadhi ya watu kuendesha makaazi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	133	Makosa na adhabu

SEHEMU YA 13 MAMBO MENGINEYO

Kifungu cha	134	Uwezo wa Waziri kutunga Kanuni
Kifungu cha	135	Vituo vya Mafunzo na miongozo pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	136	Waendeshaji waliopo pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	137	Rufaa
Kifungu cha	138	Kanuni pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha	139	Kufutwa na kubakishwa pamoja na marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza zima imeupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukulali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokaataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Watoto 2011

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwamba mswada wa Sheria ya Watoto 2011 usomwe mara ya pili.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono, wanaokaataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mhe. Waziri lakini pia niwashukuru waheshimiwa wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa katika kufanya shughuli zetu katika baraza hili, Mswada huu ulikuwa ni mkubwa lakini wajumbe mmejitahidi kuchagia vizuri kiasi cha kwamba Mhe. Waziri nae amepata faraja kwa michango mingi lakini pia kwa ufafanuzi mkubwa ambao umetolewa na Mhe. Waziri Mwenyewe, Mwanasheria Mkuu pamoja na Waziri wa Katiba.

Nichukue nafasi hii basi kuwashukuru nyote kwa mashirikiano makubwa katika shughuli zetu hizi, kwa kuwa shughuli za leo zimekwisha sasa naahirisha kikao.

(Saa 12:20 jioni Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 30/03/2011
Saa 3:00 Asubuhi)